Nipashe
Jumatano Agosti 28, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580008
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


CCM ni kiwanda chenye hazina ya viongozi bora
Mipango ya mipaka ni kero uchaguzi serikali za mitaa
siasa
HABARI BORA NA KAMILIFU
Nipashe
Rais Abbas afika ukingoni
BAADA YA MIAKA 55
Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-mwisho
Afrika bado haijajipanga kuuingia mtangamano
Dk. Bashiru: Hakuna mwanaCCM atakayekwamishwa uchaguzi serikali za mitaa Ukurasa 14



# Mtaalamu atoa somo njia kujikinga na ajali za moto

UKURASA 2

UKURASA 13

# Mchujo mkali CCM

• **Ni** ule wa serikali za mitaa, watakaopitishwa kupitia mchakato mgumu kuanzia ngazi za matawi... *Ukurasa 2*



Mshtakiwa Khamis Luwongo maarufu kwa jina la Meshack (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani, kwa kumchoma moto, akiwa amefungwa pingu miguuni, akisindikizwa na Askari Magereza, baada ya kesi yake katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UKURASA 3

# Anayedaiwa kuua mke atoa kioja mahakamani

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

**MALINZI AIELEZA MAHAKAMA NAMNA ALIVYOIKOPESHA TFF**

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, ameiambia..

## DC aagizwa kuwachapa mijeledi watumishi

UKURASA 3

**MICHEZO** **AUSSEMS: HATUACHI KITU LIGI KUU NA FA** UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akitazama chombo muhimu katika kuunda mitambo ya kuzalisha umeme wa maji na gesi (turbines), wakati alipotembelea kiwanda cha kutengeneza mitambo ya kuzalisha umeme cha Tsurumi kinachomilikiwa na Kampuni ya Toshiba, nchini Japan jana. Wa pili kulia ni Meneja Mkuu wa kiwanda hicho, Shinya Fujitsuka. **PICHA: OWM**

## MAHOJIANO MAALUM

# Wagombea wa CCM kupita mchujo mkali uchaguzi wa serikali za mitaa

**Na Enock Charles**

SIKU chache baada ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kutangaza tarehe rasmi ya uchaguzi wa serikali za mitaa, Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimeeleza namna kitakavyopata wagombea wake katika nafasi mbalimbali zinazowaniwa.

Ijumaa iliyopita, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tamisemi, Seleman Jafo, alieleza mchakato wa uchaguzi huo utakavyokuwa na kutangaza rasmi kuwa uchaguzi huo utafanyika Novemba 24, mwaka huu.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jijini Dar es Salaam juzi, Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, mbali na mambo mengine, alizungumzia uchaguzi huo na kuweka wazi kuwa kutakuwa na mchujo mkali kupata wagombea wa chama hicho.

Hata hivyo, Dk. Bashiru alisema mchakato utazingatia misingi ya kidemokrasia na kwamba utakuwa wazi na fomu zitatolewa bure.

Katika mahojiano hayo, kigogo huyo wa CCM pia alitoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali ukiwamo utekelezaji wa ahadi ya chama chake ya kugawa Sh. milioni 50 kila kijiji/mtaa.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa:-

**SWALI: Kipenga cha uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu tayari kimepulizwa. Utaratibu wa kuwapata wagombea wa CCM katika uchaguzi huo ukoje?**

**DK. BASHIRU:** Kwa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, wanachama wote watapiga kura kwenye tunachokiita mkutano mkuu wa wanachama wote wa tawi.

Kwa hiyo, kura za maoni zitapigwa katika ngazi ya tawi katika siku ya kupiga kura ambayo itapangwa. Kura za maoni kwa wagombea ngazi ya kijiji na mtaa, wanaCCM wote watapiga kura zao za maoni wakiwa katika matawi ya vijijini au matawi ya mitaa.

Kwa upande wa mjini kura zitapigwa kule ambako wanaishi na ambako ni wanachama kwa mujibu wa Ibara ya 35(6) ya Katiba yetu, na kwa upande wa vitongoji, kura za maoni zitapigwa na wanachama wote wa CCM katika kitongoji kinachohusika.

Lakini, upo utaratibu wa kuwapata wagombea wa kupigiwa kura za maoni ambapo mgombea yeyote wa CCM kabla ya kupigiwa kura za maoni, atajadiliwa kwanza na kamati ya siasa ya tawi lake.

Baada ya hapo, kamati ya siasa ya kata yake itafikiria na kuteua majina ya wana CCM wasiozidi watatu kwa kila kitongoji walioomba kugombea uenyekiti wa kitongoji ili wakapigiwe kura za maoni na mkutano wa wanachama wote wa CCM wanaoishi katika kitongoji hicho.

Kwa hiyo, kutakuwa na kujadiliwa wanaoomba halafu baadaye yatateuliwa majina matatu ndiyo yatakwenda kupigiwa kura kwa upande wa kitongoji.

Na mgombea yeyote wa CCM anayetaka kuingia kwenye chombo cha dola kwa nafasi ya uenyekiti wa kijiji ama uenyekiti wa mtaa, kabla ya kupigiwa kura za maoni atajadiliwa kwanza na kamati ya siasa ya tawi lake na kamati ya siasa ya kata yake na hatimaye kamati ya siasa ya wilaya itafikiria na kuteua majina ya wana CCM wasiozidi watatu kwa kila kijiji ama mtaa walioomba kugombea uenyekiti wa kijiji ama mtaa ili wakapigiwe kura za maoni na mkutano wa wanachama wote katika tawi husika.

Mikutano ya wanachama wote kwenye matawi ndiyo itakayohusika kwenye kura za maoni lakini mchakato utaanza kwa kuwafikiria waombaji katika ngazi husika na fomu tayari tumeshaziandaa na tunaendelea kuzisambaza.

Kwa hiyo, sharti la kwanza lazima awe mwanachama, lakini baadaye katiba na kanuni za CCM ndiyo zitakazoongoza. Na kanuni hizi ni za Juni mwaka huu, zilipitishwa na Halmashauri Kuu Juni katika kikao kilichopita na katiba hii ni ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2017.

Kwa ufupi, mchakato wetu ni wa kidemokrasia, utakuwa wazi na fomu ni bure tofauti na za ubunge na udiwani ambazo ni za gharama. (Fomu ya kuwania udiwani imekuwa ikitolewa kwa Sh. 10,000).

**SWALI: Kuna wanachama wengine hawajawahi kugombea nafasi yoyote ndani ya CCM na wanataka kugombea safari hii, na wengine ndiyo kwanza wamejiunga na chama. Huoni kwamba watakwamishwa na waliokuwapo?**

**DK. BASHIRU:** Uhai wa Mwanachama siyo umri kama mtoto mdogo katika kupiga kura za kikatiba ambako ni lazima uwe na umri wa miaka 18.

Kuwa mwanachama unapata haki zinazolingana bila kujali umetumia muda gani kwenye chama, ukishapitia mchakato wa kuomba uanachama, ukajadiliwa

INAENDELEA UK. 8

# Mtaalamu atoa somo njia kujikinga na ajali za moto

**Na Jovin Lamwel**

KIKOSI cha Zimamoto nchini kimeeleza njia za kujikinga na ajali ya moto wa mlipuko wa mafuta kwa kutahadharisha watu wasikimbie ili kuepusha kasi ya kuwaka na kujikinga ili hewa chafu isiingie kwenye mfumo wa upumuaji.

Mtendaji wa Kikosi cha Zimamoto, Sajenti Semba Maingu, alitoa tahadhari hiyo wakati akitoa mafunzo ya Zimamoto kwa wafanyakazi wa The Guardian Limited (TGL), jijini Dar es Salaam, jana.

Alisema mtu alinayeungua na moto anapokimbia anaruhusu moto huo kuongeza kasi ya kuwaka na vile vile kuvuta hewa chafu inayoingia kwenye mfumo wa upumuaji na kuharibu mapafu.

Alikuwa akitoa mfano wa ajali ya lori la mafuta lililolipuka moto eneo la Msavu, mjini Morogoro hivi karibuni ambayo mpaka sasa imesababisha vifo zaidi ya watu 100 na majeruhi wanaoendelea kupatiwa matibabu.

"Tumepoteza watu wengi kwa sababu ya kukosa uelewa wa kujiepusha na moto, wengi walivuta hewa ya moto na kuharibu mfumo wa hewa," alisema.

Alisema matukio ya milipuko ya moto yanasababisha vifo vingi kutokana na watu kutokuwa na uelewa wa kujihami na badala yake kukimbilia eneo la tukio.

Sajenti Maingu alisema idadi kubwa ya watu hawana ufahamu wa maana ya 'open flame' yaani moto unaotembea. "Moto huu ni hatari sana kwa kuwa huleta madhara makubwa sana."

Akielezea njia za kujikinga, Sajenti Maingu alisema, jambo la kwanza ni kuhakikisha eneo lote lililozingirwa na moto linamwagiwa 'fire cover' yaani dawa ambayo itazuia moto huo kusambaa zaidi.

Pia, alisema waokoaji wanatakiwa kukaa mbali na eneo la mlipuko na kutoa taarifa sahihi kwa kikosi cha Zimamoto haraka.

"Katika harakati za kutaka kujiokoa wengi wamejikuta wakiteketezwa na moto ikiwamo kupata majeraha na vifo, hali hii imesababishwa kutojua mbinu hizo kama vile kukaa mbali na eneo la mlipuko au 'open flame' moto wa wazi unaosababishwa na mafuta. Kupumua au kuvuta hewa yenye petroli inaangiza moto tumboni na kuharibu mapafu, yaani mfumo wa upumuaji pia hewa chafu iitwayo carbon monoxide na kutotoa taarifa sahihi kwa haraka," alisema.

Akielezea zaidi jinsi ya kuudhibiti moto huo, alisema unaweza kuzimwa kwa urahisi zaidi iwapo kitatumika kifaa maalumu cha kuzimia moto

INAENDELEA UK. 8

## HABARI KITAIFA

# Waziri ampa DC kazi ya 'kucharaza bakora'

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

WAZIRI wa Nchi ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amemwagiza Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Vumiliana Nyamoga, kuwachapa viboko watumishi wake wa idara ya ardhi ili waweze kupima viwanja kwa kasi kulingana na mahitaji.

Jafo aliyasema hayo jana alipokuwa akishuhudia utiaji saini kati ya Jiji la Dodoma na makandarasi watakaojenga mradi wa Hoteli ya Jiji la Dodoma pamoja na jengo la kitega uchumi katika mji wa kiserikali Mtumba.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino imekuwa ikisuasua katika upimaji wa ardhi, hali ambayo imekuwa ikileta ugumu katika uwekezaji wa miradi mbalimbali ya serikali.

"Raisi ametoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Uhuru, lakini pia tunajenga katika eneo ambalo halijapimwa," alisema na kuongeza:

"Nimekuwa nikipiga kelele kila siku na fedha tumewapa, lakini hakuna kitu hivyo mheshimiwa mkuu wa wilaya nenda kawachape viboko watu wako wanakutia aibu"alisema Jafo.

Aidha katika zoezi hilo la utiaji saini Jafo alilipongeza jiji la Dodoma kwa kubuni miradi ya maendeleo ambayo italisaidia katika kuongeza mapato.

"Hii miradi ya hoteli pamoja na jengo la uwekezaji katika mji wa kiserikali Ihumwa itawasaidia katika kuwa na chanzo cha mapato ambacho ni endelevu na kuweza kuondokana na unyafuzi wa mapato na kuendelea kuongoza kama ambavyo mnafanya sasa," alisema.

Jafo alizitaka halmashauri zote nchini kuiga namna ambavyo Jiji la Dodoma limeweza kusimamia vyanzo vya mapato na kukusanya juu ya malengo.

Pia, aliagiza halmashauri zote kuhakikisha kuwa zinatoa zabuni za ujenzi wa miradi ya maendeleo kwa makandarasi wenye uwezo ambao watakamilisha ndani ya mikataba na kwa ubora.

Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwini Kunambi, akizungumzia juu ya miradi hiyo miwili, alisema itawasaidia kuwaongezea uwezo wa kujitegemea.



Wakazi wa Mtaa wa Wapiwapi B, Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wakitafuta majina yao na namba maalumu za vitambulisho vya uraia kwenye karatasi ya orodha ya majina ya vitambulisho vya taifa (Nida), ambapo majina hayo yameanza kubandikwa, katika ofisi ya kata ya Napupa iliyopo Sokosela mjini Masasi jana. **PICHA: HAMISI NASIRI**

# Anayedaiwa kumuua mke aibua kituko tena kortini

**Na Hellen Mwango**

MSHTAKIWA Khamis Luwongo, maarufu kwa jina la Meshack (38), anayetuhumiwa kumuua mkewe kwa kumchoma moto na magunia mawili ya mkaa, Naomi Marijani, ameibua hoja mpya baada ya kuiomba mahakama iitishe simu zake ahamishe zaidi ya Sh. milioni tano.

Luwongo aliiwasilisha maombi hayo jana kwamba simu zake mbili zenye laini ya Tigo ina Tigopesa zaidi ya Sh.milioni nne na Airtel ina zaidi Sh. milioni moja.

Madai hayo aliyatoa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi Salum Ally wakati kesi yake ilipopangwa kwa ajili ya kutajwa.

Awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alidai kuwa kesi hiyo imepangwa kwa ajili ya kutajwa na kwamba upelelezi wake bado haujakamilika.

Hata hivyo, mshtakiwa aliomba nafasi ya kuzungumza na alipokubaliwa alidai kuwa ana mambo mawili.

Kwanza, anaomba nakala hati ya mashtaka yanayomkabili, pili, kibali cha mahakama kuitisha simu zake mbili kati ya nne zinazoshikiliwa na polisi ili ahamishe fedha kwenda kwenye simu ya ndugu yake.

Alidai kuwa pamoja na kwamba hafahamu mahali mtoto wake alipo, anataka kuzitoa fedha hizo kuhamishia kwenye simu ya ndugu yake kwa ajili ya kumlipia ada mtoto huyo.

Luwongo alidai kuwa laini ya Tigo ina zaidi ya Sh. milioni nne na Airtel ina zaidi ya Sh. Milioni moja kwa hiyo jumla ana zaidi ya Sh. milioni tano.

"Mheshimiwa Hakimu, ninaomba maelekezo simu ziletwe mahakamani nitoe neno la siri ili fedha hizo nihamishie kwa ndugu yangu kwa sababu laini zisipotumika muda fulani zinafutwa," alidai Luwongo.

Hata hivyo, Wankyo alipinga mahakama kusikiliza ombi la mshtakiwa kwa sababu kwanza, kesi hiyo iko katika usikilizwaji wa awali, hivyo mahakama haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Pili, simu anazoziomba mshtakiwa ni sehemu ya kesi hiyo ya mauaji na zinategemewa kutumika kama kielelezo wakati wa kusikilizwa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam.

"Mheshimiwa ni rai yetu kwa mahakama kutokufanyia kazi maombi yake kwa sababu kesi hii inasikilizwa na Mahakama Kuu. Nakala ya hati ya mashtaka nilishampa siku ya kwanza lakini nitampa nyingine ila suala la simu asubiri kesi isikilizwe,"alidai Wankyo.

Hakimu alisema mahakama yake haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo na mshtakiwa asubiri upelelezi utakapokamilika atawasilisha malalamiko yake mbele ya Jaji atakayepangiwa kusikiliza kesi yake.

Alisema kesi hiyo itatajwa Septemba 10, mwaka huu, na mshtakiwa ataendelea kukaa mahabusu.

Katika kesi hiyo, mshtakiwa anatuhumiwa kwa kosa moja la mauaji kinyume cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Na. 196 Sura ya 16 kama kilichofanyiwa marejeo mwaka 2002

Katika kesi hiyo ya mauaji Na. 4 ya mwaka 2019, Luwongo ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole eneo la Kigamboni alimwua Naomi Marijani.

Mshtakiwa hakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji.

International School of Tanganyika
Challenge | Support | Inspire

Vacancies Available

Administrative Officer

Department: Secondary School
Reports to: Principal - Secondary School

Teacher Assistant

Department: Elementary School
Reports to: Principal - Elementary School

Please visit:
www.istafrica.com/about-us/working-at-ist
For full job description and application instructions.

215391702

# Malinzi aeleza alivyoikopesha TFF mamilioni

**Na Hellen Mwango**

RAIS wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Jamal Malinzi, katika siku ya tatu ya utetezi wake, amedai mahakamani kwamba alikuwa akilikopesha shirikisho hilo bila masharti na kwamba kati ya 2014 na 2016 alilikopesha Dola za Marekani 298,000 na Sh. 340,000.

Malinzi anayekabiliwa na mashtaka ya kughushi na kutakatisha fedha, amedai kuwa aliikopesha TFF kwa nyakati tofauti bila kuilipisha riba na kwamba alilipwa deni kwa mafungu kulingana na upatikanaji wa fedha katika shirikisho hilo.

Ushahidi huo uliendelea jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi, Maira Kasonde.

Mbali na Malinzi, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Selestine Mwesigwa, Mhasibu wa TFF Nsiande Mwanga na Karani Flora Rauya.

Akiongozwa na Wakili Richard Rweyongeza, Malinzi alidai kuwa akiwa kiongozi na familia ya TFF, aliwajibika kutoa fedha zake ikiwamo kuitumia Dola za Marekani 7,000 timu ya taifa ya Tanzania (Taifa Stars) ilipokwama nchini Zimbabwe.

Alidai kuwa si yeye peke yake aliyeikopesha TFF hata shahidi wa sita wa Jamhuri, Ahmed Mgoyi, katika vielelezo vya Jamhuri vya kesi hii iko risiti ilioonyesha amelipwa Sh. milioni 55 baada ya kulikopesha shirikisho hilo.

"Mheshimiwa Hakimu, nilikuwa naikopesha TFF bila dhamana yoyote wala masharti ikiwamo kuilipisha riba bali nilijitolea na walinilipa kwa mafungu pale walipopata fedha," alidai na kuongeza:

"Utaratibu wa kuikopesha TFF ni wa kawaida kama ilivyo kwa vilabu (klabu) vya (za) mpira nchini akiwamo Mohamed Dewji kuidai Simba Sh. bilioni sita kwa ajili ya matumizi yake mbalimbali. Mheshimiwa hakimu mimi ni wa kwanza kushtakiwa kwa sababu ya kukopesha timu zilizokuwa chini yangu," alidai Malinzi.

Alidai kuwa alikamatwa Juni 27, 2017 akiwa kwenye usaili wa nafasi ya mgombea urais na alikaa mahabusu ya polisi mpaka Juni 29, mwaka huo, aliposomewa mashtaka yanayomkabili kwa mara ya kwanza na kwamba Julai Mosi, mwaka huo alitenguliwa wadhifa wake wa urais wa TFF.

Alidai kuwa makamu wake, Wales Karia, aliitisha mkutano wa Kamati ya Utendaji Julai Mosi, 2017 na walimwengua nafasi yake, walikata jina lake kama mgombea urais na hatimaye waliivunja kamati ya uchaguzi na kumpitisha Karia kuwa mgombea pamoja na kuteua kamati mpya ya uchaguzi.

Alidai kuwa kitendo cha kumwengua na kuvunja kamati hiyo ni kinyume cha kanuni na katiba ya TFF.

Malinzi ambaye aliomba kibali cha mahakama kunywa fundo kadhaa za soda aina ya Coca Cola na kukubaliwa, alidai kuwa mwenye mamlaka ya kuitisha mkutano wa kamati ya utendaji ni Rais na si vinginevyo

"Kwa mujibu wa katiba ya TFF Rais ataenguliwa endapo tu atajiuzulu, kukosa vikao vinne vya Kamati ya Utendaji, kutokushiriki kazi za TFF na kufungwa au kuhukumiwa au kulipa faini.

"Lakini mimi niko mahabusu nimeenguliwa kinyume cha katiba yetu," alidai Malinzi.

Akizungumzia alivyolipwa madeni na kupewa risiti, shahidi alidai kuwa Mhasibu Mkuu, Daniel Msangi, alijiridhisha matumizi yake ndipo alilipwa deni lake na shirikisho hilo.

Alidai kuwa alipokuwa anapewa fedha walikuwa wakimpa risiti kwa majina yake na kwamba aliendelea kutoa fedha hadi alipokamatwa mwaka 2017.

Mshtakiwa huyo alidai kuwa kati ya risiti alizo nazo zilitiwa saini na Hellen Adam ambaye alikuwa shahidi wa 10 wa upande wa mashtaka na Kaimu Mkurugenzi wa Fedha, Msangi, ambaye alikuwa shahidi wa sita. Risiti nyingine haikuwa na saini lakini kwenye taarifa ya benki ilionyesha imeingizwa kama mkopo.

Alidai risiti zote zinatunzwa na idara ya uhasibu ya TFF na kwamba amekuwa akilipwa kwa mafungu mafungu kutokana na hali ya shirikisho hilo kuwa mbaya kiuchumi.

Malinzi aliendelea kudai kuwa idara ya fedha ilikuwa ikikaa na kuangalia namna ya kumlipa kutokana na kile wanachokipata.

Kesi ya msingi namba 213/ 2017 washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha wa Dola za Marekani 173,335.



Wafanyausafi wakiwa wamejipumzisha chini ya mti kando ya Barabara ya Morogoro, eneo la Magomeni Mwembechai, jijini Dar es Salaam jana, kabla ya kuendelea na kazi yao. **PICHA: JOHN BADI**






# Makonda atamani bima afya kwa wote

**Na Mary Geofrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amewataka Watanzania kujiunga na Mfuko wa Bima ya Afya ili kuwa na uhakika wa matibabu.

Amesema anatamani kungekuwa na utaratibu wa wagonjwa wasipatiwe matibabu hadi wawe na bima ya afya ili kuhamasisha jamii kuona umuhimu wa kujiunga na huduma hiyo.

Aliyasema hayo jana alipomtembelea mkazi wa Bukoba mkoani Kagera, Ashraf Patrick, aliyelazwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), akipatiwa matibabu ya uvimbe kwenye shavu ambao umegundilika kuwa ni kansa.

Kijana huyo alisafirishwa na Makonda kwenda MNH kwa matibabu baada ya picha yake kusambaa mwenye mitandao ya kijamii akiomba msaada kutokana na kukosa fedha za matibabu.

"Nichukue nafasi hii kuhamasisha Watanzania kuwa na utaratibu wa kuwa na bima za matibabu kwa sababu ugonjwa kama huu unaweza kutibiwa kwa bima yako.

Natamani kuona watu wanaoenda hospitali wasipatiwe matibabu mpaka wawe na bima ili iwe ni njia ya kuhamasisha wananchi kuona umuhimu wa kuwa na bima ingawa watu watakasirika sana lakini itakuwa na manufaa kwa sababu watu hawana.

utaratibu kufanya mambo mpaka kuwapo na vitisho," Makonda alisema.

Alisema kijana huyo kama angekuwa na bima ya afya angeweza kupatiwa matibabu mapema na kuondoka na adha aliyoipata wakati wote wa kuugua kwake.

"Unaweza kukuta kukata bima ni gharama kubwa ila huwezi kuona umuhimu wake mpaka uugue ndipo utafahamu umuhimu wa bima hii," Makonda alisema.

Alisema kwa Mkoa wa Dar es Salaam wana bima ya CHF iliyoboreshwa ambayo familia ya watu sita wanalipa Sh. 150,000 na mtu mmoja Sh. 40,000, lakini bado watu hawachangamkii fursa hiyo.

Aliwataka Watanzania kujenga utamaduni kwa kusaidia watu wasio na uwezo ili kupata huduma za matibabu kwa sababu ni matendo ya huruma yanayompendeza Mungu.

SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




SHABIKI MKUU WA TAIFA STARS




# Wenye vyeti feki kiama kingine chaja

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imewaagiza wakuu wa taasisi za umma na maofisa utumishi nchini kumaliza uhakiki wa vyeti vya watumishi wote vya ufaulu kidato cha nne, sita na ualimu baada ya kubaini uwapo wa watumishi wenye vyeti vya kughushi katika baadhi ya halmashauri na taasisi za umma.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Dk. Laurean Ndumbaro, alitoa agizo hilo ikiwa ni sehemu ya msisitizo wa utekelezaji wa maelekezo ya Rais John Pombe Magufuli, aliyoyatoa wakati akizindua Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Novemba, 2015 akitaka utumishi wa umma nchini uwe wa uadilifu, unaowajibika na wenye sifa stahiki.

Alifafanua kuwapo kwa taarifa za watumishi wenye vyeti vya kughusi mpaka sasa kuunaashiria kuwa kuna baadhi ya wakuu wa taasisi na maofisa utumishi hawajalipa uzito agizo hilo la kuwaondoa watumishi wenye vyeti vya kughushi.

"Mpaka sasa bado tunapata taarifa za baadhi ya watumishi wenye vyeti vya kughushi kuendelea na utumishi wa umma katika baadhi ya halmashauri na taasisi, hivyo inatulazimu kuwasilisha vyeti vyao Baraza la Mitihani kwa ajili ya uhakiki badala ya kuendelea na utekelezaji wa majukumu mengine ya kitaifa," Dk. Ndumbaro amesisitiza.

Dk. Ndumbaro pia aliwataka watumishi wa umma nchini kuwajibika kwa serikali na wananchi pindi wanapofuatwa huduma katika taasisi zao ili kujenga uhusiano mzuri kati ya serikali na wananchi.

Alitoa wito kwa wakuu wa taasisi kuhakikisha wanasimamia nidhamu mahala pa kazi ili watumishi wa umma waweze kutumia muda wao wa kazi vizuri kwa kutoa huduma bora kwa umma.

# Upelelezi kesi ya mawakala ATCL waiva

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam imeambiwa na upande wa Jamhuri kwamba upelelezi wa kesi inayowakabili Mawakala 10 wa Shirika la Ndege Tanzania (ATCL) kwa madai ya kutakatisha Sh. Milioni 10.8 umekamilika.

Kesi hiyo ilitajwa jana katika mahakama hiyo mbele ya Halimu Mkazi Mwandamizi Salum Ally.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa na upelelezi wake umekamilika.

Alidai kuwa upande wa Jamhuri unasubiri nyaraka kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kwa ajili ya kuendelea na kesi.

Hakimu alisema kesi hiyo itaendelea leo baada ya upande wa Jamhuri kukamilisha nyaraka zao muhimu.

Washtakiwa hao ni Fabian Ishengoma (34), Adam Kamara (27), Marlon Masubo (29), Neema Kisunda (24), Alexander Mgalonzo (29) na Tunu Kiluvia (32).

Wengine ni Jobu Mkumbwa (30), Mohammed Issah (38), Godfrey Mgomela, Absalom Ambilikile na Janeth Lubega.

Katika kesi ya msingi, ilidaiwa kuwa kati ya Machi 10 na Oktoba 9, mwaka jana, mahali tofauti jijini Dar es Salaam na Mwanza, washtakiwa kwa pamoja wakiwa mawakala wa ATCL walilisababishia shirika hilo hasara ya Sh. 10,874,280.




Mkurungenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi (kulia), akibadilishana nyaraka na Mkurungenzi wa Kampuni ya ujenzi ya Mohammad Builder Ltd, Mhandisi Taher Jaffereji, baada ya kusaini mkataba wa zaidi ya Sh. bilioni 27 wa ujenzi wa majengo ya kitenga uchumi katika Jiji hilo, katika hafla iliyofanyika jana. Katikati ni Meya wa Jiji hilo, Prof. Davis Mwamfupe. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Waziri Mkuu aipigia debe Toshiba kuwekeza nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekutana na kufanya mazungumzo na viongozi wa kampuni ya Toshiba nchini Japan na kushawishi kufungua ofisi kubwa na viwanda vya bidhaa za umeme nchini.

Majaliwa aliyasema hayo leo baada ya kutembelea Makumbusho ya Sayansi ya kampuni ya Toshiba na kiwanda cha kutengeneza mitambo ya kuzalisha umeme cha Tsurumi kinachomilikiwa na kampuni hiyo.

Akizungumza na viongozi wa kampuni hiyo, Waziri Mkuu aliwashawishi kufungua viwanda vya kutengeneza bidhaa mbalimbali za kielektroniki kama vile redio, televisheni, pasi na viwanda vingine watakavyoona vinafaa kujengwa nchini.

Aliwahakikishia viongozi hao kwamba hawatajuta kuwekeza Tanzania kutokana na sera nzuri na mazingira mazuri ya uwekezaji na biashara pamoja na soko la uhakika la bidhaa zitakazozalishwa kwa kuwa Tanzania imezungukwa na nchi nyingi.

"Wawekezaji wote wanaokuja kuwekeza Tanzania wakiwamo na wa kutoka Japan pamoja na kampuni ya Toshiba, watambue kwamba serikali imeboresha mazingira ya uwekezaji na kuyafanya yawe rafiki. Nina uhakika wawekezaji watakaoamua kuwekeza Tanzania hawatajutia uamuzi wao huo," alisema.

Waziri Mkuu alisema ujio wa kampuni kubwa kutoka Japan, utawapa Watanzania fursa ya kujifunza teknolojia mpya na namna bora ya uendeshaji wa biashara unaozingatia viwango vya kimataifa.

Mkurugenzi wa Makumbusho ya Sayansi ya Toshiba, Takano Lwakiri, alimwambia Waziri Mkuu kuwa kampuni yake iko tayari kupanua ofisi yake ya Tanzania na kufungua biashara, lakini akaomba yafanyike mazungumzo yatakayotoa dira sahihi ya kufanikisha jambo hilo.

TAIFA STARS vs BURUNDI
SEPTEMBA 8, 2019 • UWANJA WA TAIFA

HAIUZWI KWA WALIO NA UMRI CHINI YA MIAKA 18. TAFADHALI KUNYWA KISTAARABU.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mtoto kubwia mihadarati Zanzibar lifanyiwe kazi

**MAMBO** mengine yamekuwa yakishangaza na kustua, lakini hili la mtoto visiwani Zanzibar kubwia mihadarati na kulazwa hospitalini Mnazi Mmoja kwa siku kadhaa linahofisha na kushangaza zaidi.

Mtoto huyu mdogo alielezwa na mama yake kuwa aliokota dawa hizo jirani na nyumbani kwao na kubwia unga ambao ulimfanya azirai na kuuumia kimwili na kisaikolojia.

Watoto kuokota na kula dawa mitaani hili si jambo la kupuuzwa hata kidogo. Na kwa wataalamu walioko Mnazimmoja mtoto huyu anahitaji tiba zaidi kwa sababu mihadarati inaathiri ubongo na ina madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kuchanganyikiwa na kuwa na maruweruwe.

Kutumia dawa hizo kukishaleta maruweruwe kwa mtoto kunasababisha kuvurugika kwa mawazo yake, kujisikia vibaya ambako kunaweza pia kumwathiri nguvu za macho, hisia na hata mfumo mzima wa namna mwili unavyofanyakazi.

Si wakati wa kutoa mlolongo wa matatizo yanayotokana na kutumia dawa za kulevya kwa watoto, bali ni muda wa kuangalia ni kwa jinsi gani dawa za kulevya zinavyokuwa tishio kwa jamii zetu kiasi kwamba mihadarati inaweza kuanguka na kuzagaa mitaani kama ilivyotokea Zanzibar.

Ni wazi kuwa kuna haja ya kuanzisha msako wa vijiwe vya kuuza na kusambaza dawa hizo mitaani ili kuujua ukweli na hali halisi ya kusambaa dawa hizo hata kufikia pengine hatua ya kete kuangushwa mitaani ili wateja wazipate lakini matokeo yake zinaangukia mikononi mwa watoto wachanga kama ilivyotokea visiwani.

Uchunguzi hadi kuujua ukweli ni suala hilo ni muhimu ili watu na jamii iwe salama kwa vile wakati mwingine tunashawishika kuamini kuwa wapo baadi ya wauza mihadarati hiyo, wanaisambaza kwa wateja wao ili wawe salama bila kukamatwa pengine ndiyo maana utaratibu huo ukatumika. Ila ukweli wa suala hili ni lazima uchunguzwe na ikiwezekana ufahamike.

Biashara ya dawa hizo haiwezi kuzuka kama giza au mwanga, ni lazima kunakuwa na wahusika na mkono wa watu hao unaweza ukakamatwa iwapo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), ifanye misako na mikakati kama ilivyotokea kwa Tanzania Bara.

Ni wazi kuwa msako wa wateja na waathirika wa mihadarati wanafahamika maeneo wanayoishi mitaani na kama ilivyofanyika Bara na Unguja pia inawezaekana. Huenda kuna watumiaji wengi ambao wanakula dawa hizo hadi zikazagaa mitaani.

Kwa ujumla suala la tatizo la dawa za kulevya kuwafikia watoto halipendezi na wakati polisi wakiendelea na uchunguzi kwa upande wao, jambo la muhimu ni wazazi kuwalinda watoto na ikibidi kuangalia mazingira wanayochezea na vitu wanavyookota na kuvila.

Kilichompata mtoto huyu kinaweza kuwapata watoto wengine si Visiwani hata Bara pia na hiyo ni changamoto nyingine inayoelekeza kutafiti zaidi iwapo watoto wa wadogo wa mitaa hiyo walishawahi kuziona kete ama kutumiwa kubeba kete hizo kuzipeleka kwa wateja.

Hii inawezekana kwa kuwa watoto wadogo wanaweza kutumiwa na wauza mihadarati kuwafikia wateja kwa sababu si rahisi polisi, mzazi au mwanajamii yeyote kumhofia mtoto kuhusika na biashara hiyo.

Pengine kuanguka kete ya dawa hizo si jambo rahisi kwa vile watumiaji wana thamini sana kilevi hicho kwa hiyo kitendo cha kudondoka dawa hizo mitaani hata kuangukia mikononi mwa watoto wadogo ni kitu kinachotuachia maswali mengi.

Lakini la muhimu ni wazazi kuwalinda watoto, mazingira wanayoishi na kucheza iwapo kuna vijiwe vinavyoshukiwa kuwa karibu na nyumbani ni muhimu pia kuchunguzwa na kuangalia ni kwa namna biashara hiyo inavyofanyika mitaani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Jamii ichukue hatua kulinda maadili ya wanafunzi shuleni

**KATIKA** mfumo wa maisha huwa ni jambo la kawaida mtoto kutunzwa au kulelewa na wazazi hata na ndugu akielekezwa kuzingatia maadili mema, ambayo yanalenga kumfanya awe mtu mwema katika jamii.

Hivyo iwapo watoto watazingatia mfumo huo wa malezi, mwisho wa siku wanaweza kuwa raia wema na wenye manufaa kwa familia zao, jamii na taifa kwa ujumla.

Hata hivyo, mfumo unazidi kubadilika kutokana na migongano ya maisha, uchumi duni, umaskini, ufukara na utandawazi katika zama hizi, hatua inayosababisha madhara makubwa kwa watoto.

Miongoni mwa madhara hayo ni mmomonyoko wa maadili, unaosababisha watoto wakiwamo wanafunzi kujiingiza katika vitendo vibaya vinavyoweza kuwaharibia ndoto zao za baadaye.

Wiki iliyopita, wadau mbalimbali wa maendeleo ya mtoto walikutana katika warsha iliyolenga kuwa na mkakati wa kutambua mbinu za kuwasiliana kwa ajili ya kukomesha vitendo vya ukatili kwa watoto.

Warsha hiyo ilioandaliwa na taasisi ya Ekama Development Foundation Tanzania, ilishirikisha wadau 120 ambao ni wanafunzi, walimu, wazazi, viongozi wa serikali za mitaa kutoka wilaya za Temeke na Kigamboni.

Ilidaiwa na baadhi ya wanafunzi na walimu kwamba wapo baadhi ya wanafunzi ambao hufanyiana vitendo vya ukatili (kulawitiana) wenyewe kwa wenyewe.

Kutokana na madai hayo, viongozi wa dini waliombwa kusaidia kukemea mmomonyoko wa maadili ili jamii ilirudi kwenye mstari unaozingatia malezi mema badala ya kukaa kimya huku watoto wakiendelea kuharibika.

Ofisa Elimu ya Msingi wa Wilaya ya Temeke, Mectilda Rukoijo, anasema mmomonyoko wa maadili kwa vijana, hasa wanafunzi wa shule za msingi usipodhibitiwa kikamilifu utasababisha madhara makubwa ikiwa ni pamoja na kuwa na taifa lisilo na maadili.

Muungwana anawaasa wazazi kutafakari mienendo yao ili kumaliza tatizo hili ambalo linakwenda kinyume na maadili.

Kuwapo kwa vitendo hivyo vya mmomonyoko maadili shuleni maana yake ni kwamba chanzo kipo, hivyo ni wajibu kwa wazazi kutafakari mienendo yao au malezi yao kwa watoto.

Pamoja na kwamba juhudi mbalimbali za kulinda maadili zimekuwa zikichukuliwa na wadau mbalimbali wa haki za watoto, bado wazazi wana sehemu kubwa ya malezi bora kwa watoto wao.

Wazazi wasipochukua hatua kwenye suala hili wanaweza kusababisha vijana wao kujikuta wakiwa na maambukizi ya virusi ya Ukimwi, kwani tatizo hilo ni kubwa haliwezi kufumbiwa macho.

Kila mzazi anatakiwa kufuatilia na kujua mwenendo wa mtoto wake na kuurekebisha pale anapoona unakwenda kinyume kwani shule ni sehemu ya kupata elimu, si kufanyia mambo ya mmomonyoko wa maadili.

Sidhani kwamba wazazi na walezi wanaweza kukwepa lawama au kujitetea katika hili kwani ni muhimu ijulikane wanakojifunzia vitendo hivi watoto wao.

Kama watoto wanaachwa huru kupita kiasi, basi wazazi wajue kuwa mtindo huo unachangia kuwapo kwa vitendo hivyo, ambavyo kama nilivyosema, madhara yake ni makubwa kwa maisha yao ya baadaye.

Kwa mazingira ya aina hiyo, ipo haja sasa wazazi kuwakagua watoto wao mara kwa mara kwani wanaweza kufanyiwa ukatili na mtu wa karibu au wenzao shuleni na kujikuta wakiharibika.

Wazazi ni nguzo muhimu ya malezi kwa watoto wao, lakini yanapolega, maana yake ni kuharibika kwa mtoto.

Muungwana anatafakarisha kwa mfano suala la baadhi ya wazazi kulala chumba kimoja na watoto wao wakubwa, nini hatma yake?

Wengine wanaacha watoto wakiangalia hata picha za ovyo kwenye vibanda vya kuonyeshea video mitaani na kwa mazingira kama hayo ni lazima vitendo vya mmomonyoko wa maadili vitatokea.

Viongozi wa dini wana umuhimu wao katika suala zima la kukemea tabia hiyo ili kulinda watoto dhidi ya mmomonyoko, ambao unaweza kusababisha kukawa na taifa bovu la baadaye.

## HABARI KITAIFA

# Hii kero Mikese hadi lini?

**Ndugu Mhariri**

*SISI wananchi tunaoishi Kitongoji cha Ukomanga, Kijiji cha Fulwe, Kata ya Mikese, mkoani Morogoro tunaleta masikitiko yetu makubwa kwako ili wahusika wapate kulielewa hili tukitegemea kupatiwa ufumbuzi kabla ya hali ya sintofahamu haijatokea.*

*Masikitiko yetu makubwa/ kero yetu kubwa ni juu ya uwepo wa baadhi ya makanisa katika kitongoji chetu na utaratibu wake wa uendeshwaji kwa kutofuata sheria, ambapo imefikia kuwa kero, mateso, adhabu na hata kukosa amani.*

*Baadhi ya kero hizo ni pamoja na upigaji kelele kwa kutumia spika kubwa ambazo hutoa muziki mkubwa usiku kucha na kila siku, mbaya zaidi, makanisa haya yapo katikati ya makazi ya watu.*

*Hali hiyo husababisha wagonjwa, watoto, wazee na wanafunzi kuteswa na kelele na hata kupelekea kutofanya vizuri kimasomo.*

*Aidha, miradi yao ya ufugaji wao wa nguruwe pasipo kufuata utaratibu, kwani hufuga katikati ya jamii na kuwaacha wakizurura ovyo, usafi mdogo na mabanda yanayopelekea kutoa harufu kali na isiyovumilika, hali ambayo inahatarisha afya zetu.*

*Sisi kama wanakitongoji tulishawahi kuwaita hawa wamiliki wa makanisa na kuwaeleza tena kiungwana tu juu ya haya tukitegemea kupata suluhu, na badala yake wakawa na majibu yasiyotarajiwa.*

*Wakatoa majibu kuwa wao wana kibali cha serikali na wataendelea bila mtu yeyote kuwasumbua. Ninauliza hivi kweli huu ndio utaratibu wa uendeshaji wa makanisa? Je kwa majibu haya kuna amani hapa?*

*Haya malalamiko ya kero hizi tumezifikisha katika uongozi wa serikali ya kijiji, Ofisi ya Diwani, Kata ya Mikese lakini utekelezaji haupo.*

*Hivyo basi, kwa matumaini makubwa tuliyonayo kupitia gazeti lako pendwa, barua yetu wahusika wataiona na kulitatua hili kabla ya hali kuwa mbaya zaidi.*

**Ahsante ni sisi wanakitongoji,**
**Ukomanga-Fulwe, Mikese.**

## WASILIANA NASI:

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Zimamoto tufunzeni alama na 'saini' hizi

**Na Gaudensia Mngumi**

KATIKA zama hizi za sayansi na teknolojia ni nyakati ambazo zimesaidia kutatua matatizo mengi ikiwamo kuongea kwa alama na ishara mbalimbali ambazo zina ujumbe ili kama huwezi kusoma uangalie picha.

Mfano kama unakatazwa kuvuta sigara, unakutana na alama au maandishi X kwenye sigara lakini pia kama unazuiliwa kugusa kitu kwa mikono isiyokingwa utawekewa glovu.

Kadhalika kama kuna mionzi na vihatarishi vikali alama au picha za koti la plastiki, buti na 'maski' zitawekwa. Na inapotokea kuna sumu hatari inayoua alama ya fuvu na mifupa huchorwa.

Kwa Tanzania mara nyingi alama na ishara hizi huenda zinapuuzwa, ndiyo maana watu wanapoona 'Petroleum Danger', 'No Smoking' hawaielewi.

Pengine mtu anaweza kuingia katika kituo cha mafuta akaanza kuvuta sigara bila kuelewa kuwa kuna alama ya onyo ya 'no smoking' na sigara imepigwa X.

Ni dhahiri kuwa alama hizo kama zingefuatwa na kuheshimiwa watu wangeokoa maisha na kuwa salama zaidi kwenye matukio ya ajali zinazohusisha milipuko, sumu na wakati mwingine kemikali.

Pengine kutokana na kile kilichotokea Msamvu mkoani Morogoro ni wakati wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kuanza mafunzo ya namna ya kuzijua alama za hatari zinazotambulisha athari na madhara mbalimbali yaliyo kwenye vimiminika kama petrol, mitungi ya gesi, dawa, kemikali za mashambani pamoja na viuatilifu.




Jeshi la Zimamoto linawajibika kuwaeleza watu maana ya alama na maandiko hayo kama No Smoking, Petroleum Danger, Highly Volatile na alama kama fuvu na mifupa na nyingine mbalimbali ambazo kama watu watazifahamu wataepuka ajali kama ile ya Morogoro iliyotokea wiki chache zilizopita.

Watanzania wengi wanakutana na alama kama X kwenye ghala pengine hawafahamu kuwa hii inamaanisha kuwa ndani ya nyumba hiyo au ghala hilo kuna sumu kali hivyo wasilisogelee.

Aidha, wanapoona fuvu na mifupa ni alama ya sumu hatari kwa maisha ya binadamu inaweza kuwa sumu ya kemikali na dawa.

Aidha, inawezekana pia wakaona picha ikionyesha bomba lenye maji yanayotiririka na chini kuna mikono inamaanisha tindikali ni hatari isiguse mikono ni alama zinazohusisha maji ya betri.

Wakati mwingine michoro inaonyesha duara na ndani yake kuna alama ya pembetatu yenye alama ya kushangaa.

Huo ni ujumbe kuwa sehemu hiyo ina karantini ni hatari imezuiliwa usiisogelee. Si kwamba kuna karantini ya kipindupindu au maradhi ya dengu na eneo lililozuiliwa kutokana na uwepo wa sumu au kemikali au hadhari ya kitu kingine chochote.

Kuna michoro kama alama ya kushangaa na njiti ya kibiri inayotoa moto au moto nao umechorwa pamoja na alama ya mshangao ndani ya pembetatu yote hayo ni ya kuzingatia.

Pamoja na alama za maandishi kuna michoro kama miwani hiyo mhusika afahamu moja kwa moja kuwa analazimika kuvaa miwani kulinda macho.

Pamoja na miwani kuna buti ajue anatakiwa kuvaa buti miguuni na pia kama imechorwa 'maski' ni vizuri kuhakikisha kuwa unafuata masharti kulinda maisha na usalama wako.

Upo wasiwasi kuwa wakazi wengi mijini ambako pengine kuna kiwango kikubwa cha uelewa hawahangaiki na alama hizi.

Mathalani, dawa za kupulizia wadudu kama mbu au mende zinaonyesha kuwa ni hatari zisiwekwe karibu na moto. Lakini ukweli ni kwamba baadhi ya watu hupuuza dawa hizo, zinawekwa jikoni tena kwa wanaopikia mkaa na gesi.

Vitu kama betri za redio na za simu ni hatari lakini hakuna anayejali zinachomwa moto kwenye majalala na wakati mwingine hulipuka na kuumiza watu.

Wakazi wengi wa mijini wanaofuga hasa ng'ombe hutumia dawa za josho na kutupa vifungashio jalalani japo wanaona alama za fuvu na mifupa kwenye vifungashio hivyo viwe vya plastiki au chupa.

Kupuuza alama za maonyo ni tatizo ambalo linaathiri taifa japo huenda halifahamiki ni kwa kiasi gani. Japo ukweli ni kwamba sumu kama zebaki zinatumiwa migodini bila wanaochenjua dhahabu kutumia tahadhari.

Inatakiwa kila unapochenjua dhahabu kwa kutumia zebaki, epuka kuichoma hewani maana inaathiri hewa, hairuhusiwi kushikwa bila glovu, kutumika bila kuvaa buti na pia isitumiwe au kushikwa na watoto.

Yote yanapuuzwa, mpaka chupa na vifungashio vyake huachwa kuzagaa kila mahali.

Hili la alama na ishara za maonyo ni muhimu Jeshi la Zimamoto likatenga muda na kuwafundisha wananchi kuhusu alama hizo na kuwaepusha na ajali na hata vifo ambavyo vingeepukwa.

## KABWELA NA FADHIL MOHAMMED



# Wagombea wa CCM kupita mchujo mkali uchaguzi wa serikali za mitaa

INATOKA UK 2

kwenye tawi lako ukakubaliwa, ukapewa uanachama, ukalipia kadi Sh. 300, ukalipia kila mwezi Sh. 100, wewe ni mwanachama.

Na mwanachama anatajwa si kwa umri wake au kwa muda aliokuwa mwanachama, hapana! Haki zinalingana na ukisoma haki humu (kwenye Katiba ya CCM), hukuti kwamba kuna haki za madaraja, chama cha namna hiyo kitakuwa siyo chama cha kidemokrasia.

Katika Ibara ya 14, ziko haki tano; kwanza haki ya kushiriki katika shughuli zote za CCM kwa kufuata utaratibu uliowekwa. Kwa hiyo, kikubwa hapo ni utaratibu.

Kuna haki ya kuhudhuria na kutoa maoni yake katika mikutano ya chama pale ambapo anahusika kwa mujibu wa Katiba.

Haki ya kujitetea na kutoa maelezo yake mbele ya kikao cha CCM kinachohusika katika mashtaka yoyote yaliyotolewa juu yake pamoja na haki ya kukata rufani ya kwenda kikao cha juu zaidi cha CCM kama kipo endapo hakuridhika na hukumu iliyotolewa na haki ya kumwona kiongozi yeyote wa CCM kwa mujibu wa utaratibu.

Mimi ndiye mkurugenzi wa uchaguzi katika chama, ninasaidiwa na makatibu wa chama ngazi zote. Kwa mfano, kwenye matawi mkurugenzi wa uchaguzi katika ngazi ya tawi ni katibu wa tawi, kwenye wilaya katibu wa wilaya, kwenye mkoa katibu wa mkoa na kitaifa ndiyo mimi.

Na tunao mfumo wa wazi na wa haki, wasiwe na wasiwasi wowote, wasiporidhika kuna taratibu za kukata rufaa, rufaa zikasikilizwa na haki ikatendeka, nawahakikishia hakuna atakayekwamisha kwa namna yoyote, kitakachomkwamisha mtu kitawekwa wazi kama ni sifa, kama ni ushindani lakini kinachoongoza ni katiba, kanuni na taratibu zetu.

**SWALI: CCM imejipangaje katika uchaguzi huu ukizingatia hali ya siasa nchini kwa sasa?**

**DK. BASHIRU:** Tumejipanga vizuri sana na tumejipanga tukiwa na kianzio kizuri, maeneo yote ambayo tunayashikilia ya serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, tumejipanga kutoyapoteza na yale ambayo yapo kwenye vyama vya upinzani, tumejipanga pia kushinda.

Tunawashukuru wananchi kuendelea kukiunga mkono chama chetu nchi nzima na viongozi wa upinzani katika ngazi hizo wamerejea kwenye chama chetu, tumewapokea kwa shangwe na tunawashukuru sana kwa heshima hiyo, tumeongeza nguvu kutoka kwenye vyama vya upinzani.

Tumepata pia wabunge wengi waliorudi, tumepata madiwani wengi waliorudi na wanachama wengine karibia vyama vyote vya upinzani na hiyo ni nguvu kubwa, lakini pia tumejipanga kwa sababu tumepata wanachama wengi wapya hasa vijana, tulikuwa na kadi zaidi ya milioni mbili kwa zaidi ya miezi sita tumesajili wanachama wapya na hizo zote ni kura.

**SWALI: Kwa sasa CCM ina wanachama wangapi?**

**DK. BASHIRU:** Tupo tunahakiki kwa kutumia mfumo mpya wa Tehama, kufikia Desemba, ndiyo tunaweza tukajua ni kiasi gani, lakini rekodi tuliyonayo ni wanachama milioni 12, milioni 13 mpaka 15.

Unapohakiki majina, kuna wengine wanafariki dunia, kuna wengine siyo hai kwa sababu hawalipi ada. Kwa hiyo, ni vigumu sana kwa sasa kwa chama kikubwa kama hiki na kina wanachama nchi nzima kusema sasa kina wanachama idadi hii.

Lakini hatuko chini ya wanachama milioni 10 ambao wana uhai na rekodi baada ya hizi kadi kuzigawa, tunafikia milioni 14 mpaka 15, lakini sasa itabidi tuanze kuhakiki upya na zoezi hilo linaendelea nchi nzima.

**SWALI: Kuna vyama vya upinzani vinalalamika kuhusu kanuni za uchaguzi wa serikali za mitaa zilizotolewa hivi karibuni. CCM mmeridhikia na kanuni hizo?**

**DK. BASHIRU:** Sisi tulishiriki na hapakuwa na maoni ya CCM peke yake, yalichukuliwa maoni ya wadau na wala siyo vyama vya siasa peke yake, mchakato ule mimi nimeufuatilia na nimeridhika kuwa ulikuwa ni mchakato wa wazi, huru na haki.

Ni mchakato ambao unakidhi sifa za mchakato wa kidemokrasia, taasisi zisizokuwa za kiserikali zimehusika, vyama vyote vimehusika na wengine tumekutana kwenye mchakato huo na sisi tumetoa maoni yetu na sisi tuna maoni ambayo hayakukubaliwa, hatujatoka hadharani kusema ni mangapi, lakini mwafaka umeshafikiwa.

**SWALI: Maoni ya CCM yamechukuliwa kwa kiasi gani katika kanuni hizo mpya?**

**DK. BASHIRU:** Sisi sasa hatupimi kwamba haya ndiyo yametupwa na haya ndiyo yamekubaliwa, sisi tunasema kwamba kuna kanuni ambayo tunaridhika kuwa imetosheleza, wala hatuhitaji kwamba ni kanuni ngapi hata ungeweza kusema moja, ikapatikana hiyohiyo moja, ni asilimia mia (100), haina maana yoyote.

Hapa tunachokizungumza ni kwamba ipo kanuni ambayo imetengenezwa kwa mujibu wa mahitaji ya kidemokrasia na mahitaji ya kidemokrasia ni haki ya mtu kusema na kusikilizwa, na haki ya kujieleza na kushiriki na hao mimi naheshimu mawazo yao, hata kulalamika pia ni sehemu ya demokrasia na hata kutoridhika ukatoka hadharani ukasema siridhiki, ni sehemu ya demokrasia lakini ninachowaomba vyama vya upinzani na sisi CCM tupo tayari, tuache visingizio.

**SWALI: Kanuni za uchaguzi huo zimeweka siku saba pekee kwa ajili ya kampeni. Muda huo unatosha?**

**DK. BASHIRU:** Tumeshatangaziwa, muda umejulikana ndiyo huo, sasa tutafanyaje? Sikiliza, kwanza mtaa una watu wangapi? Tusiseme hapa kama vile siyo Watanzania, huu ni uchaguzi unaohusu wakazi wa mtaa, mtaa unalinganaje?

Yaani siku saba mtu haujapiga kampeni mtaa mzima? Siku saba hujapiga kampeni kijiji kizima? Siku saba hujapiga kampeni kitongoji kizima?

Na kumbuka hao watu wanaopiga kura uwape mwezi mzima, hao watu wanafanya kazi, yaani sisi wanasiasa kama tumeifanya siasa kwamba sasa ndiyo kazi, tujue pia wapigakura wana kazi zao, wana ratiba zao hizo.

Siku saba wana siku za kulima, siku saba hizo wana siku za kuhangaika na maisha yao ya kiuchumi, kuna ibada, hakuna muda usio na thamani, kwanza hata hizo siku saba mie naona bado nyingi sana, huu siyo uchaguzi mkuu kwamba mgombea lazima azunguke nchi nzima.

Kuna kijiji gani kinalingana nchi au labda wanataka kuwa na helikopta kwenye kampeni za kijiji, kama hawana mfumo wa kuwa kila mahala, sasa hiyo wasilalamike.

Mimi ninachojua bungeni kuna siasa na kuna wanasiasa wa vyama vyote, vijijini kuna wanasiasa wa vyama vyote, kitongoji na kuna madiwani nimeona wanafanya mikutano ya hadhara, wabunge wanafanya mikutano ya hadhara, halafu wanatoka wanasema wamezuiwa, hakuna aliyezuiliwa, waache visingizio.

Kama wana wabunge wachache mikutano itakuwa michache na kama wana madiwani wachache na mikutano itakuwa michache pia, wasituonee wivu.

**SWALI: Yapo pia malalamiko ya vyama vya upinzani kwamba waratibu wa shughuli za uchaguzi huo ni wakuu wa wilaya na mikoa ambao ni makada wa CCM. Wewe huoni shida katika hili kidemo**

**DK. BASHIRU:** Huu siyo uchaguzi wa kwanza, tumeanza uchaguzi wa serikali za mitaa tangu mwaka 1994, tumefanya uchaguzi mwingine, eeh nadhani ilikuwa ni mwaka 2009, tukafanya mwingine 2014.

Kwa hiyo, huu ni uchaguzi wa nne sawa, na usimamizi wake ni uleule, hakuna kitu kipya, labda kwa ambao hawajawahi kushiriki uchaguzi huo ndiyo watakaodanganywa na ninaomba vyombo vya habari waambieni wananchi ukweli, uchaguzi huu siyo mpya na hakuna utaratibu mpya, wasimamizi ni walewale na wanateuliwa kwa mujibu wa katiba na kanuni na hazijataja mkuu wa mkoa na mkuu wa wilaya.

**SWALI: Umesema hakuna kitu kipya katika uchaguzi huo. Je, kupunguzwa kwa muda wa kampeni na kuwa siku saba, huoni kwamba huu ni utaratibu mpya?**

**DK. BASHIRU:** Sasa, hayo yamejadiliwa na ndiyo yaliyopita, kama itaonekana kwamba yamekuwa na kasoro, kanuni hizi na sheria hizi siyo misaafu, zitabadilishwa, huu siyo mwisho wa dunia, kila uchaguzi unatufundisha mabadiliko.

**SWALI: Upinzani wanalalamika maoni yao hayachukuliwi, kanuni hizo zitabadilishwaje?**

**DK. BASHIRU:** Eeh zamu nyingine ikija kwa sababu lazima ufike wakati uamuzi ufanyike na uamuzi una pande mbili, kuna uamuzi ambao unamridhisha mtu na kuna uamuzi ambao haumridhishi mtu.

Na uamuzi mzuri siyo ule ambao unaridhisha kila mtu, bali ni uamuzi ambao sasa upo kazini unatumika, vyama vya upinzani bado vina safari ndefu kwa sababu vimejikita katika siasa za matukio.

Havijajikita katika siasa za kitaasisi, taasisi zinazofahamika ambazo zina miundo na mifumo ambayo imeenea nchi nzima. Kwa hiyo, vyama hivi haviko mahala pote ndiyo maana wanalalamika na hawafanyi vizuri, wanakuja kufanya vizuri kwenye uchaguzi ambao unahusisha urais na ubunge kwa sababu unakuwa wa kitaifa.

Kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa inatakiwa chama kifike mahali husika, siyo kinakwenda na mgombea palepale, CCM ina viongozi wa matawi na vijiji waliozoeleka, mpaka ukaweza, ukadhani huyo mtu ndiyo kijiji chenyewe, ha ha ha!

Tuna ofisi za matawi, ni nzuri na za kisasa kuliko makao makuu ya vyama vingi, viko vyama vinapanga mpaka leo miaka ishirini, kuna kimoja nilitaka kuwatania kule Busega wanajenga ofisi mpya ya chama kwa sababu ile ni wilaya mpya, nikawaambia natamani ingekuwa ni makao makuu ya ACT.

## Mtaalamu atoa somo njia kujikinga na ajali za moto

INATOKA UK. 2

(Fire extingusher) yenye povu au poda na kama itakosekana, mchanga mkavu unaweza kutumika kama njia mbadala.

Hata hivyo, ameonya watu kuacha kutumia mchanga kumwagia mtu anayeungua kwa kuwa madhara yake ni makubwa kwenye ngozi ambayo husababisha hata kifo.

Alisema mtu anayeungua anatakiwa kuzimwa kwa blanketi maalumu na pia anayeokolewa na mwokoaji wanatakiwa walindwe wasivute hewa ya moto ili isiharibu mfumo wa upumuaji.

Sajenti Maingu pia alitaja aina nne za moto ambazo mtu anatakiwa kuchukua tahadhari ambazo ni; moto unaosababishwa na asili ya mimea zikiwamo nguo, nyasi, samani za nyumba ambao unaweza kuzimwa kwa kutumia kizima moto cha maji na poda.

Aina nyingine ya moto ni ule wenye asili ya vimiminika vyenye milipuko ambavyo ni mafuta ya petroli, mafuta ya taa, pombe na tindikali, ambao moto wake unaweza kuzimwa kwa kizimamoto cha povu, poda au mchanga mkavu.

Aina ya tatu ya moto ni wenye asili ya gesi ambao huzimwa kwa kizimamoto cha poda na aina ya nne ni moto wenye asili ya chuma, kama makaa ya mawe, aluminium, magnesium ambao huzimwa na poda kavu yenye kemikali au mchanga mkavu.

Sajenti Maingu pia alishauri nyumba ziwe zinabadilishwa waya wa ardhini (earth wire) angalau kila baada ya miaka mitano, ili kuepuka nyumba kupata hitilafu na kuungua.

HABARI KITAIFA

# CMSA yazipa mbinu benki za biashara kuanzisha uhifadhi

Na Mary Geofrey

BENKI za biashara nchini zimeshauriwa kuanzisha huduma ya Uhifadhi wa Dhamana na Usimamizi wa Uwekezaji katika masoko ya mtaji ili kuzisaidia kuongeza idadi ya wawekezaji na kuchochea ukuaji wa uchumi wa nchi.

Pia zimetakiwa kutumia fursa zilizopo katika sekta ya masoko ya mitaji ikiwamo kuuza dhamana kwa umma na kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam ili kuzisaidia kuongeza mitaji yao.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, katika hafla ya uzinduzi wa huduma za Uhifadhi wa Dhamana na Usimamizi wa Uwekezaji wa Benki ya I&M.

"Hatua hii itasaidia utekelezaji wa agizo la serikali kwa benki zote za biashara na benki za wananchi katika kutimiza matakwa ya kisheria ya kuwa na mtaji wa kutosha ili kujiendesha kibiashara," Mkama alisema.

Alizitaka kampuni za bima kutumia fursa zilizopo katika sekta ya masoko ya mitaji ili kuongeza mitaji yao na kuzisaidia kuwa na uwezo wa kushindana na kampuni za nje zinazotoa huduma za bima nchini.

"Vilevile natoa wito kwa mifuko ya hifadhi ya jamii na taasisi za fedha kuunga mkono malengo na azma ya serikali ya kujenga uchumi wa viwanda kupitia masoko ya mitaji nchini," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji wa Benki I&M, Baseer Mohammed, alisema benki hiyo inaenda kufanya vizuri sokoni katika utoaji wa huduma hiyo kwa sababu ni fursa kwa wawekezaji wa nchini kuwekeza katika masoko ya mitaji na dhamana ndani na nje ya nchi pamoja na nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki.

"Tuna furaha kuanzisha huduma nyingine ambayo ina kwenda kutanua wigo wa huduma zetu na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi. Kuanzishwa kwa huduma hii ni ushahidi tosha wa kuendelea kusimamia dhamira yetu ya kuwa na benki imara ukanda wa Afrika Mashariki," Mohammed alisema.

# Uhaba vifaa kujisitiri wasichana masomo

Yasmine Protace

UHABA wa vifaa vya kujisitiri kwa wanafunzi wa kike, ni moja ya sababu inayochangia wanafunzi kutoshiriki masomo kikamilifu.

Hayo yalisemwa na mmoja wa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mabibo jijini Dar es Salaam, Mariam Ayubu, wakati akichangia mada katika semina za jinsia na maendeleo (GDSS), ambazo hutolewa na TGNP Mtandao.

Katika semina hizo ajenda zake zinazungumzia masuala ya kijamii.

Mwajuma ni mmoja wa wanafunzi walioshiriki semina hiyo na kutoa kilio chake juu ya vifaa vya kujistiri ambavyo vinakuwa ni changamoto katika shule hiyo.

Alisema mwanafunzi wa kike anapoingia katika mabadiliko ya mwili, anapatiwa kifaa kimoja cha kujistiri na shule, lakini kutokana na bei kuwa kubwa madukani ya kununua kifaa cha kujistiri wanalazimika kutokuja shule na kukaa majumbani mpaka hali ya mwili itakapokaa sawa.

Alisema hali hiyo inachangia hata kuyakosa masomo, hivyo kuiomba serikali iwasaidie ili waweze kuwa wanapatiwa vifaa hivyo kwa wingi, na waweze kuvitumia ili waache kukatisha masomo.

Aliongeza kuwa changamoto nyingine shuleni kwao ni kukosekana kwa kifaa cha kuhifadhia taka ngumu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu Wenye Ulemavu), Jenista Mhagama, akipata maelezo kuhusu vioski tembezi vilivyotolewa na Kampuni ya Sigara Tanzania (TCC ) kwa wafanyabiashara ndogo ndogo wa Wilaya ya Chato. Wengine kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Sheria na Uhusiano wa TCC P, Godson Killiza, Mbunge wa Chato, Dk. Medard Kalemani, Mkurugenzi wa Masoko wa TCC, Awaichi Mawalla na Mkuu wa Wilaya ya Chato, Mtemi Msafiri Simeon. **MPIGAPICHA WETU**

# TCC yawanyanyua wafanyabiashara Chato

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Sigara Tanzania (TCC) imetengeneza fursa katika Wilaya ya Chato mkoani Geita baada ya kugawa vioski tembezi kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na kuchangia katika kubadilisha maisha yao.

Fursa hiyo itawawezesha kufanya biashara katika mazingira mazuri zaidi.

Ugawaji wa vioski hivyo ulishuhudiwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama na Mbunge wa Chato ambaye pia ni Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani pamoja na viongozi mbalimbali na wawakilishi kutoka kampuni hiyo.

Mhagama aliipongeza TCC kwa kubuni mradi huo ambao umesambaa nchi nzima na kuunga mkono jitihada za serikali za kuwawezesha Watanzania kiuchumi kwa kuwapa rasilimali na mafunzo, huku akizitaka kampuni nyingine ziige mfano huu.

Aliainisha umuhimu wa vioski hivyo kwa wanufaikaji hao 20 kwani wataweza kufanya biashara zaidi kwani vioski hivyo ni tembezi na pia wanaweza kuuza bidhaa nyingine tofauti na sigara. Alisema sasa wataweza kukimu familia zao vizuri zaidi na pia kuchangia katika maendeleo ya Wilaya ya Chato.

"Ni matumaini yangu kuwa mnaopokea vioski hivi mtavitunza na kufanya kazi kwa bidii ili wafanyabiashara wa Chato wawe mabalozi wazuri wa mradi huu," alisema.

Aliipongeza TCC Plc kwa kutekeleza kwa vitendo sera ya Tanzania yenye viwanda kwa kutumia kampuni ya Kitanzania inayoitwa Sign Express Industries kutengeneza vioski hivyo na malighafi ya humu humu nchini. "Huu ni mfano wa kuigwa na wawekezaji wengine kwani hapa mmeongeza ajira nchini," alisema. Dk. Kalemani alisema TCC imeweka historia kwani hii ni mara ya kwanza kwa wakazi wa Chato kushuhudia mradi kama huu na kusisitiza kuwa mradi huo utabadili maisha ya wafanyabiashara hao kwani wataweza kuzungusha bidhaa zao kutoka sehemu moja na kwenda sehemu nyingine kutafuta biashara zaidi kwani vioski hivyo vinavyosogea.

"Mradi huu ulipozinduliwa Dodoma, sikujua kama itafika Chato. Niliwaomba TCC ikumbuke Chato katika awamu hii na wameonyesha kweli wanawajali wafanyabiashara wadogo. Vioski hivyo vina sehemu kubwa ya kupanga bidhaa," alisema Dk. Kalemani.

Mkurugenzi wa Masoko wa TCC Awaichi Mawalla, alisema mradi huu umekuwa na mafanikio makubwa toka waanze kugawa vioski hivyo katika awamu ya kwanza, ambapo jumla ya vioski 400 vimegawiwa kwa wafanyabiashara wadogo nchi nzima ikiwa ni njia mojawapo ya kukuza biashara zao kwani wataweza kufanya biashara kwa muda mrefu na kusaidia biashara nyingine.

"Tuna mpango wa kuzindua awamu ya pili ili tuweze kuwafikia wafanyabiashara wengi zaidi kwani tunataka kusaidia serikali kutekeleza kauli mbiu ya serikali ya 'Hapa Kazi Tu'," alisema, huku akieleza kuwa kati ya wafanyabiashara 400 waliopokea vioski hivyo nchi nzima, 96 walikuwa wanawake.

Mawalla alisema TCC inaamini Chato ni sehemu sahihi ya kuwekeza kwani imezungukwa na nchi za Afrika Mashariki zilizozingirwa na Ziwa Victoria na kufanya Chato iwe kituo muhimu cha biashara kwani viongozi kadhaa waliotembelea Chato wameonyesha nia ya kuwekeza Chato.

Alisema wafanyabiashara waliopokea watatengeneza fedha zaidi kwani vioski hivyo vina umeme wa sola na sehemu ya kuchaji simu," alisema. Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, Elizabeth James, ambaye ana ulemavu wa mguu alisema vioski hivyo vimeongeza hadhi ya biashara yake.

Mnufaika mwingine, Bembeleza Chigala alisema, "Sasa tutaweza kufanya kazi hadi usiku na kufungia bidhaa zetu kwenye vioski."

# Uwasa yafanya ukarabati mkubwa wa madarasa

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira jijini Tanga (UWASA) imefanya ukarabati mkubwa wa madarasa matatu kwenye Shule ya Msingi Usagara iliyopo jijini Tanga, ikiwa ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais John Magufuli za kuinua sekta ya elimu.

Ukarabati huo uliogharimu zaidi ya Sh. milioni 19 uzinduzi wake umefanywa na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, ambao utasaidia kuondoa changamoto zilizokuwa zikiwakabili wanafunzi wa shule hiyo, hatua itakayochochea kuongeza kasi ya ufaulu shuleni hapo.

Akizungumza baada ya kuyazindua madarasa hayo, Waziri Mbarawa aliipongeza mamlaka hiyo kwa juhudi kubwa wanazofanya katika kusaidia shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo suala la elimu.

Alisema hatua hiyo itachochea wanafunzi kuweza kusoma bila kuwapo kwa vikwazo kwani mamlaka hiyo, imekuwa ikisaidia serikali katika maeneo mbalimbali na kusema ni mamlaka ya kuigwa na mamlaka zingine nchini.

"Nimefarijika sana, nimezunguka katika mamlaka nyingi nchini sijaona wakifanya mambo makubwa kama Tanga Uwasa mnavyofanya... hili ni jambo kubwa sana sababu elimu yeyote inatengenezwa kwa kuwapo kwa miundombinu na mazingira mazuri," alisema Waziri Mbarawa.

Waziri Mbarawa aliwataka walimu shuleni hapo kulinda vyema miundombinu ya madarasa hayo, ili yaweze kutumika katika vizazi vijavyo kwani jitihada hizi ni sehemu ya kuunga mkono jitihada za Rais katika kufanikisha utoaji wa elimu bure.

Katika hatua nyingine, Waziri Mbarawa alikemea tabia ya baadhi ya wananchi kujiunganishia huduma ya maji kinyemela badala yake aliwataka kufuata taratibu zilizowekwa ili kuepuka kuisababishia hasara mamlaka hiyo.

"Lakini ni wajibu wetu wananchi kuhakikisha tunalipa bili za maji kwa wakati na kutunza vyanzo vya maji, ili kuifanya mamlaka hiyo iweze kujiendesha ipasavyo, pia wananchi mnapaswa kutoa taarifa kwa wataalamu wa maji pindi mnapoona mabomba ya maji yamekatika katika maeneo yenu," alisisitiza Waziri Mbarawa.

Mwenyekiti wa Bodi aliyemaliza muda wake wa Tanga Uwasa, Salum Shamte, alikuwa kipindi cha miaka sita katika uongozi wake waliweza kutumia zaidi ya Sh. milioni 90 kwa ajili ya kusaidia miradi mbalimbali ya maendeleo inayotekelezwa na serikali.

Alisema Sh. milioni 70 waliweza kutumia katika sekta ya elimu, huku Sh. milioni 20 zikitumika katika sekta ya afya, michezo, na walemavu ambapo aliiasa bodi mpya kuhakikisha inaguswa kusaidia huduma mbalimbali za kijamii.

Mkuu wa wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, alisema mamlaka hiyo imekuwa ikifanya mambo mengi makubwa ya kuhakikisha wanaunga mkono juhudi za serikali hususani kwenye sekta ya elimu kwa kukarabati na kujenga madarasa kuanzia mwanzo katika msingi mpaka inakamilika.



Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Elimu Solutions, Neithan Swed (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu hafla ya utoaji wa Tuzo za Elimu Tanzania 2019, takayofanyika Mlimani City Jumamosi ijayo Agosti 31. Kulia ni Mratibu wa Mradi huo, Peter Goardian na Mkurugenzi wa Masoko, Catherine Ndosi. **PICHA: JOHN BADI**

## BancABC yasaidia mazishi kwa mteja

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya BancABC imetoa msaada wa mazishi kwa mke wa mmoja wa wateja wake wa Mkopo Rahisi wa jijini Dar es Salaam ambaye amefiwa na mume.

Mkopo Rahisi ni moja ya huduma ambayo hutolewa na BancABC kwa ajili ya kufariji familia ya mteja wake inapotokea kifo kwa kufuta mkopo uliokuwa umebaki pamoja na kutoa msaada wa Sh. 500,000/- kwa familia.

Akizungumza jijini Dar es Salaam leo wakati wa kukabidhi hundi ya fedha hizo kwa mjane huyo, Maria Privatus ambaye mume wake alikuwa mteja wa BancABC Mkopo Rahisi kabla ya kufariki, Meneja wa BancABC Kanda ya Dar es Salaam, Ferdinand Mgeni, alisema kuwa benki hiyo imekuwa ikitoa msaada kwa familia ambayo mteja alikuwa na Mkopo Rahisi kutoka BancABC.

"Kile ambacho mnaona tukifanya hapa leo ni jambo ambalo tulikuwa tukifanya siku zote. Sisi BancABC ambao ni kampuni tanzu ya Atlas Mara Tanzania tuliamua kuwa na kipengele cha aina hii kwenye mikopo yetu ya Mkopo Rahisi ili tuwe tofauti na wengine kwenye soko. Lakini zaidi ni kufanya familia ya wafiwa kuwa na amani kwani mbali na kutoa rambi rambi ya Sh. 500,000, lakini tunafuta deni la mkopo ambalo marehemu alikuwa anadaiwa," Mgeni aliongeza.

Mgeni aliongeza kuwa mkopo wa Mkopo Rahisi unao faida nyingi kwa mteja kwani una riba ya chini ya asilimia 1.6 kwa mwezi. "Nia yetu ni kupunguza mzigo kwa wateja wakati wa kulipa mikopo yao. Vilevile Mkopo Rahisi unatoa muda mrefu wa kulipa kwani muda wake ni miezi 72 (miaka 6) na wateja wanaweza kupata mkopo hadi Sh. milioni 40," alisema.

Akizungumza baada ya kupokea rambirambi hiyo, Maria Privatus ambaye mumewe alifariki akiwa ni mwalimu wa Shule ya Wasichana ya Zanaki ya jijini Dar es Salaam, alisema: "Nawashukuru sana BancABC kwa kutoa muda wenu na kuja kunitembelea pamoja na kunipa rambirambi hii. Nimekuwa nikifanya biashara ya kuuza chakula hapa shuleni ambapo mume wangu alikuwa ni mwalimu. Nitatumia pesa hii kwa ajili ya kukuza biashara yangu na hatimaye niweze kuendesha familia kwani kwa sasa nimebaki bila ya kuwa na mtu wa kunisaidia."

# Kinamama wajasiriamali waiomba serikali msaada

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

WAJASIRIAMALI wa vikundi vya ufugaji wa ng'ombe, mbuzi, sungura, kuku na kanga vilivyopo kijiji cha Furaha shehia ya Mvumoni Wilaya ya Chakechake, wameiomba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuwakagua na kujua matatizo yanayowakabili, kuwapatia mafunzo, ili wapate utaalamu wa kushughulikia mifugo yao.

Walisema wamekuwa wakishughulikia mifugo yao kwa mazoea tu na sio kwa utaalamu, jambo ambalo linawatia hasara kubwa, kutokana na mifugo mingi kuingiwa na maradhi na hatimaye kufa kabisa.

Walisema kwa vile wananchi wameamua kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha vikundi vya ushirika kwa lengo la kujikwamua na maisha magumu, hivyo ipo haja kwa serikali kupitia wizara husika kuwapitia wanavikundi hao na kuwapa elimu ambayo itawasaidia katika shughuli zao.

"Kwa kweli hatujapata utaalamu wa mifugo, tunafuga tu kwa mazoea jambo ambalo linatutia huzuni maana mifugo yetu inakumbwa na maradhi, lakini hatujui tufanye nini, kwa hiyo wanakufa kwa wingi, hii ni hasara kubwa kwetu, kwani ndio ajira yetu," alisema mwanamke aliyejikita na ufugaji, Safia Hamad Iddi.

Alisema changamoto nyingine ni ukosefu wa banda la kudumu la kufugia pamoja na ukosefu wa huduma ya maji, jambo ambalo linaathiri sana mifugo.

"Mimi ninao ng'ombe sita, mbuzi 20, kanga sita, kuku 150 na sungura wawili na nimewaajiri wanangu na mume wangu, lakini kutokana na kuwa tunafuga mbali na majumbani, tunalazimika tupate maji ya kuwanywesha mifugo hiyo, na pia banda letu ni bovu, hivyo wezi wanatunyemelea," alisema.

Alisema kuna mafanikio mengi aliyoyapata ikiwamo kujenga nyumba, kuwatafutia wanawe wake, kuwaajiri watoto na mume wake na kueleza kuwa, iwapo wataendelea kukosa utaalamu, ukosefu wa nyenzo muhimu watarudi nyuma kimaendeleo na kubaki nyumbani bila ya kazi yoyote.

Mumewe alisema mkewe ni jasiri na mwenye tamaa, kwani ameinua familia yao kiuchumi, jambo ambalo linawapa furaha na faraja kubwa ya kushirikiana naye katika kuendeleza mifugo hiyo.

"Kwa kweli najivunia sana kuwa na mke jasiri, pamoja na changamoto zinazotukabili, lakini hatujakata tamaa tunaendelea, tunaiomba serikali itusaidie ili tujikwamue zaidi na umaskini, hii ndio ajira yetu," alisema.

# Washauriwa kutumia mbegu za asili

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WAKULIMA nchini wametakiwa kutumia mbegu ya asili zaidi kuliko mbegu za kisasa kwa kuwa zinahimili magonjwa mbalimbali na mabadiliko ya hali ya hewa.

Akizungumza katika warsha ya wanahabari jijini Arusha, iliyoandaliwa na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (Mviwata) Mkoa wa Arusha, mtaalamu wa mbegu kutoka mtandao huo, Abdalah Mkindi, alisema mbegu za asili zimeshindwa kuingizwa kwenye mfumo unaojitegemea utakaofanya zitambulike na kulindwa, ili kunusuru hazina ya asili inayotishia kutoweka.

Alisema Mviwata imeanza kampeni ya kuhamasisha wakulima kutumia mbegu za mahindi ya asili ili kuepusha kutoweka kwa mbegu hizo kutokana na mbegu mpya nyingi za kigeni zinazotumiwa na wakulima nchini.

Mkindi alisema mfumo rasmi wa mbegu unachangia kwa asilimia 30 tu ambao ni mchango kidogo kwa taifa, huku mfumo usio rasmi ukichangia asilimia 70, japokuwa hautambuliki na serikali.

"Wananchi wanategemea zaidi mbegu za kienyeji kutoka kwa wakulima, hivyo ni vyema serikali ikatambua mifumo yote hii miwili ili kuwezesha wakulima kuendeleza mbegu hizi, kwani zina faida nyingi kwa jamii na taifa," alisema Mkindi.

Alisema mbegu za asili licha ya kustahimili ukame na mabadiliko ya tabianchi, pia zina sifa zingine kama kutoa chakula, hutumika kama dawa, mafuta pamoja na kutumiwa kupandwa mara nyingi iwezekanavyo tofauti na mbegu za kisasa mpaka msimu tu.

Mkindi alibainisha baina ya sera na sheria zinazoongoza mbegu ikiwamo Sheria ya Mbegu ya mwaka 2003 inayoainisha adhabu dhidi ya atakayebainika kuuza mbegu zisizo rasmi, kutozwa faini isiyopungua Sh. milioni moja au isiyozidi Sh. milioni tano.

Pia alisema sheria ya mwaka 2014 inamtaka mtu anayejihusisha na mbegu hizo kulipa faini isiyopungua Sh. milioni 100 au isiyozidi Sh. milioni 500.

Alisema jitihada za makusudi zinahitajika kwa serikali kuhamasisha wakulima kuendelea kuhifadhi mbegu za asili ili kumkomboa mkulima na mabadiliko ya tabianchi.

Makamu Mwenyekiti Mviwata Mkoa wa Arusha, Anna Ephata, alisema lengo la warsha hiyo ni kuwajengea waandishi uwezo wa uelewa wa mbegu za asili ili kuwafikia watu wengi zaidi katika kutoa elimu hiyo.

Alisema Mviwata wanatamani kuona serikali ikitoa kipaumbele kwa mbegu za asili ambazo zinamilikiwa na wakulima kwa kuwa zina faida nyingi ikiwamo manufaa katika afya ya mlaji tofauti na mbegu mpya za mahindi ambayo yamekuwa hayana radha kwa mlaji.



Kaimu Ofisa Madini Mkazi Mkoa wa Kimadini wa Simanjiro, Mhandisi Castro Maduwa, akizungumza kwenye uzinduzi wa soko la madini la Mji Mdogo wa Orkesumet jana. **PICHA: GIFT THADEY.**

## Vijana watakiwa kupata elimu afya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

VIJANA wa Halmashauri ya Arusha DC wilayani Arumeru, wametakiwa kuwa na utaratibu wa kuhudhuria kwenye vituo vya afya kupata mafunzo ya afya ya uzazi wa mpango kupitia huduma rafiki kwa vijana, ya mradi wa Tupange Pamoja.

Mradi huo unatekelezwa na halmashauri kwa kushirikiana na Shirika lisilo la kiserikali la Kimataifa la Jhpiego.

Mratibu wa Jhpiego Mkoa wa Arusha, Waziri Njau, alisema hayo katika semina ya mafunzo ya afya ya uzazi kwa vijana kupitia huduma rafiki kwa vijana, yaliyofanyika kwenye ofisi ya Kata ya Moivo.

Njau alisema kwa kawaida elimu ya afya ya uzazi na uzazi wa mpango, hubadilika kutokana na utafiti mbalimbali unaoendelea kufanywa na wanasayansi, hivyo ni vyema vijana kuhudhuria mafunzo hayo mara kwa mara ili kufahamu zaidi juu ya afya ya uzazi na uzazi salama.

"Elimu ya afya ya uzazi iliyokuwa ikitolewa zamani ni tofauti na elimu ya sasa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hii imesababisha kugundulika kwa dawa na vimelea mbalimbali ambavyo hapo awali havikujulikana," alisema Njau.

Mratibu wa Tupange Pamoja, Kata ya Moivo, Kylie Gyubi, alisema vijana wanapaswa kujitambua na kutambua afya zao kwa kutembelea vituo vya afya na kukutana na wataalamu wa afya ya uzazi salama ili kupima na kupata ushauri wa afya zao.

"Vijana wengi wamekuwa wakitumia njia za uzazi wa mpango bila kufuata ushauri wa wataalamu wa afya jambo ambalo linasababisha wengi kupata madhara ya kiafya wakidhani kuwa njia hizo si salama, kumbe tatizo ni taarifa zisizo sahihi juu ya dawa hizo," alisema Gyubi.

Alisema kupitia mafunzo hayo, vijana wamekiri kuwa na taarifa zaidi ya uzazi wa mpango kuliko afya ya uzazi, kutokana na kutokuwa na elimu.

# Wahimizwa kuchangia damu kwa wajawazito

**Na Cynthia Mwilolezi,** BABATI

WANANCHI wa Mkoa wa Manyara wametakiwa kuwa na mwamko wa kuchangia damu, ili kuwasaidia wahitaji waliopo kwenye hospitali mbalimbali nchini, wakiwamo wajawazito na majeruhi wanaopata ajali.

Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM (UVCCM) Mkoa wa Manyara, Moses Komba, aliyasema hayo jana wakati akielezea mpango wao wa kuchangia damu ya kuwasaidia majeruhi wa ajali iliyotokea Morogoro.

Komba alisema umoja huo unawaomba wananchi kuwa na tabia ya kujitokeza kuchangia damu kwa ajili ya kuwasaidia wahitaji mbalimbali.

Alisema viongozi, wanachama na vijana wa CCM, wanapaswa kuchangia damu ili kuokoa maisha ya majeruhi waliopata ajali ya moto mkoani Morogoro.

"Tunapaswa kuchangia damu kwani huu ndio utamaduni wa Watanzania kushirikiana wakati wa shida na raha bila kujali dini, kabila, rangi na itikadi ili kuonyesha umoja wetu kwa kusaidia ndugu zetu," alisema Komba.

Katibu wa UVCCM mkoani Manyara, Daniel Muhina, alisema wamepata uniti 58 za chupa za damu na wanaendelea na uchangiaji damu hadi Agosti 31 mwaka huu.

Muhina alisema shughuli za uchangiaji damu zinaendelea mkoa mzima na kwa mjini Babati, waende kwenye ofisi za CCM Bagara na Halmashauri ya Wilaya ya Babati ni Kituo cha Afya Magugu.

Alisema sehemu nyingine ni ofisi ya CCM ya Wilaya ya Hanang', Hospitali ya Wilaya ya Mbulu, Kituo cha Afya Orkesumet wilayani Simanjiro na Hospitali ya Wilaya ya Kiteto.

Mmoja wa vijana hao, Carol Gisimoy, alisema wanaungana na Watanzania wengine nchini, katika kuwasaidia kuchangia damu majeruhi wa ajali hiyo ya Morogoro.

Agosti 10, mwaka huu, ajali ya lori la mafuta ilitokea Msamvu mkoani Morogoro na kusababisha zaidi ya watu 100 kufariki dunia na majeruhi 12 wamelazwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Dar es Salaam.





# Waziri ataka mkandarasi kujisalimisha

**Na Godfrey Mushi,** HAI

SERIKALI imeamuru kujisalimisha katika ofisi ya Waziri wa Nishati jijini Dodoma Mkurugenzi wa Kampuni ya Urban and Rural Engeneering iliyopewa kazi ya mwaka mmoja ya kusambaza umeme katika vijiji vya mkoa wa Kilimanjaro.

Mkandarasi huyo anadaiwa kukwamisha utekelezaji wa ahadi ya Rais John Magufuli kwa kushindwa kuunganisha umeme katika vijiji 68 kati ya 83 vilivyoko katika mkataba wake, huku muda wa mkataba huo ukikaribia kufikia ukomo Desemba, mwaka huu.

Jana, wakati anazindua mradi wa umeme kwenye taasisi za elimu na viwanda kwenye wilaya za Siha na Hai, Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema mkandarasi huyo alitia saini mkataba wa utekelezaji wa mradi huo wenye thamani ya Sh. bilioni 12.

"Kila tukimpigia simu hajibu na nimewasiliana naye kwa ujumbe mfupi wa maandishi (sms) hajajibu. Sasa naagiza ajisalimishe katika Wizara ya Nishati, Dodoma. Aje kujieleza ni kwa nini asichukuliwe hatua kwa kukwamisha mradi huu wa Wakala wa Umeme Vijijini (REA) awamu ya tatu," alisema.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, kukwama kwa utekelezaji wa mradi huo kumesababisha baadhi ya wananchi kwenye vijiji vilivyoko ndani ya mradi huo, kutumia mafuta ya taa na umeme wa jua.

"Huyu mkandarasi namtaka wizarani haraka iwezekanavyo. Nia yetu serikali ni kupitia upya mkataba wake ili kujiridhisha kama ana uwezo wa kutoa huduma ya usambazaji umeme kwa wananchi vijijini na kama atabainika kuwa na makosa atachukuliwa hatua," alisema Mgalu.

Akiwa katika Wilaya ya Hai, Mkuu wa Wilaya hiyo, Lengai Ole Sabaya, alisema mkandarasi huyo amekuwa kero kubwa katika utekelezaji wa ahadi ya Rais Magufuli aliyoitoa katika wilaya hiyo.

"Hata mimi nimemwita mara kadhaa, nikimtaka kufika ofisi kwangu kuonyesha mpango kazi wa kuwaunganishia wananchi umeme, lakini amekuwa akikaidi wito wangu na hajawahi kuja," alisema Ole Sabaya.

Uamuzi wa Naibu Waziri huyo kutoa amri ya kujisalimisha kwa mkandarasi ulitokana awali na malalamiko ya baadhi ya wananchi wa Wilaya za Hai na Siha kwamba wanaona giza katika utekelezaji wa mradi huo kwa sababu wanaona kama matumaini yanafifia wakati mkataba wake ukikaribia kufikia ukomo.

Kutokana na hali hiyo, walimwomba Naibu Waziri kufuatilia kwa karibu mradi huo katika wilaya zao baada ya mashimo ya kuweka nguzo kuchimbwa kwa muda mrefu ambayo katika baadhi ya maeneo yamesababisha hasara kwa kuumiza watoto.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme (TEMESA), Mhandisi Japhet Maselle, akimpongeza mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Warioba Sanya (kulia), baada ya kuzindua ujenzi wa vivuko vipya viwili kwa ajili ya maeneo ya Chato-Nkome (Chato) na Bugorora-Ukara (Wilaya ya Ukara), katika karakana ya Songoro Marine Boatyard Ltd, Ilemela jijini Mwanza jana. **PICHA: TEMESA**

# TRA yabuni mbinu kuwabana wateja

**Na Paul William,** MOSHI

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imeanzisha mbinu mpya kuwabana wafanyabiashara wasio waaminifu baada ya kuanza kujilipa kodi kutokana na wateja wao kwa kuchukua fedha moja kwa moja kwenye akaunti ya mteja mwenyewe.

Akizungumza na Nipashe jana katika mahojiano maalum kuhusu utaratibu huo, Meneja wa TRA Mkoa wa Kilimanjaro, Gabriel Mwangosi, alisema kitendo hicho cha kuchukua kodi moja kwa moja katika akaunti ya mteja, litakuwa likifanyika kwa wateja ambao wamekuwa wakikaidi kulipa wenyewe kwa hiari.

"Wako walipakodi ambao wamekuwa hawalipi kodi kwa wakati na kusababisha kuwa na madeni ya kodi. Hivi sasa TRA tutakuwa tukichukua kodi zetu moja kwa moja kwenye akaunti za benki za wateja hao," alisema Mwangosi.

Alisema changamoto kubwa wanayokutana nayo kwa sasa katika mpango huo wa kuchukua fedha ya kodi moja kwa moja inatokana na baadhi ya walipakodi ambao taarifa zao zipo TRA, zinatofautiana na taarifa za benki.

Pia alisema wako baadhi ya wateja ambao wamekuwa wakiandika hundi kwa ajili ya kulipa kodi, lakini wanapofika benki wanakuta fedha hizo hazipo katika akaunti ya mteja, hivyo kuwasababisha usumbufu maofisa wake.

Kwa mujibu wa Mwangosi, kwa sasa maofisa wa mamlaka hiyo wamekuwa wakipita mtaa kwa mtaa kuwaelimisha walipakodi kutambua umuhimu wa kulipa kodi kwa wakati pamoja na kusikiliza kero zinazowakabili katika masuala ya kodi.

Pia alisema changamoto nyingine waliyobaini katika utekelezaji wa kutembelea wateja ni kuwapo wafanyabiashara ambao hawajalipa kodi kwa muda mrefu, tangu mwaka 2016 na wengine wakiwa hawatumii mashine za kutolea risiti za kielektroniki (EFD).

Mwangosi alitoa mfano wa hujuma zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu baada ya siku mbili zilizopita walipowatembelea wafanyabiashara 51 na kati yao 19 wakiwa wamevunja sheria mbalimbali za kikodi na kutozwa faini.

# Kilimanjaro kupatiwa mbolea tani 1,200

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Kilimo, Omari Mgumba, amesema serikali inakusudia kuupatia mkoa wa Kilimanjaro tani 1,200 za mbolea ya kupandia na kukuza mazao mbalimbali ya chakula na biashara.

Amesema hadi kufikia sasa zaidi ya tani 400 zimeshawasili mkoani humo kwa kutumia treni ya mizigo iliyozinduliwa Julai, mwaka huu, na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Mgumba aliyasema hayo wakati wa kongamano la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Kilimanjaro, lililofanyika wiki iliyopita kwa ajili ya kumpongeza Rais John Magufuli kwa kutekeleza ilani ya uchaguzi kwa mwaka 2015 hadi 2019.

"Mkoa wa Kilimanjaro una zaidi ya hekta 83,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Sasa niwape habari njema kwamba mwaka huu serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 2.2 kwa ajili ya kuimarisha sekta ya kilimo na hasa umwagiliaji katika mkoa wa Kilimanjaro. Tumeagizwa na Mheshimiwa Rais tulete tani 1,200 za mbolea," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema mkoa wa Kilimanjaro pia umepatiwa zaidi ya lita 2,000 za dawa mbalimbali za viuatilifu kwa ajili ya kupambana na wadudu waharibifu wa mazao mashambani.

Udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao kwa kutumia viuatilifu, hugharimu fedha nyingi kwa mkulima na hivyo kumlazimu kupambana nao ili kupata mavuno.

Alisema wataalamu wanaeleza kuwa, kwenye kilimo iwapo wakulima watatumia viuatilifu sahihi kulingana na aina za wadudu wanaoshambulia shamba au mazao husika, watakuwa wamepata suluhisho la kudumu la tatizo hilo.

Aina ya wadudu waharibifu wa mazao hasa nafaka ni pamoja na vidukari (aphids), viwavi na 'ballworms'.

Wadudu hao hudhoofisha mimea kwa kufyonza na kutoboa kwenye mimea husika, lakini huambukiza magonjwa ya virusi kwenye mimea inayoshambuliwa.

**Mkoa wa Kilimanjaro una zaidi ya hekta 83,000 zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Sasa niwape habari njema kwamba mwaka huu serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni 2.2 kwa ajili ya kuimarisha sekta ya kilimo na hasa umwagiliaji katika mkoa wa Kilimanjaro. Tumeagizwa na Mheshimiwa Rais tulete tani 1,200 za mbolea**



Ukurasa 15

**Migogoro ya mipaka ni kero uchaguzi serikali za mitaa**

CCM ni kiwanda chenye hazina ya viongozi bora



Ukurasa 19



Ukurasa 20

**Rais Abbas afika ukingoni**


# siasa

JUMATANO AGOSTI 28, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe




Ukurasa 18

**Afrika bado haijajipanga kuuingia mtangamano**

BAADA YA MIAKA 55

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano-mwisho

PIUS Msekwa (84), ni miongoni mwa wakongwe waliobeba wasifu mkubwa katika kulitumikia taifa, ikiwamo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Katibu Mtendaji wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), pia mshauri muhimu wa serikali na chama (TANU na CCM) kwa mengi.

Pia Msekwa ana sifa nyingine ya kipekee, kuwa mdau anayefahamu fika picha kamili ya dhana ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, ambao mzizi wake kwa hatua, wengi hawaufahamu kwa kina kutokana na umri na si yote yaliyokuwa bayana.

Ili kuliweka hilo wazi kwa kina tangu vuguvugu na kuundwa Muungano huo, ameamua kuandika kitabu alichokizindua siku chache zilizopita, kiitwacho Historia ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, kinachoweka undani wa historia kwa hatua. Gazeti hili limeamua kuchapisha maudhui yake kwa hatua, kila siku kama ya leo katika jarida hili la Siasa na leo hii tunaendelea kutokea tulipoishia wiki iliyopita. Endelea na sehemu hii ya mwisho ya kitabu hicho inayoanzia na sehemu ya 7.2.1 inayozungumzia kikao kilichofanyika.

7.2.1 Chafanyika Kikao cha pamoja

Hatua ya kwanza ilikuwa ni kufanya kikao cha pamoja kilichojumuisha Halmashauri Kuu ya Taifa, Kamati ya Wabunge wote wa CCM, pamoja na Kamati ya Wawakilishi wote wa CCM, am-

**INAENDELEA UK.16**



Mzee Pius Msekwa. **PICHA: MTANDAO**

**Dk. Bashiru: Hakuna mwanaCCM atakayekwamishwa uchaguzi serikali za mitaa** Ukurasa 14

# Dk. Bashiru: Hakuna mwanaCCM atakayekwamishwa uchaguzi

## • Kitakachomkwamisha mtu kitawekwa wazi • Kama ni sifa, kama ni ushindani • Kinachoongoza ni Katiba, kanuni na taratibu

**Na Enock Charles**

WAKATI Taifa likielekea kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba 24, na uchaguzi mkuu mwakani, Nipashe kupitia mwandishi wake ilifanya mahojiano na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, kuhusiana na uchaguzi huo na masuala mengine mbalimbali. Fuatilia sehemu ya kwanza ya mahojiano hayo kwa siku ya leo...

**SWALI: Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimejipanga vipi kwa uchaguzi wa serikali za mitaa?**

**JIBU:** Tumejipanga vizuri sana na tukiwa na kianzio kizuri. Maeneo yote ambayo tunayashikilia tayari ya serikali za mitaa, vitongoji na vijiji, tumejipanga kutoyapoteza. Na yale ambayo yapo kwenye vyama vya upinzani, tumejipanga pia kushinda. Tunawashukuru wananchi kwa kuendelea kukiunga mkono chama chetu nchi nzima, lakini pia viongozi wa upinzani katika ngazi hizo ambao wamerejea kwenye chama chetu nao tumewapokea kwa shangwe na tunawashukuru sana kwa heshima hiyo, kwani tumeongeza nguvu kutoka vyama vya upinzani.

Tumepata pia wabunge wengi waliorudi...tumepata madiwani wengi waliorudi na wanachama wengine kutoka karibu vyama vyote vya upinzani. Na hiyo ni nguvu kubwa lakini pia tumejipanga kwa sababu tumepata wanachama wengi wapya hasa vijana. Tulikuwa na kadi zaidi ya milioni mbili kwa zaidi ya miezi sita tumesajili wanachama wapya na hizo zote ni kura.

**SWALI: CCM ina wanachama wangapi kwa sasa?**

**JIBU:** Tupo tunahakiki kwa kutumia mfumo mpya wa Tehama. Kufikia Desemba, ndio tunaweza tukajua ni kiasi gani lakini rekodi tuliyonayo ni wanachama milioni 12 mpaka milioni 15. Ingawaje sasa majina unapohakiki kuna wengine wanafariki, kuna wengine si hai, hawalipi ada. Kwa hiyo ni vigumu sana kwa sasa kwa chama kikubwa kama hiki na kina wanachama nchi nzima kusema sasa. Hata hivyo hatuko chini ya wanachama milioni 10 ambao wako hai na rekodi baada ya hizi kadi kuzigawa tunafikia milioni 14 mpaka 15...tuko kwenye uhakiki mpya, zoezi ambalo linaendelea nchi nzima.

**SWALI: Utaratibu wa kuwapata wagombea wa CCM katika uchaguzi wa serikali za mitaa kwa sasa ni upi?**

**JIBU:** Kwa uchaguzi wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, wanachama wote watapiga kura kwenye tunachokiita Mkutano Mkuu wa wanachama wote wa tawi. Kwa hiyo kura za maoni zitapigwa katika ngazi ya tawi katika siku ya kupiga kura ambayo itapangwa. Kura za maoni za wagombea ngazi ya kijiji na mtaa, wanaCCM wote watapigakura zao za maoni wakiwa katika matawi ya vijijini au matawi ya mitaani kwa upande wa mjini ambako wanaishi. Hawa ni wale ambao ni wanachama kwa mujibu wa Ibara ya 35(6) ya Katiba yetu. Na kwa upande wa vitongoji, kura za maoni zitapigwa na wanachama wote wa CCM katika kitongoji kinachohusika.



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally. **PICHA: MTANDAO**

> Kwa ufupi mchakato wetu ni wa kidemokrasia. Mchakato utakuwa wazi na fomu ni bure tofauti na za ubunge na udiwani, ambazo ni za gharama.

Lakini upo utaratibu wa kuwapata wagombea wa kupigiwa kura za maoni ambapo mgombea yeyote wa CCM, kabla ya kupigiwa kura za maoni atajadiliwa kwanza na Kamati ya Siasa ya tawi lake na hatimaye kamati ya siasa ya kata yake itafikiria na kuteua majina ya wana CCM wasiozidi watatu kwa kila kitongoji walioomba kugombea uenyekiti wa kitongoji ili wakapigiwe kura za maoni na mkutano wa wanachama wote wa CCM wanaoishi katika kitongoji hicho. Kwa hiyo kutakuwa na kujadiliwa kwa wanaoomba, halafu baadaye yatateuliwa majina matatu, ndiyo yatakwenda kupigiwa kura kwa upande wa kitongoji.

Na mgombea yeyote wa CCM anayetaka kuingia kwenye chombo cha dola kwa nafasi ya uenyekiti wa kijiji ama uenyekiti wa mtaa, kabla ya kupigiwa kura za maoni atajadiliwa kwanza na kamati ya siasa ya tawi lake na kamati ya siasa ya kata yake na hatimaye kamati ya siasa ya wilaya, itafikiria na kuteua majina ya wana CCM wasiozidi watatu kwa kila kijiji ama mtaa walioomba kugombea uenyekiti wa kijiji ama mtaa ili wakapigiwe kura za maoni na mkutano wa wanachama wote katika tawi husika.

Kwa hiyo mikutano ya wanachama wote kwenye matawi ndiyo itakayohusika kwenye kura za maoni, lakini mchakato utaanza kwa kuwafikiria waombaji katika ngazi husika na fomu tayari tumeshaziandaa na tunaendelea kuzisambaza. Kwa hiyo sharti la kwanza lazima awe mwanachama lakini baadaye katiba na kanuni za CCM ndizo zitakazoongoza na kanuni hizi ni za mwezi Juni mwaka huu. Zimepitishwa na Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM mwezi Juni, katika kikao kilichopita na Katiba hii ni ya mwaka 1977 toleo la mwaka 2017.

Kwa ufupi mchakato wetu ni wa kidemokrasia. Mchakato utakuwa wazi na fomu ni bure tofauti na za ubunge na udiwani, ambazo ni za gharama.

**SWALI: Kuna suala la wanachama wengine ambao hawajawahi kugombea nafasi yoyote ndani ya CCM na wanataka kugombea safari hii, lakini inawezekana wakakwamishwa na waliopo. Je, unalizungumziaje hili?**

**JIBU: Uhai wa mwanachama sio umri k**ama mtoto mdogo katika kupiga kura za kikatiba, ambapo lazima uwe na umri wa miaka 18. Lakini kuwa mwanachama unapata haki zinazolingana bila kujali umetumia muda gani kwenye chama. Ukishapitia mchakato wa kuomba uanachama, ukajadiliwa kwenye tawi lako ukakubaliwa, ukapewa uanachama, ukalipia kadi Sh. 300, ukalipia kila mwezi Sh. mia mia wewe ni mwanachama.

Na mwanachama anatajwa si kwa umri wake au kwa muda aliokuwa mwanachama hapana, haki zinalingana. Na ukizisoma zile haki hukuti kwamba kuna haki za madaraja. Chama cha namna hiyo, kitakuwa si chama cha kidemokrasia. Katika Ibara ya 14, ziko haki tano. Kwanza haki ya kushiriki katika shughuli zote za CCM kwa kufuata utaratibu uliowekwa, kwa hiyo kikubwa hapo ni utaratibu. Haki ya kuhudhuria na kutoa maoni yake katika mikutano ya chama pale ambapo anahusika kwa mujibu wa Katiba.

Haki ya kujitetea na kutoa maelezo yake mbele ya kikao cha CCM kinachohusika katika mashtaka yoyote yaliyotolewa juu yake pamoja na haki ya kukata rufani ya kwenda kikao cha juu zaidi cha CCM kama kipo, endapo hakuridhika na hukumu iliyotolewa. Na haki ya kumuona kiongozi yeyote wa CCM kwa mujibu wa utaratibu.

Mimi ndiye Mkurugenzi wa uchaguzi katika chama, ninasaidiwa na makatibu wa chama ngazi zote. Kwa hiyo kwa mfano kwenye matawi mkurugenzi wa uchaguzi katika ngazi ya tawi ni katibu wa tawi. Kwenye wilaya, katibu wa wilaya. Kwenye mkoa, katibu wa mkoa na kitaifa ndio mimi. Na tunao mfumo wa wazi na wa haki, hivyo wasiwe na wasiwasi wowote. Wasiporidhika, kuna taratibu za kukata rufani, rufani zikasikilizwa na haki ikatendeka. Nawahakikishia hakuna atakayekwamishwa kwa namna yoyote. Kitakachomkwamisha mtu kitawekwa wazi kama ni sifa, kama ni ushindani, lakini kinachoongoza ni katiba, kanuni na taratibu zetu.

**SWALI: Vyama vya upinzani vinalalamikia kanuni zilizotolewa hivi karibuni za uchaguzi wa serikali za mitaa. Kwa upande wa CCM, hili likoje?**

**JIBU:** Sisi tulishiriki na hapakuwa na maoni ya CCM peke yake, yalichukuliwa maoni ya wadau na wala sio vyama vya siasa peke yake. Mchakato ule mimi nimeufuatilia na nimeridhika kuwa ulikuwa ni mchakato wa wazi, huru na haki. Ni mchakato ambao unakidhi sifa za mchakato wa kidemokrasia. Taasisi zisizokuwa za kiserikali zimehusika, vyama vyote vimehusika na wengine tumekutana kwenye mchakato huo na sisi tumetoa maoni yetu. Na sisi tuna maoni ambayo hayakukubaliwa, hatujatoka hadharani kusema ni mangapi lakini mwafaka umeshafikiwa.

**SWALI: Maoni ya CCM yamechukuliwa kwa kiasi gani katika kanuni hizi mpya?**

**JIBU:** Sisi sasa hatupimi kwamba haya ndiyo yametupwa na haya ndio yamekubaliwa. Sisi tunasema kwamba kuna kanuni ambazo tunaridhika kwamba zimetosheleza wala hatuhitaji kwamba ni kanuni ngapi. Hata ungeweza kusema moja ikapatikana hiyo hiyo moja ni asilimia 100, haina maana yoyote hapa. Tunachokizungumza ni kwamba ipo kanuni ambayo imetengenezwa kwa mujibu wa mahitaji ya kidemokrasia, na mahitaji ya kidemokrasia ni haki ya mtu kusema na kusikilizwa. Na haki ya kujieleza na kushiriki na hao, mimi naheshimu mawazo yao, hata kulalamika pia ni sehemu ya demokrasia. Na hata kutoridhika, ukatoka hadharani ukasema siridhiki, ni sehemu ya demokrasia. Lakini ninachowaomba vyama vya upinzani na sisi CCM tupo tayari, tuache visingizio.

ITAENDELEA WIKI IJAYO

# Migogoro ya mipaka ni kero uchaguzi serikali za mitaa

Na Sabato Kasika

UCHAGUZI wa serikali za mitaa ukihusisha vijiji 12,319, mitaa 4,264, vitongoji 64,384, lakini vilevile wenyeviti wa mitaa, vijiji, vitongoji na wajumbe wa halmashauri wa maeneo hayo, unatarajia kufanyika Novemba 24 mwaka huu kama ambavyo serikali imetangaza.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Selemani Jafo, ndiye aliyetangaza tarehe hiyo wiki iliyopita na kutoa mtiririko wa matukio yatakayotangulia kabla ya uchaguzi huo.

Mtiririko huo unajumuisha mipaka ya vijiji na vitongoji ikiambatana na tangazo la majina na mipaka ya vijiji na vitongoji kwa siku 72 kabla ya siku ya uchaguzi.

Pia msimamizi wa uchaguzi kutoa maelekezo ya uchaguzi, siku 62 kabla ya siku ya uchaguzi.

Vilevile uteuzi wa mwandikishaji wa wapigakura, msimamizi wa uchaguzi kumteua mtumishi wa umma, ambaye ataandikisha na kuandaa orodha ya wapigakura, huku uandikishaji ukifanyika kwa siku saba.

Mtiririko huo wa matukio ni mrefu, ila nimetaja machache, lengo ni kutaka kuzungumzia zaidi suala la mipaka ambalo limekuwa ni changamoto hadi kusababisha baadhi ya watu kushindwa kushiriki katika uchaguzi.

Kwa mfano uchaguzi wa mwaka 2014, katika baadhi ya mitaa kuna watu walilalamikia suala la mipaka wakidai kuzungushwa kila walipokwenda kwenye vituo kupigakura.

Mfano mmojawapo ni kwenye baadhi ya mitaa ya Kata ya Kwembe Dar es Salaam, ambako baadhi ya wapigakura walidai kuzuiwa kupigakura wakiambiwa siyo wakazi wa maeneo waliyokwenda kupigakura.

Waliambiwa vituo vyao vya kupigakura ni vya mitaa mingine, lakini walikoelekezwa nako wakakataliwa na kujikuta wakishindwa kushiriki katika uchaguzi huo, huku tatizo kubwa likiwa ni mipaka.

Bahati nzuri serikali imeiona changamoto hiyo na kutenga siku 72 za kushughulikia suala la mipaka kabla ya uchaguzi ili kuhakikisha kila Mtanzania mwenye sifa zinazotakiwa, anashiriki uchaguzi huo.

### KUMALIZA TATIZO LA MIPAKA

Mikoa na halmashauri inaelekezwa kumaliza migogoro iliyopo ndani ya uwezo wake kama ya wilaya na wilaya, kijiji na kijiji, kitongoji au mtaa na kadhalika ili kuepusha kuvuruga uchaguzi huo.

Serikali inasema imeshaandaa orodha ya mikoa, wilaya, halmashauri, vijiji, vitongoji na mitaa ili kuondoa matatizo madogo madogo yanayojitokeza wakati wa uchaguzi kama ilivyokuwa kwa chaguzi zilizopita.

"Mwaka huu matarajio ni kuondoa kabisa kasoro na migogoro isiyo na tija kwa kuhakiki maeneo ya utawala ikiwamo kumaliza migogoro inayojitokeza maeneo yote ya utawala nchini, kazi ikikamilika litatolewa tangazo la serikali kuhusu maeneo hayo ya utawala," anasema Mhandisi Joseph Nyamhanga.



Waziri wa Tamisemi, Selemani Jafo. **PICHA: MTANDAO**

> Wengine ni wenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa (kundi mchanganyiko wa wanaume na wanawake) na wajumbe wa kamati ya mtaa (kundi la wanawake) katika mamlaka za miji.

Huyo ni Katibu Mkuu Tamisemi anayewataka wakurugenzi wa halmashauri nchini kufanya maandalizi ya kutosha ikiwamo kuhakiki orodha ya vijiji, vitongoji na mitaa, idadi ya maeneo ya utawala na majina yake kwa usahihi.

"Ni lazima mikoa na halmashauri wamalize migogoro iliyopo ndani ya uwezo wao kama ya wilaya na wilaya, kijiji na kijiji, kitongoji au mtaa na kadhalika ili kuepusha kuvuruga wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa," anasema.

Mhandisi Nyamhanga alikaririwa na vyombo vya habari akisema hayo hivi karibuni wakati akizungumza na wajumbe wa Kamati Tendaji ya Wilaya ya Hanang (CHMT) alipohitimisha ziara yake ya kikazi wilayani humo.

### UFAFANUZI WA WAZIRI

Waziri Jafo anasema, tangu kurejeshwa kwa mamlaka za serikali za mitaa katika mfumo wa utawala kupitia Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura ya 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura ya 288, uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika ngazi ya mtaa, kijiji na kitongoji, umekuwa ukifanyika kila baada ya miaka mitano.

Anafafanua kuwa uchaguzi wa mwisho ulifanyika mwezi Desemba mwaka 2014, hivyo uchaguzi mwingine unatakiwa kufanyika mwaka 2019, huku akiwa ametangaza kuwa utafanyika Novemba 24.

"Uchaguzi huu unaongozwa kwa kanuni za uchaguzi wa viongozi wa mamlaka za serikali za mitaa ngazi ya vijiji, vitongoji na mitaa katika mamlaka za wilaya na mamlaka za miji, kwa mujibu wa matangazo ya Serikali Na. 371, 372 373 na 374 ya mwaka 2019," anasema Jafo.

Anabainisha kuwa nafasi zitakazowaniwa katika uchaguzi huo kuwa mwenyeviti wa kitongoji katika mamlaka za miji midogo, kwa nafasi hiyo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za miji midogo za mwaka 2019, (Tangazo la Serikali Na. 371 la Mwaka 2019).

"Wengine ni wenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa (kundi mchanganyiko wa wanaume na wanawake) na wajumbe wa kamati ya mtaa (kundi la wanawake) katika mamlaka za miji," anasema na kuongeza:

"Kwa nafasi hizo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa mtaa na wajumbe wa kamati ya mtaa katika mamlaka za miji za mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 372 la Mwaka 2019)."

Anasema mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za wilaya.

Kwamba kwa nafasi hizo zitaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za wilaya za mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 373 la Mwaka 2019).

"Mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi mchanganyiko la wanaume na wanawake), wajumbe wa halmashauri ya kijiji (kundi la wanawake) na wenyeviti wa vitongoji katika mamlaka za miji," anasema Jafo na kuongeza:

"Kwa nafasi hizo, uchaguzi utaendeshwa kwa mujibu wa kanuni za uchaguzi wa mwenyekiti wa kijiji, wajumbe wa halmashauri ya kijiji na mwenyekiti wa kitongoji katika mamlaka za miji za mwaka 2019 (Tangazo la Serikali Na. 374 la Mwaka 2019)."

### UMUHIMU WA UCHAGUZI

Kimsingi utawala wa kijiji ni miongoni mwa tawala katika serikali za mitaa za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ukiwa chini kimuundo ukitanguliwa na utawala wa kitongoji.

Jambo la muhimu kutambua ni kwamba utawala wa chini haina maana kuwa umuhimu wake ni mdogo, bali ni kupitia utawala huo ndiko mambo mengi huamriwa na kupangwa na tawala za juu kama serikali na kutekelezwa.

Katika utawala wa kijiji huelekeza wananchi kutumia madaraka yao ya kidemokrasia kuamua juu ya mambo yanayowahusu kama wanakijiji moja kwa moja, bila kupitia mlolongo au urasimu mrefu.

Aidha, wananchi wanashiriki katika serikali za mitaa kupitia vikao au mikutano kujadili na kutoa mapendekezo yao kuhusu mipango na matatizo yanayowakabili kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi na kurahisisha uboreshaji wa huduma za kijamii katika maeneo yao wanamoishi.

Yapo mengi yanayohusu serikali za mitaa, kikubwa zaidi cha kutambua ni kwamba ushiriki wa wananchi ni jambo la msingi kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao katika vijiji na mitaa.

# Pius Msekwa aeleza misumari ya siri iliyoshikilia Muungano -mwisho


Moja ya manjonjo yaliyoambatana na maadhimisho ya sherehe za Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

**INATOKA UK.13**

bacho kilifanyika mjini Dodoma tarehe 12 Agosti, 1993. Baada ya mjadala mrefu na wa wazi, kikao hicho kilikubaliana kwamba, muundo wa serikali mbili ndiyo sera ya Chama Cha Mapinduzi. Lakini, kilikubaliana vilevile, kwamba, suala hili la muundo wa serikali lipelekwe kwa wanachama wote ili kupata maoni yao kama wanataka kuendelea na sera hiyo ya muundo wa serikali mbili, au wangependa kuibadilisha. Na kwamba, wafanye hivyo kwa njia ya kupiga kura za maoni (referendum) kuonyesha kama wanataka ama tubaki na sera ya serikali mbili; au tubadili na kuwa na sera ya serikali tatu; au tubadili na kuwa na sera ya serikali moja.

7.2.2 Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa

Kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM kilifanyika mjini Dodoma tarehe 14 hadi 16 Oktoba, 1993. Kikao hicho kilijadili taarifa ya serikali kuhusu Azimio la Bunge lililoitaka serikali 'iandae na kusimamia utaratibu wa kuwashirikisha wananchi na taasisi mbalimbali kutoa mapendekezo yao juu ya muundo mwafaka wa Muungano, ambao ungezingatia haja ya kuwapo kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano."

> Lakini, yale malengo yaliyobaki, yaani lengo la pili, la kuimarisha ulinzi wa nchi, pamoja na lengo la tatu, la kudumisha udugu na maelewano; kwa hakika hayo yamefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana.

Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama iliagiza Kamati Kuu ya Chama, pamoja na mambo mengine, iandae waraka wa maelekezo juu ya namna ya kupata maoni ya wana-CCM nchini kote. Kwa mujibu wa maelekezo yaliyotolewa na Kamati Kuu, wana-CCM na viongozi wa ngazi zote za Chama, walitakiwa kutoa maoni yao kwa kupiga kura ya siri katika mikutano ya wanachama wote katika matawi yao.

Baada ya uamuzi huo Mwalimu Nyerere alitoa maoni yake kuwa "Siamini hata kidogo kwamba, wanachama wa CCM watakubali hoja ya serikali tatu."

Baada ya hapo, maandalizi yalifanywa kwa ajili ya kuendesha zoezi la kura ya maoni itakayopigwa na kila mwanachama wa CCM katika matawi yao wanakoishi, au matawi wanakofanya kazi. Zoezi hilo lilifanyika mnamo mwezi Machi 1994, ambapo wana-CCM walitakiwa kuonyesha kwa kura ya siri, ni muundo gani wa Muungano wanaoupendelea kati ya serikali moja, serikali mbili au serikali tatu.

Matokeo ya kura hiyo ya maoni yaliwasilishwa kwenye kikao cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama kilichofanyika mwezi Agosti 1994, na yalionyesha kwamba, wanachama walio wengi zaidi (61.75%) katika matawi karibu yote, waliunga mkono muundo wa Serikali mbili. Kwa hiyo, sera ya Chama cha Mapinduzi ya muundo wa Muungano wa serikali mbili, ikawa imeridhiwa na wanachama wote wa CCM.

Chama kilichukua hatua hiyo ya kufanya referendum kwa sababu tu ya kuepusha mgogoro wa kikatiba ambao ungeweza kuwapo. Kwani, lengo halisi la kufanya kura hiyo ya maoni ya wanachama wote wa CCM lilikuwa kuwaonyesha wabunge hao wa CCM kwamba, azimio lao kumbe halikuwa linawakilisha matakwa ya wana CCM wenzao walio wengi zaidi. Kwa hakika, mkakati huo ulifanikiwa, kwani Bunge lilikubali kufuta azimio lake hilo lenye utata. Kwani, hapo baadaye katika kikao kilichofuata cha kawaida cha Bunge cha mwezi Oktoba 1994, matokeo hayo yaliwasilishwa kwa Wabunge husika katika kikao chao cha Kamati ya Wabunge wote wa CCM. Baada ya kuyapokea, walikubaliana kurejea bungeni, na kufuta azimio lao la awali la kudai kuwapo kwa Serikali ya Tanganyika. Tatizo hilo likawa limetatuliwa ipasavyo.

7.3 Hofu ya kuvunjika kwa Muungano

Tumekwishazungumzia chemsha bongo iliyopo, kwamba, katika malumbano kuhusu ni muundo gani wa Muungano unaofaa zaidi kati ya serikali mbili na serikali tatu, kila upande unadai kwamba, muundo wanaoutetea ndiyo kinga ya Muungano usivunjike. Ni vema pia tuangalie vizuri uzito wa hofu hii ya Muungano kuvunjika.

7.3.1 Sababu za kweli za kuvunjika kwa Muungano

Kwa kurejea uchambuzi wetu hapo juu, tumeainisha mambo mawili yanayoweza kusababisha kuvunjika kwa Muungano wetu, kwamba ni:

- Kutoweka kwa utashi wa kisiasa kwa yeyote miongoni mwa viongozi wakuu wa pande zote mbili, na
- Vitendo viovu vya viongozi wa ngazi ya taifa wenye mamlaka husika.

7.3.2 Kinga dhidi ya Muungano kuvunjika

Kwa hakika zipo kinga za kikatiba, kisheria na kihistoria, ambazo zinaweza kuwabana viongozi au wanasiasa wengine watakaoingia katika kishawishi cha kutaka kuvunja Muungano, wasiweze kufanya hivyo.

(a)Kinga za kikatiba na kisheria

Tumekwishakutaja Ibara ya Katiba inayowabana viongozi wakuu kwa njia ya kuwataka kula kiapo cha kuulinda Muungano. Ndiyo kusema kwamba, kiongozi atakayekwenda kinyume na Ibara hiyo atakuwa amevunja katiba, na atastahili kupewa adhabu ya kuvunja Katiba ya nchi.

Lakini, vilevile, kwa upande wa sheria za kawaida, ipo sheria namba 22 ya mwaka 1964. Kifungu cha kwanza cha sheria hiyo kinasomeka kama ifuatavyo:

- "From Union Day and ever after, the Republic of Tanganyika and the Peoples' Republic of Zanzibar are United into one Sovereign State of Tanganyika and Zanzibar."

Maneno hayo ya "and ever after" yaliyomo katika sheria hiyo, yanamaanisha kwamba, Muungano huu umekusudiwa kudumu milele. Maana yake nyingine ni kwamba, kitendo cha kuuvunja ni kosa kisheria.

(b)Kinga ya udugu wa kihistoria

Kama alivyosema Rais Nyerere, "Tanganyika na Zanzibar ni nchi ndugu, tunashirikiana kwa historia, lugha, mila, tabia na siasa." Kuna matumaini kwamba, udugu huo wa kihistoria utaweza kuzuia wanasiasa wenye nia mbaya ya kuvunja Muungano, waone ugumu wa kuekeleza nia yao hiyo.

(c)Kinga dhidi ya vitendo viovu vya viongozi

Lakini, katika hali ya hulka za kibinadamu zinavyotofautiana, wanaweza bado wakatokea viongozi wenye nia mbaya na Muungano huu, basi, wakatengeneza njama ya kuuvunja kwa sababu zao za ubinafsi tu. Hapo mapema, tulinukuu maneno ya Mwalimu Nyerere aliposema kwamba "Yeltsin wa Tanganyika atavunja Muungano." Mwalimu alikuwa akimzungumzia kiongozi mmoja wa Urusi mwenye jina hilo la 'Yeltsin' ambaye, kwa ujeuri wake tu, alisababisha kuvunjika kwa Muungano uliokuwapo wa nchi za USSR (Union of Soviet Socialist Republics). Ni katika kikao kimojawapo cha mfululizo wa vikao vya Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi vilivyofanyika katika juhudi ya kutatua mgogoro uliokuwa umesababishwa na Azimio la Bunge la kutaka 'Serikali ya Tanganyika,' ndipo Mwalimu Nyerere alipotumia mfano huo wa 'Yeltsin' akiutumia kujenga hoja yake kwamba kwa kuwa Tanganyika ndiyo inayobeba sehemu kubwa zaidi ya gharama za kuendesha Muungano huu, akitokea Rais wa Serikali ya Tanganyika ambaye atakuwa na jeuri kama huyo Yeltsin, ataweza kuidai Zanzibar ichangie sehemu kubwa zaidi katika gharama za kuendesha Muungano, na kama Zanzibar itashindwa kufanya hivyo, basi, 'Yeltsin huyo wa Tanganyika,' atakuwa amepata kisingizio cha kuvunja Muungano huu. Kutokuwapo kwa Serikali ya Tanganyika kunazuia kuwapo kwa 'Yeltsin huyo wa Tanganyika."


Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere (kushoto) na Mzee Abeid Karume, Waasisi wa Muungano wa Tanzania. **PICHA: MTANDAO**

(d)Kinga ya Serikali mbili

Muundo wa serikali mbili pia ni kinga dhidi ya kuvunjika kwa Muungano kwa sababu mbili zifuatazo: Kwanza, kutokuwapo kwa 'Serikali ya Tanganyika,' kunaondoa uwezekano wa kuwapo kwa 'Yeltsin wa Tanganyika,' anayeweza kuleta madhara kama hayo yaliyohofiwa na kuonambali, Mwalimu Nyerere. Lakini, pili, muundo wa serikali mbili, pia unaondoa tatizo kubwa linalowakumba hivi sasa, wananchi wa upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Cameroon huko Afrika Magharibi; tatizo ambalo, kimsingi, ni matokeo ya muundo wao wa serikali moja tu ya Muungano, ambapo serikali hiyo (ambayo imejaa wazungumza Kifaransa) imeamua kufanya jeuri mbaya ya kuwanyima haki wanazostahili kuwa nazo, wenzao wa upande wa pili unaozungumza Kiingereza. Hii ni kwa sababu watu wa upande huo wa pili hawana serikali yao inayosimamia mambo ya ndani ya eneo lao, hususan elimu, pamoja na mengine yote ya ndani. Badala yake, mambo hayo yote yanaamuliwa na serikali ya Muungano tu, (ambayo ni ya wazungumza Kifaransa). Katika kutekeleza jeuri yao hiyo mbaya sana, serikali hiyo ya Muungano imegeuka kuwa ndiyo 'Yeltsin' wa kwao, wakaamua kibabe kufifisha matumizi ya lugha ya Kiingereza, na kuwaamuru watumie lugha ya Kifaransa tu.

Hatua hizo za uonevu zimezusha hasira kubwa miongoni mwa watu wa upande wa pili, hadi kufikia hatua ya kuzalisha kundi la waasi wanaoleta ghasia nyingi katika harakati zao za kudai kujitoa katika Muungano huo, ili waunde taifa lao tofauti litakaloitwa "Ambazonia."

Ni dhahiri kwamba, muundo wetu wa serikali mbili ambao unawapatiwa wananchi wa upande wa pili wa Muungano, yaani, Zanzibar, kujiamulia wenyewe mambo yao yote ya ndani, ikiwa ni pamoja na elimu na mengine yote yasiyokuwa ya Muungano, umetuwezesha kuepusha hatari ya kutokea 'Yeltsin' katika Serikali ya Muungano, atakayeweza kufanya jeuri kama hiyo ya kuwanyang'anya Wazanzibar, haki ya kujiamulia mambo yao wenyewe; na kwa ajili hiyo, kuzalisha migogoro kama hiyo inayotokea huko Cameroon.

7.4 Je, malengo yaliyokusudiwa ya Muungano huu yamefikiwa?

Tarehe 26 Aprili, 2017, tulisherehekea mwaka wa 53 wa uhai wa Muungano wetu. Kama ambavyo ingetegemewa, watu wengi, pamoja na vyombo mbalimbali vya habari, vilitumia fursa hiyo kufanya tathmini ya ufanisi wa Muungano wetu katika miaka hiyo mingi. Kwa mfano, Waziri wa nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais mwenye dhamana ya kushughulikia masuala ya Muungano, Mhe January Makamba (Mb); alitoa kauli kwamba "Serikali ya Muungano imepata mafanikio makubwa katika kutatua kero za Muungano zilizojitokeza katika kipindi hiki". Naye mhadhiri mmoja wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Bashiri Ally, akiafiki kauli hiyo ya Waziri Makamba, aliongeza neno kwamba "Kila tatizo lililotatuliwa limeongeza thamani ya kuwapo kwa Muungano huu," na pia, kwamba, "Kazi ya kulinda na kudumisha Muungano ni kazi endelevu, kwa hiyo, nchi haipaswi kutosheka na mafanikio yaliyopatikana katika kutatua baadhi ya kero za Muungano. Inabidi vilevile, kupima na kuona kama Muungano umefanikiwa katika kutekeleza malengo muhimu yaliyokusudiwa na waasisi wake, yanayohusu uboreshaji wa maisha ya wananchi.

> Kwa mfano, suala kwamba, ulinzi wa nchi yetu uko imara kabisa, lilipata uthibitisho pale ambapo majeshi ya Uganda yalipotumwa na Rais wa nchi hiyo, Iddi Amin Dada, kuishambulia nchi yetu...

Ndugu Bashiru Ally baadaye alichaguliwa kuwa Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi.

Kutokana na maoni ya msomi huyo, ndipo linakuja swali hili: je, malengo yaliyokusudiwa katika kuunda Muungano huu, yamefikiwa?

7.5 Tujikumbushe malengo yaliyokusudiwa

Malengo yaliyokusudiwa na waasisi wa Muungano wetu, yameainishwa vizuri katika Sura ya Kwanza ya kitabu hiki. Kwa kifupi ni kwamba, kulikuwa na malengo makuu matatu yafuatayo: (i) Kutekeleza azma ya kuunda Umoja wa Bara la Afrika; (ii) Kuimarisha ulinzi wa nchi; na (iii)Kuimarisha udugu na maelewano yaliyokuwapo baina ya watu wa nchi hizi zilizoungana.

Kama ambavyo sote tunajua, lengo la kwanza la kuunda Umoja wa Afrika halikufanikiwa kabisa. Lile wazo la Mwalimu Nyerere kwamba, "Ikiwa nchi mbili ambazo ni marafiki, na ni jirani, zikiweza kuungana, muungano huo utakuwa ni uthibitisho wa vitendo kwamba matumaini ya Umoja wa Afrika siyo ndoto tu, kwani kama nchi mbili zinaweza kuungana na kuwa nchi moja, basi, nchi tatu pia zinaweza. Na kama nchi tatu zinaweza, basi hata nchi zote za Afrika pia, zinaweza." Ni bahati mbaya sana kwamba mawazo hayo yalibaki kuwa ni ndoto tu, kwani hata nchi tatu za Afrika Mashariki wakati huo, yaani, Tanzania, Kenya na Uganda, pia hazikuweza kuungana; na Umoja wa Afrika vilevile, umebakia kuwa ni ndoto tu, hadi hii leo.

Lakini, yale malengo yaliyobaki, yaani lengo la pili, la kuimarisha ulinzi wa nchi, pamoja na lengo la tatu, la kudumisha udugu na maelewano; kwa hakika hayo yamefanikiwa kwa kiwango kikubwa sana. Kwa mfano, suala kwamba, ulinzi wa nchi yetu uko imara kabisa, lilipata uthibitisho pale ambapo majeshi ya Uganda yalipotumwa na Rais wa nchi hiyo, Iddi Amin Dada, kuishambulia nchi yetu kwa upande wa mkoa wa Kagera, mnamo mwaka 1978; ambapo, kwa kuwa yalikuwa ni mashambulizi ya ghafla sana, wavamizi hao waliweza kufanya uharibifu mkubwa kwa muda mfupi, kabla ya majeshi yetu hayajafika huko kuwaonyesha wavamizi hao kile 'kilichomtoa nyoka pangoni.' Kwani siyo tu kwamba, wavamizi hao walifukuzwa mara moja kutoka katika ardhi yetu, bali pia majeshi yetu yalikwenda mpaka Kampala kumuadhibu ipasavyo Iddi Amin mwenyewe. Na hatimaye, ilivyotokea ni kwamba, adhabu yake ikawa siyo tu kwamba majeshi yake yalisambaratishwa kabisa ili yasithubutu tena kutuchokoza, bali, pia, hata yeye mwenyewe alilazimika kuikimbia nchi yake na kwenda kuishi uhamishoni huko Saudi Arabia, hadi mauti yalipomkuta.

***Mungu ibariki Tanzania.***

***Tunamwomba Mwenyezi Mungu aulinde Muungano wetu, uendelee kuwapo katika hali ya utulivu na usalama kwa miaka mingine mingi ijayo.***

# Afrika bado haijajipanga kuuingia mtangamano



Mwenyekiti wa sasa wa Umoja wa Afrika (AU) ambaye ni Rais wa Misri, Abdel-Fattah el-Sisi. **PICHA: MTANDAO**

**Na Gaudensia Mngumi**

TATHMINI ya kusaini, kuridhia na kuanza kutekeleza mkataba wa Umoja wa Afrika (AU) wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi Bora (ACDEG), iliyofanywa na asasi za kiraia za Kusini mwa Afrika, inaibua hoja na maswali yanayoashiria kuwa pengine Afrika inaendeleza ushirikiano, lakini haina nia ya kuwa na mtangamano.

Hali hiyo inaibuliwa na asasi za SADC hivi karibuni kwenye mkutano uliofanyika sambamba na ule wa 39 wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Ushirikiano wa Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) jijini Dar es Salaam.

NGO za SADC zinapokutana kuangalia hatua za utekelezaji wa mkataba huo ambao kwa mujibu wa AU, jumuiya za ushirikiano kama SADC au ECOWAS kwa Afrika Magharibi, ndizo nguzo za kutekeleza agenda, maazimio na mikataba ya AU katika kanda zao, zinaona udhaifu mwingi.

Akizungumzia uhalisia wa kutekeleza Mkataba wa African Charter on Democracy, Elections and Governance (ACDEG), ambao ndio unaoleta mtangamano, Meneja Miradi wa Mtandao wa Asasi za Kiraia za SADC -CNGOs Rangarirai Machemedze, anasema:

"Tangu mkataba huu ulipokubaliwa Januari mwaka 2007 na kuanza rasmi kutumika Februari 2012, hakuna taifa lililoutekeleza kikamilifu...hii ni ajabu kama kuna nia ya mtangamano hapo," anahoji Machemedze ambaye ni raia wa Zimbabwe.

Anasema wakuu wa AU walipokutana Addis Ababa, waliona mkataba huo ni muhimu na ndiyo njia pekee ya kuimarisha na kuendeleza demokrasia pamoja na uongozi bora, kudumisha haki za binadamu na za kijamii ndipo wakauidhinisha, lakini wote wameupa kisogo.

> "Maswali hayo ni pamoja na inachongoja Afrika kutekeleza mkataba huo uliokubaliwa na AU Addis Ababa miaka 12 iliyopita karibu miongo miwili sasa.

Anasema kinachoonekana hapo ni Afrika kuendelea na ushirikiano kama wa kibiashara, kiuchumi, kiulinzi lakini si mtangamano (integration), unaohusisha kuwa na sheria moja, viza na pasi moja, soko la aina moja na hata sarafu moja, ndiyo maana masuala ya utaifa na mamlaka za dola zinakuwa na nguvu kuliko maamuzi ya AU.

Anabainisha kwamba hakuna anayejali mikataba kama huo ambao una maono ya kuiunganisha Afrika.

"Mkataba huu hauzungumzii uchaguzi na uongozi bora pekee. Viongozi wa Afrika angalieni Ibara ya 27 inayozungumzia kuifanya Afrika iwe bora zaidi kisiasa, kiuchumi na jamii," anasema.

## KUSUSA MKATABA

Mambo makubwa yanayoonyesha kuwa Afrika inaogopa kivuli chake yanajengwa na maswali kadhaa anayoyaibua Machemedze:

"Maswali hayo ni pamoja na inachongoja Afrika kutekeleza mkataba huo uliokubaliwa na AU Addis Ababa miaka 12 iliyopita karibu miongo miwili sasa," anasema na kuongeza:

"Hadi sasa kuna mikakati gani imewekwa kuhakikisha mkataba unatangazwa, unafikishwa kwa wananchi na ACDEG inafahamika katika ngazi za taifa, kanda na bara zima na mengineyo mengi?"

## HALI HALISI

Kwa mujibu wa Idara ya Siasa ya AU hadi sasa mataifa 46 ya AU yaliyosaini mkataba huo (kuusaini inamaanisha kuukubali), kati ya hayo 34 yameuridhia na nchi moja pekee Jamhuri ya Togo, ndiyo iliyowasilisha makao makuu ya AU ripoti ya utekelezaji wa mkataba huo. Nyingine zote haziutekelezi.

Kwa upande wa SADC wanachama 14 wameusaini, Tanzania na Botswana hazijausaini wala kuuridhia mkataba huo, zimeuweka pembeni.

"Hata hivyo, mataifa mengine yaliyouridhia hayajaugusa wala hayautekelezi, hivyo hayana tofauti na Tanzania na Botswana," anasema Machemedze.

## CHIMBUKO ACDEG

Kuanza kutumiwa mkataba wa ACDEG si jambo geni kwani umo ndani ya mikataba na malengo makuu yanayounda Umoja wa Afrika (AU) kwenye Ibara ya 3 (g na h) pamoja na 4 (m), ambazo zinasisitiza umuhimu wa utawala bora.

"Lakini pia ushirikishwaji umma na utawala wa sheria unaozingatia Katiba na kuheshimu haki za raia, kupambana na rushwa na kutumia raslimali za umma kuleta maendeleo, anasema Meneja Miradi wa SADC- CNGOs," anasema Machemedze.

## NGUZO ZA ACDEG

Viongozi wanakumbushwa kuwa nguzo zilizounda mkataba huo zimetokana na maazimio na matamko yaliyofanywa na uliokuwa Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), ambao sasa ni Umoja wa Afrika (AU) ukihusisha mikataba kama ule Mkataba wa Afrika wa Haki za Binadamu wa mwaka1981.

Nyingine ni maamuzi ya mwaka 1999 ya Algiers, kukabiliana na mapinduzi kubadili serikali kinyume na Katiba.

Msingi mwingine ni Azimio la Lomme la mwaka 2000 la muundo wa OAU la kukabiliana na mabadiliko ya serikali yasiyozingatia katiba. Pia azimio la mwaka 2002 la OAU/AU la misingi na taratibu za uchaguzi wa kidemokrasia barani Afrika na mkataba wa kuundwa AU yenyewe.

ACDEG inazitaka nchi za Afrika ili kufikia azma ya umoja unaozaa matunda na mtangamano wa kweli hazina budi kila mwanachama miongoni mwa nchi 52 kuimarisha uwezo wa Bunge na mhimili wa sheria kusimamia haki, uongozi bora na kutunga sheria zinazolinda maslahi ya raia.

Aidha, mkataba huo unataka kuendeleza demokrasia na ushirikishwaji wa vyama vya upinzani, kufanya uchaguzi ulio huru na haki, na kuruhusu vyama vya siasa.

Pia unataka kuwapo uhuru wa mawazo na kufuatilia mwenendo wa serikali kusimamia haki, kuleta maendeleo ya umma na kuendeleza demokrasia na uongozi bora.

Eneo jingine ni ushirikishwaji na kushirikiana na vyama vya kiraia (NGOs), kwa kufanya marekebisho ya mara kwa mara ya sheria na mfumo wa Mahakama ili kuongeza utoaji na kusimamia haki za raia.

Vilevile kupambana na kutokomeza rushwa, kushirikiana na sekta binafsi, kutumia raslimali za umma kuleta maendeleo endelevu.

Aidha, kuwahakikishia raia uhuru wa maoni, kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano kuhabarishana, kutokomeza maradhi kama malaria, kifua kikuu (TB) Ukimwi na VVU na ebola.

## MKURUGENZI

Awali akifungua mkutano wa wajumbe wa SADC, NGO, Mkurugenzi wa Tanzania wa Shirika la ActionAid, Yaekob Metena, anasema inasikitisha kuwa mwitikio wa viongozi wa Afrika kutekeleza mkataba wa demokrasia, uchaguzi na uongozi bora ni mdogo.

"AU ilifikia maamuzi mwafaka ya kuanzisha muundo wa uongozi wa Afrika (Africa Governance Architecture -AGA), lakini wanachama wanaupuuza.

"Wanachama wa AU wengi wamesaini na kuuridhia, lakini utekelezaji hauridhishi," anasema mkuu wa shirika hilo linalofanya kazi na azaki kuhamasisha utekelezaji wa mkataba huo.

## MAONI YA WAJUMBE

NGO za SADC zikiwamo vyama vya wanasheria viliona kama AU na Jumuiya za Kikanda kama SADC na ECOWAS hazijawajibika vya kutosha kutimiza lengo la kuwa na mtangamano wala kukemea uvunjifu wa haki za binadamu, rushwa na kusimamia haki kupitia vyombo ilivyoviunda.

Mathalani, Afrika inaikataa Mahakama ya Kimataifa ya ICC au ya The Hague na imeunda Mahakama ya Afrika, lakini raia hawanufaiki kwa kuwa bara zima halijasaini mkataba wa ACDEG unaowezesha kutumia chombo hicho.

Afrika kunatokea mapinduzi na mateso ya raia kama vurumai zilizotokisa Sudan, Malawi na Lesotho hakuna anayekemea na kusimamia kidete, kisa heshima ya dola na utaifa (sovereignty) vina nguvu kuliko Umoja wa Afrika.

Marais wanachezea wanavyopenda Katiba ili watawale milele, lakini bado wanakuwa wenyeviti wa AU. Kuna wengine wanatokana na mapinduzi na Mahakama za AU ziko kimya. Wajumbe wakapendekeza kuwa ili ACDEG iridhiwe na kutekelezwa kikamilifu ni vyema maamuzi ya AU yakapewa nguvu kuliko 'sovereignty' au mamlaka ya dola na utaifa.

Ifike wakati suala la AU liwe juu, nchi zote 52 ziwe chini ya mamlaka moja na si kila mmoja kujiamulia anavyotaka, kwani huko ndiko kunakokwamisha mtangamano.



Rais John Magufuli (katikati mwenye suti nyeusi) akikata utepe kuzindua moja ya barabara nchini ili kuboresha usafiri. **PICHA: MTANDAO**

# CCM ni kiwanda chenye kutoa hazina ya viongozi bora nchini

## • Mjadala uwe ni kulipa kodi

**Na Reubeni Lumbagala**

UTENDAJI kazi uliotukuka wa Rais wa John Magufuli ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), unaonekana kuwakuna wengi.

Na ndiyo maana kuna baadhi ya Watanzania waliokuwa wamefikia hatua ya kutamani Katiba iangaliwe upya ili tu Rais Magufuli aendelee kuliongoza taifa hata baada ya kumalizika mihula yake miwili kwa mujibu wa Katiba ya nchi.

Ni jambo la jema kwamba nchi yetu imepata kiongozi mwenye nia, uthubutu, malengo na utashi wa kisiasa wa kuwaletea wananchi maendeleo na Taifa kwa ujumla.

Pamoja na matamanio hayo, ni vyema Watanzania wakaelewa nchi inaongozwa kwa mujibu wa Katiba na sheria ambapo hakuna aliye juu ya sheria kwa mujibu wa nguzo za utawala wa sheria na utawala bora.

Kimsingi, Rais Magufuli amekulia na kulelewa na CCM kabla ya kutwaa uongozi wa nchi na yote anayofanya ni katika kutekeleza Ilani ya Chama chake kilichompitisha kugombea na hatimaye kushinda nafasi hiyo ya juu nchini.

Hivyo, ni jambo la muhimu kwa wananchi kutambua kwamba CCM, chama ambacho kilimlea Rais Magufuli katika misingi bora ni taasisi ya mfano.

Ni Taasisi kubwa mfano wa kiwanda kinachozalisha bidhaa bora na nyingi.

Baadhi ya wanachama wa CCM na wananchi wengine wamekuwa na mtizamo wa kutamani kiongozi huyu atakapomaliza muda wake kwa mujibu wa katiba yetu mabadiliko yafanyike.

> Akipata ridhaa ya kuongoza kwa awamu ya pili mwakani, atapumzika baada ya muda wake kwani CCM wala serikali ya CCM haina nafasi ya kuwa na viongozi masultani.

Mabadiliko yafanyike kwenye Katiba ili kumruhusu Dk. Magufuli aendelee kuongoza nchi, mtizamo ambao yumkini si wa kikatiba na hasa ikizingatiwa kuwa Chama cha Mapinduzi pamoja na Rais Magufuli mwenyewe ni waumini wazuri wa kuheshimu katiba ya nchi.

Mara kadhaa, Rais Magufuli ameliongelea hili akibainisha kwamba anaheshimu katiba na hayupo tayari kuongeza muda wa uongozi kwani kufanya hivyo ni kukiuka Katiba aliyoapa kuilinda na kuitetea nguvu zake zote.

Pamoja na kuliongelea hili, wapo baadhi ya watu wanaendeleza mjadala huu pengine kwa hofu ya nani naweza akaziba pengo la kiongozi huu na hasa ikiangaliwa kazi nzuri aliyoifanya.

Kimsingi, hakuna haja ya Watanzania kuwa na hofu kwani CCM imejipambanua kuwa taasisi imara yenye wanachama wengi wa kuweza kuendeleza kazi nzuri zilizofanywa na Rais Magufuli.

Chama Cha Mapinduzi ni taasisi imara ambayo kwayo wanapatikana viongozi bora waliopikwa na kuandaliwa vyema kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Hivyo, Watanzania wawe na matumaini kuwa Rais Magufuli atakapomaliza muda wake, atapatikana wa kuyaendeleza mazuri yanayofanywa sasa na hata zaidi ya haya.

**KATIBU MKUU**

Katibu Mkuu wa CCM, Taifa Dk. Bashiru Ally akizungumza katika mkutano wa kuimarisha demokrasia kwenye ngazi ya mashina Jijini Dodoma, alisema Rais Magufuli akimaliza muda wake wa miaka 10 wa mihula miwili atapumzika.

"Akipata ridhaa ya kuongoza kwa awamu ya pili mwakani, atapumzika baada ya muda wake kwani CCM wala serikali ya CCM haina nafasi ya kuwa na viongozi masultani," anasema Dk. Bashiru na kuongeza:

"CCM ina hazina kubwa ya viongozi na wananchi wasiwe na hofu baada ya kuondoka Rais Magufuli katika uongozi kwani watapatikana viongozi bora wa kuendeleza nchi."

**KATIBU WA ITIKADI**

Naye Katibu wa Itikadi na Uenezi wa CCM, Humphrey Polepole, alinukuliwa hivi karibuni akilizungumzia hilo.

"Nimetumwa na Mwenyekiti wa chama hicho Dk. Magufuli nibainishwe kwamba hana mpango wa kuongeza muda wa kuongoza nchi hata dakika tano pindi muda wake utakapomalizika," alisema na kuongeza:

"Wale wanachama wenzangu ambao mnaendeleza huu mjadala wa kuongezwa muda wa uongozi, naomba muuache maana Mwenyekiti anasema anakwazwa."

Polepole anasisitiza kuwa Rais Magufuli anaheshimu Katiba na sheria za nchi, kwahiyo, muda wake ukimalizika ataondoka na kuwaachia wengine kuendeleza kijiti cha uongozi.

**MJADALA UWE KULIPA KODI**

Ni maoni ya mwandishi wa makala haya kwamba ili kumuunga mkono Dk Magufuli ni muhimu wananchi wajikite kuhakikisha wanajituma katika kufanya kazi kwa bidii kwani kazi ni msingi wa maendeleo.

Taifa lenye watu wasiopenda kufanya kazi, hata wakiwa na rais bora, nchi haiwezi kusonga mbele kimaendeleo.

Sambamba na hili, suala la kulipa kodi liwe agenda ya kitaifa kuhakikisha kila mwananchi mwenye sifa ya kulipa kodi anatimiza wajibu wake kwa maendeleo.

Utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimaendeleo inayosimamiwa na serikali ni matokeo ya wananchi kulipa kodi na usimamizi bora wa kodi hizo zinazokusanywa ili nchi iendelee kupata maendeleo endelevu.

Naamini, wananchi sasa hawataendeleza tena mjadala wa kuongeza muda wa urais kwa maana kuwa muda wake utakapomalizika atapumzika kama ilivyokuwa kwa watangulizi wake akina Mzee Ali Hassan Mwinyi, Mzee Benjamin Mkapa na Mzee Jakaya Kikwete. Tafakari.

***Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali iliyoko wilaya ya Kongwa mkoani Dodoma.***

***Anapatikana kwa namba: (+255) 764 666349***

# Rais Abbas afika ukingoni

## • Aapa milioni moja watakufa wakiingia Yerusalemu



Rais Mahmoud Abbas wa Palestina. **PICHA: MTANDAO**

**Na Ani Jozeni**

RAIS Mahmoud Abbas wa Palestina amefikia hatua ya mwisho katika kile kinachoitwa kutafuta amani Mashariki ya Kati na kuwashangaza baadhi ya mashabiki wake katika nchi za Magharibi wanaomdhania kuwa ni kiongozi wa siasa za 'wastani.'

Ameonyesha makucha yake hivi karibuni akihutubia hadhara ya watu takriban 8,000 karibu na Ramallah, akizungumza siyo kama tu kiongozi wa Palestina bali wa nchi za Kiarabu na hata dunia ya Kiislamu kwa jumla, kuhusu jukumu la kuitwa Yerusalemu kwani ni yao, Wapalestina.

Alisema wapiganaji milioni moja kutoka miongoni mwa Wapalestina, Waarabu, Waislamu na Wakristo wataenda kwa miguu kuingia Yerusalemu na ikibidi wateketee huko. Na hadhara ilishangilia.

Msimamo huo wa Rais Abbas umekuja baada ya utawala wa Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu wa Israel kuwazuia wabunge wawili wa Marekani, Rashida Tlaib na Ihlan Omar kuingia nchini Israel na kutembelea maeneo yanayokaliwa zaidi na Wapalestina.

Hatua hiyo ilichukuliwa baada ya Rais Donald Trump kumshinikiza Netanyahu kutoruhusu wabunge hao waingie kwa kuwa ni wapinzani wakubwa wa Israel, na Trump anaamini kuwa wanawachukia Wayahudi.

Mzozo kati ya wakinzani wa Israel nchini Marekani na utawala wa Trump umempa nguvu Rais Abbas, kuona ngome hiyo ya Israel sasa inaanguka.

> Vyombo vya habari vya Israel vilitaja makundi mawili ya Wapalestina ambao Marekani inapinga familia zao kulipwa kwa fedha zinazotokana na UNRWA au Umoja wa Ulaya, n.k.

Lipo eneo jingine lililomlazimisha Rais Abbas kuingia katika kuchoshwa na hali iliyopo na kuanza kutaka imalizike kwa Wapalestina kuingia Yerusalemu kwa mamia ya maelfu, hata milioni moja.

Nalo ni hatua ya utawala wa Trump kuondoa kwa sehemu kubwa michango ya Marekani kwa Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia wakimbizi wa Palestina (UNRWA).

Ni kutokana na kutolewa malipo kwa familia za wapiganaji wa Kipalestina wanaokufa hata katika mashambulio ya kigaidi kama ya kujitoa mhanga, na nchi za Ulaya kushindwa kujazia pengo linalotokana na Marekani kufuta sehemu kubwa ya michango yake.

Rais Abbas alisema kamwe hatakubali 'mashahid' waitwe magaidi, malipo yaondolewe.

Vyombo vya habari vya Israel vilitaja makundi mawili ya Wapalestina ambao Marekani inapinga familia zao kulipwa kwa fedha zinazotokana na UNRWA au Umoja wa Ulaya, n.k.

Nayo ni wanaokufa kwa kubeba mabomu kulipua maeneo yenye Wayahudi, au kufa wakijaribu kuua raia wa Kiyahudi au maofisa wa utawala wake unaokalia eneo la Ukingo wa Magharibi wa mto Jordan, na sasa Israel inatayarisha sheria maeneo yote Wayahudi wanapokaa kuwa sehemu ya Israel.

Rais Abbas alisema misaada kwa familia hizo itaendelea kupelekwa, kwani 'mashahid' ni hazina kuu ya Palestina ambayo inapita kitu kingine chochote kwa thamani yake kwa taifa hilo.

Katika hotuba hiyo, Rais Abbas alikwenda mbali zaidi na kusema kuwa watu wake hawawezi kuondolewa katika nchi yao, na kuwa 'kila jengo lililojengwa na wakaliaji wa Kiyahudi litateketezwa na kutupwa katika jalala la historia.'

Wachambuzi wa habari walijitahidi kuonyesha kuwa katika hotuba hiyo yako maeneo ambako Rais Abbas alikuwa anazungumzia kukaliwa na 'utawala wa Kizayuni' akilenga Ukingo wa Magharibi wa mto Jordan, na maeneo mengi tu ambako dhana ya 'kukaliwa' ilikuwa inahusu Israel yote, siyo eneo hilo peke yake. Ni mwelekeo wa fikra kwa upande Rais Abbas ambayo si ya kawaida.

Kwa mwelekeo huo ina maana kuwa hakuna tofauti ya sera kati ya Rais Abbas na utawala wa Hamas unaoshikilia eneo la Gaza, kuwa hakuna tena suala la kupatikana kwa suluhisho la nchi mbili kama jitihada za kidiplomasia za kuunga mkono Wapalestina zinavyotaka.

Ni kama hatua ya 'kujilipua' ambayo matokeo yake ni kuiwezesha Marekani kufaulu kisera. Inasema hakuna wa kuafikiana naye.

Kuna eneo jingine ambako Rais Abbas aligusia, akitoa hisia za kina za fikra ya harakati ya Palestina ambayo haiendani na kinachofahamika kihistoria, aliposema kuwa Wapalestina ndio Wakaanani wa kale na kuwa Wapalestina wamekaa katika eneo hilo kwa miaka 5000 (yaani kuanzia miaka 3000 kabla ya Kristo).

Kuna ubishi mwingi kuhusu suala hilo lakini kimsingi kabila la kale linalofanana na Wapalestina ni Wafilisti, ambao wanaonekana takriban miaka 2000 baada ya kipindi halisi cha Kaanani ya kale (enzi za Ibrahimu na Melchizedek, mfalme wa Salem ambayo Daudi, mfalme wa Israel, alijenga upya na kuipa jina la Yerusalemu).

Daudi alitawala miaka 1000 KK na ndiyo kipindi Waisrael wanapigana na Wafilisti.

Hakuna ubishi kuwa Wakaanani wa kale wanaendana na mataifa ya sasa yenye uhusiano wa karibu na Wabantu kwa upande mmoja na Wakushi kwa upande mwingine, kwani wakazi wa Salem hawakutajwa moja kwa moja lakini eneo la miji kenda ya Kaanani ya kale ilikuwa zaidi ya Waamori, ambao pamoja na Waamaleki (kundi lingine la kipindi cha Sauli na Daudi, wafalme wa Israel) wanaendana na Waafrika kwani walikuwa weusi.

Watalaamu nchi za Magharibi wanawaona Wapalestina kuwa wametokana na makundi ya waeneza dini na wapiganaji wengine tangu kuanzishwa kwa Uislamu.

Na hata kiutamaduni, au koo zinazotawala, hakuna tofauti kati ya Saudia na maeneo ya jirani kama Jordan, na hata Iraq kabla.

Msimamo huo wa Rais Abbas inaelekea utawafurahisha baadhi ya wakinzani wake na washirika wa Israel katika eneo la Ghuba ambao walishiriki kongamano la 'amani kwa njia ya uchumi' katika eneo la Mashariki ya Kati, ikiwa ni pamoja na Palestina.

Ni mtazamo wenye lengo la kufungua eneo hilo kwa uwekezaji mkubwa kwa kuweka pembeni mjadala wa kihistoria wa kuundwa kwa nchi mbili tofauti, ya Israel na ya Palestina, kwani tatizo tangu mwanzo ni kuwa sehemu isiyo ndogo ya Palestina inaamini kuwa eneo lote hilo ni lao, na Wayahudi ni wavamizi tu kutoka nchi za Magharibi.

Walikuwapo Wayahudi elfu kadhaa mwanzo wa karne iliyopita katika eneo la Palestina, ila ni kwa juhudi za kutaka kurudi nyumbani wakaongezeka baadaye.

Wakati huo huo, Rais Trump aliwasha moto kuhusu safari iliyofutwa ya wabunge wawili wanawake nchini Israel akisema katika mazungumzo na waandishi wa habari kweye viwanja vya Ikulu kuwa Wayahudi ambao ni raia wa Marekani wanaokipigia kura chama cha Democratic ni wajinga na wanaonyesha utovu wa utii kwa nchi ya Israel.

Rais Trump aliendelea na madai kuwa chama cha Democratic kwa jumla sasa kinaipinga Israel, na kuwa wanataka mambo mabaya kwa nchi hiyo kama kuondolewa kwa misaada kutoka nje. Rafiki bora wa Israel duniani ni Marekani.

Suala la kuondolewa kwa misaada ya Marekani kwa Israel lilitajwa na wabunge hao baada ya safari yao ya kwenda Israel kufutwa, hasa Ihlan Omar ambaye alitaka Marekani iangalie upya misaada inayotoa kwa Israel.

Vyombo vya habari vya Israel na makundi ya Wayahudi nchini Marekani, wanamuunga mkono Trump na hata kuanza kumtangaza kuwa ni mwokozi wa Israel, na kushindwa kwa nchi za Kiarabu kujazia pengo la misaada ya Marekani kutokana na eneo hilo kugubikwa na vita, ni changamoto kwa Rais Abbas kuhakikisha utawala wake unaleta neema kwa Wapalestina.

Ni nafasi nyingine kwa Iran kuvuta Wapalestina katika harakati kali zaidi sasa.





# Uzalishaji wa pareto bado 'kiduchu'

**Na Ashton Balaigwa**, MBEYA

LICHA ya Tanzania kuwa nchi ya kwanza duniani kwa uzalishaji wa pareto bora, bado kiwango cha uzalishaji kipo chini kutokana na upatikanaji wa mbegu bora.

Mtafiti Mkuu wa pareto kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) Uyole iliyopo mkoani Mbeya, Biles Nzilano, alisema juzi kuwa uzalishaji huo uko chini kutokana na wakulima kutumia mbegu za kizamani ambazo hazina tija.

Alisema kuwa kwa sasa Tanzania ni nchi ya pili duniani kwa uzalishaji wa pareto na uzalishaji wake kwa sasa umefikia tani 3,000 kwa miaka miwili mfululizo ikiongozwa na Tasmania ambayo ni ya kwanza.

Nzilano ambaye pia mratibu wa utafiti wa zao hilo, alisema ili kuongeza uzalishaji wa pareto nchini kunahitajika serikali kukiwezesha kituo hicho kuzalisha mbegu za teknolojia ya kisasa ili zisambazwe kwa wakulima.

Nzilano alisema zao hilo ambalo ni la biashara ni maalumu kwa ajili ya kutengeneza dawa mbalimbali zinazoua wadudu mashambani, ghalani, nyumbani na kwenye mifugo.

"Pareto limekuwa zao pekee linalotoa kiuatilifu ambacho ni rafiki wa mazingira na hakina madhara kwa mtumiaji," alisema.

Alisema nchini kote kwa sasa kuna wakulima 20,000 wanaohusika na uzalishaji wa pareto katika mikoa ya Mbeya (Wilaya ya Mbeya), Songwe (Ileje), Njombe na Ludewa na Iringa (Kilolo na Mufindi), Arusha (Arumeru), Manyara (Mbulu na Babati) na Kilimanjaro eneo la West Kilimanjaro.

"Asilimia kubwa ya pareto nchini inatoka Nyanda za Juu Kusini na sasa maeneo ya Kaskazini wakulima wanajitahidi," alisema.

Alisema uwezo wa kuzalisha pareto nchini ni mkubwa lakini umekuwa katika kiwango kidogo kutokana na upatikanaji wa mbegu bora ambao ni mdogo, hivyo kushauri nchi iangalie uwezeshaji kwenye utafiti ili wakulima wapate mbegu bora.

Zao la pareto lilitoka Australia na nchini Tanzania liliingia mwaka 1930 likitokea nchini Kenya.

Naye Mkurugenzi wa Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema kituo kwa sasa kina tani 2,250 za mbegu ya pareto na kwamba wanahamasisha viwanda kununua ili wakaushe kwa kuwa ekari moja inaweza kutoa kilo 840.

Alisema kituo hicho kimetafiti aina sita za mbegu ya mahindi, ulezi aina mbili, ngano aina tano, parachichi aina tano, soya aina nne, maharage aina 12 na mazao mengine.

## Utafiti wabaini chanzo cha uzalishaji hafifu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UTAFITI uliofanywa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari) Kituo cha Uyole, umebaini kuwa mikoa saba ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inakabiliwa na changamoto ya tindikali kwenye udongo hali inayoathiri uzalishaji wa mazao hususani ya chakula.

Hayo yalibainishwa jana na Mtaalamu wa Utafiti wa Udongo kutoka Tari- Uyole, Fredrick Mlowe, alipokuwa akizungumza na Nipashe juu ya matumizi sahihi ya ardhi kuelekea msimu wa kilimo.

Alisema utafiti huo umebaini kuwa mikoa yote saba ya Nyanda za Juu Kusini inakabiliwa na tatizo hilo hali inayosababisha wakulima wengi kuzalisha mazao yao bila kupima udongo.

Mlowe alisema kwenye utafiti huo, wamebaini uwapo wa tindikali nyingi kwenye udongo ambayo hairuhusu mazao hasa ya chakula kustawi na kutoa mavuno mengi.

"Maeneo mengi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yanakabiliwa na changamoto ya tindikali katika udongo hali inayosababisha wakulima kupata hasara ya mazao kukauka au mavuno duni, hivyo tumeamua kutoa elimu namna ya kukabiliana na hali hiyo," alisema Mlowe.

Aliongeza kuwa mimea mingi haistahimili kukua kwenye udongo wa tindikali isipokuwa zao la chai pekee na kwamba wanaendelea kuwaelimisha wakulima kupima udongo kupitia maabara zilizopo.

Mkurugenzi wa Kilimo kutoka Shirika la Kilimo Afrika (The Nature Conservancy), Felix Kamau, alisema wakulima wadogo nchini wanadhani uzalishaji duni wa mazao yao unatokana na wao kutotumia mbolea ipasavyo.

Alisema wanaamini msingi mkubwa wa kupata mavuno mengi ni matumizi ya mbolea dhana ambayo ni potofu wanasahau kuwa kilimo bora ni kile kinachozingatia pia matumizi sahihi ya udongo.

Mkurugenzi wa Tari-Uyole, Tulole Bucheyeki, kutokana na matokeo ya utafiti huo, aliwataka wakulima wa kanda hiyo kutumia kituo hicho kupima udongo ili kuzalisha kwa tija.



Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Hamis Juma (wa pili kushoto), akikagua ujenzi wa jengo la Mahakama ya Mwanzo Makete, wilayani Makete mkoani Njombe jana, akiwa katika ziara ya mikoa ya Njombe na Iringa. Wa nne kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Christopher Ole Sendeka. **PICHA: LYDIA CHURI**

## Ashauri kutoegemea misaada ya wafadhili

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KIONGOZI wa Kanisa la Efatha nchini, Josephat Mwingira, amewashauri viongozi wa serikali kuacha kutegemea misaada kutoka mataifa ya Ulaya badala yake wajitahidi kuboresha miundombinu ya uwekezaji kwenye madini, gesi na kilimo ili kujikwamua kiuchumi.

Mwingira alitoa kauli hiyo Jumapili iliyopita jijini hapa wakati akihubiri kwenye Kanisa la Efatha lililoko Forest.

Alisema Tanzania imebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi kama madini, na gesi ambazo zikisimamiwa vizuri zitasaidia kuondokana na utegemezi.

**Ni dhambi kubwa kuona taifa la Tanzania linaendelea kutegemea misaada kutoka mataifa ya Ulaya wakati tumebarikiwa kuwa na rasilimali kibao ambazo zinaweza kututoa kwenye wimbi la umaskini. Nashauri serikali kuongeza juhudi kwenye uwekezaji na kuboresha miundombinu ili tujitegemee**

"Ni dhambi kubwa kuona taifa la Tanzania linaendelea kutegemea misaada kutoka mataifa ya Ulaya wakati tumebarikiwa kuwa na rasilimali kibao ambazo zinaweza kututoa kwenye wimbi la umaskini. Nashauri serikali kuongeza juhudi kwenye uwekezaji na kuboresha miundombinu ili tujitegemee," alisema Mwingira.

Alisema si jukumu la serikali pekee kuhakikisha taifa linaondokana na utegemezi kutoka kwenye mataifa ya Ulaya badala yake taasisi zikiwamo za kidini kuwahubiria waumini kuchapa kazi kwa bidii, ili kuondokana na umaskini badala ya kushinda kwenye nyumba za ibada.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ambaye alishiriki ibada hiyo, alimpongeza Mwingira kwa kuishauri serikali mambo ya kufanya ili kuleta maendeleo tofauti na wengine ambao wamekuwa wakiikosoa bila kutoa suluhu ya nini kifanyike.

Alisema anawachukia wananchi wanaobeza kila jambo la maendeleo linalofanywa na serikali badala yake watumie fursa hizo kuanzisha miradi ambayo inaunga mkono juhudi zinazofanywa na viongozi.





# Agizo watumishi kuacha ubaguzi watumiaji CHF

**Na Paul Mabeja,** CHAMWINO

NAIBU Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Dk. Doroth Gwajima, amewataka watumishi wa afya kuacha kufanya ubaguzi kwa wateja wanaotumia kadi za bima ya afya ya jamii (CHF) iliyoboreshwa kwa kutoa kipaumbele kwa kuwahudumia watu wenye fedha mkononi.

Dk. Gwajima aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na watumishi wa Kituo cha Afya cha Chamwino Ikulu alipofanya ziara ya kukagua utoaji huduma za afya kwa wateja wenye kadi za CHF iliyoboreshwa.

Alisema watumishi wa afya wanatakiwa kuwapa kipaumbele wagonjwa wanaotumia kadi hizo ili kuongeza idadi ya watu wanaotumia mfumo huo nchini.

Dk. Gwajima alisema matumizi ya kadi za bima ya afya ya jamii iliyoboreshwa pamoja na ule wa NHIF, unahitajika kuendelea kufanyiwa uhamasishaji ili watu wajiunge ili kupata matibabu wakati ambao wanakuwa hawana fedha mkononi.

Alisema hivi sasa CHF iliyoboreshwa imefanyiwa marekebisho makubwa na serikali hali ambayo inamwezesha mgonjwa kupata huduma katika hospitali yoyote hadi ngazi ya mkoa.

"Awali kadi hizi zilikuwa zinamwezesha mtu kupata huduma katika eneo lake tuu, lakini sisi kama serikali tukaona kuwa ipo haja ya kufanya maboresho hivyo sasa kupitia kadi yako hii unaweza kupata huduma katika eneo lolote nchini kuanzia ngazi ya zahanati hadi hospitali ya mkoa," alisema.

Aidha, aliwataka watumishi wa afya nchini kutoa huduma zenye ubora ili kuwavutia wananchi kujiunga na mifumo hiyo ya bima.

"Kama tusipotoa huduma bora hivi vituo vyetu tulivyojenga nchi nzima vitakuwa havina maana, lazima sisi kama watumishi wa afya tubadilike ili kuwavutia wananchi kuja katika vituo vyetu kupata huduma," alisema Dk. Gwajima.

Pia Dk. Gwajima alitoa wiki mbili kwa waganga wakuu wa mikoa kuhakikisha kuwa wanazifanyia kazi changamoto zote zilizopo katika mifumo ya utoaji wa huduma za bima afya ya jamii.

"Sitaki kusikia baada ya siku hizi 14 kuwa kuna kituo kimeshindwa kutuma taarifa zake au mifumo inakataa kwani kila kituo kinatakiwa kutuma taarifa zake za wateja waliohudumiwa ili kuweza kurejeshewa fedha zake ambazo zitatumika katika mahitaji mbalimbali ya eneo hilo," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya Chamwino, Dk. Zipora Mfugale, alisema wamejipanga kuhakikisha wanaongeza idadi ya wagonjwa wanaotumia mfumo wa CHF iliyoboreshwa.



Mariagorete Charles kutoka mradi wa bomba la mafuta ghafi (EACOP) kutoka Hoima nchini Uganda hadi Tanga, akitoa taarifa ya mradi huo, kwa viongozi wa Mkoa wa Dodoma jana, walipokutana kwa ajili ya kuelezea maendeleo yake. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**.

# Wenye ulemavu sasa kufuatwa kila nyumba kupelekwa shule

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeweka mikakati ya kupita nyumba hadi nyumba kwa ajili ya kuwatambua watoto wenye ulemavu ili waweze kupelekwa shule kwa ajili ya kupata elimu kama ilivyo jamii nyingine.

Aidha, serikali imesisitiza miundombinu ya zamani na ile mipya inayojengwa iboreshwe ili iwawezeshe watu wenye mahitaji maalumu kufika sehemu husika.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi Msaidizi kutoka Wizara ya Tamisemi anayeshughulikia elimu ya msingi, Dk. George Jidamva, katika ufunguzi wa mkutano wa nchi mbalimbali zinazotekeleza mradi wa elimu jumuishi chini ya Taasisi ya Leonard Cheshire.

Wadau walioshiriki ni kutoka Kenya Uganda, Zambia, India, Afrika Kusini na wenyeji Tanzania.

Alisema timu hiyo itajumuisha wataalamu ambao watapita kuwatambua watoto wenye ulemavu ili wale wenye umri wa kwenda shule waandikishwe.

"Timu yetu ya wataalamu inapita kila mwaka lengo ni kuwatambua watu wenye uhitaji maalumu na kuwapeleka shule wale waliofikia umri unaostahili," alisema Dk. Jidamva.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka watoto hao waweze kupata elimu jumuishi pamoja na jamii nyingine katika sehemu moja.

"Hivi sasa tunataka kuondoa hiyo ya kusema shule za uhitaji maalumu ndio maana tumekutana katika mkutano huu," alisema Dk. Jidamva.

Alisema wenyeji Tanzania wanapaswa kuuzingatia yanayojadiliwa ili kupata uzoefu kwa nchi ambazo tayari zinatekeleza mpango huo wa elimu jumuishi.

"Naomba zingatieni kile mnachojadili katika semina hii, tunahitaji kupata uzoefu toka kwa wenzetu ambao tayari wanatekeleza mpango huo," alisema Dk. Jidamva.

Kuhusu suala la miundombinu, alisema ni lazima majengo mapya na yale ya zamani yaboreshwe ili kuwawezesha watu wenye uhitaji maalumu kufika katika eneo husika kupitia usafiri au kifaa chochote ambacho anacho kwa ajili ya kusaidia kufika eneo husika.

"Miundombinu mipya katika ujenzi ni lazima iboreshwe kwa sababu tunahitaji watu hawa wapate elimu jumuishi," alisema.

Meneja Mradi wa Elimu Jumuishi mkoani Dodoma, Menance Mhombe, alisema lengo lao ni kuona watoto wenye uhitaji maalumu wanapata elimu jumuishi pamoja na wenzao jambo ambalo linawasaidia kujua vitu vingi wakiwa darasani.

Alisema kwa Dodoma mradi huo unatekelezwa katika wilaya za Chamwino na Dodoma, ambapo jumla ya shule 20 kutoka wilaya hizo zipo chini ya mradi huo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Tanzania Cheshire Foundation (TCF), Steven Masangia, aliushukuru mkutano huo kufanyika nchini, na anaamini utaleta matokeo mazuri kwa jamii inayotuzunguka.

# Mbinu kuwainua wafanyabiashara wadogo wadogo

**Na Ibrahim Joseph Joseph,**

DODOMA

IMEELEZWA kuwa wafanyabiashara wadogo wanahitaji kupewa mafunzo ili kuondokana na changamoto ya namna ya kukuza mitaji yao na kufikia hatua ya kuwa wafanyabiashara wa kati.

Hayo yalielezwa na Dk. Wambuka Rangi kutoka Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT) alipokuwa akiwasilisha taarifa ya utafiti kwenye warsha ya tathmini kuhusu hali halisi na mazingira ya wafanyabiashara wadogo mkoani hapa mwisho wa wiki jijini hapa.

Dk. Rangi alisema wafanyabiashara hao wanahitaji kupewa mafunzo ya namna ya kuwasaidia ili waweze kupata mitaji, wakue na kufikia wafanyabiashara wa kati.

Alisema utafiti huo ulishirikisha jumla ya watu 446, na timu ya watafiti wawili wa OUT kwa niaba ya Shirika la Tanganyika Christian Refugee Service (TCRS).

Alisema katika utafiti huo wametambua kuwa kundi hilo la wafanyabiashara ndogo ni watu muhimu wanaotoa huduma kwa jamii.

Dk. Rangi alisema utafiti huo ulifanyika katika kata tisa jijini Dodoma kwa kuangalia mazingira wanayofanyia biashara na changamoto wanazokutana nazo na kutoa mapendekezo ya nini kifanyike.

Kata hizo ni Nzuguni, Uhuru, Madukani, Viwandani, Kizota, Chang'ombe, Tambuka Reli na Majengo.

Aliyataja mapendekezo ya watafiti hao ni elimu itolewe kwa wafanyabiashara kuhusu haki zao kama mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za kifedha pamoja na kuelimishwa kuhusu sera na sheria za jiji.

Mkurungenzi wa Mradi wa TCRS Mkoa wa Morogoro, Rehema Samwel, alisema shirika hilo linafanya kazi katika maeneo ya Kishapu, Ngara, Kibondo, Kakonko, Kilwa, Morogoro na Dar es Salaam.

Samwel alisema awali shirika hilo lilikuwa likifanyakazi ya kuhudumia wakimbizi katika maeneo mbalimbali nchini, lakini baada ya kubaini changamoto katika jamii waliona wasaidie katika kuinua uchumi.

Aliongeza kuwa TCRS, inaendelea kuunga mkono juhudi za serikali katika kuwahudumia wananchi, lakini wao wamejikita zaidi katika utafiti kwa wafanyabiashara wadogo katika mikoa michache.

Alibainisha kuwa shirika hilo kwa kushirikiana na Chuo cha Biashara (CBE) mwaka 2017 walifanya utafiti katika Manispaa ya Morogoro na mwaka 2018 walifanya utafiti huo Mkoa wa Dar es Salaam na mwaka huu ulifanyika Jiji la Dodoma.



# Paka kutumika kudhibiti panya waharibifu mananasi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKULIMA wa mananasi katika Kijiji cha Donge Mkoa wa Kaskazini Unguja, wamelazimika kufuga paka katika mashamba kwa ajili ya kulinda mazao yao.

Wakizungumza na Nipashe wakulima hao walisema, wameamua kufanya uamuzi huo kutokana na mazao yao kushambuliwa na wadudu waharibifu aina ya panya.

Salum Taimur Ali ni miongoni mwa wakulima wa kijiji hicho, alisema kuna panya wengi katika mashamba yao ambao wamekuwa wakiyashambulia mananasi yakiwa machanga.

"Tumeamua tufuge paka mashambani ili kuwadhibiti hawa panya maana wamekuwa wakitutia hasara," alisema.

Mkulima Nyange Zuheri Makame, alisema zaidi ya hekari 20 za mananasi zimeharibika kutokana na kuvamiwa na panya na kusababisha hasara kwa wakulima wa bonde la kichanga.

Alisema licha ya kuweka dawa mbalimbali kwa ajili ya kuwaua wadudu hao, bado dawa hizo hazijasaidia.

Naye Msaidizi Mkurugenzi Sekta ya Kilimo Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini B, Suleiman Khamis Suleiman, alisema watahakikisha wanawasaidia wakulima hao ili kuwatatulia changamoto zinazowakabili ikiwamo uwepo wa panya katika mashamba yao.

Alisema zaidi ya asilimia 80 ya wananchi wa wilaya hiyo hutegemea kilimo kwa ajili ya kujikimu kiuchumi na kuondokana na hali ya umaskini.

"Wakulima wa wilaya hii wamekuwa wakifanya vizuri katika kilimo, hivyo si vyema kuwatupa mkono lazima tuwe nao bega kwa bega ili kunufaika na kilimo," alisema.

Kwa upande wake ofisa utibabu wa mimea Wilaya ya Kaskazini B, Khamis Muhammed Khamis, aliwaomba wakulima kuwa na subira kwa kuwa tayari wameanza kulifanyia utafiti suala hilo la uwepo wa panya katika mashamba yao.



Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha St. Joseph, David Philip Gunda, ambaye ametengeneza mashine ya kuchakata samaki akitoa maelezo jinsi inavyotumika akiwa katika maonyesho ya teknolojia ya sayansi, katika viwanja vya Kumbukumbu Michezani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Wafanyabiashara watakiwa kuondoka eneo la shule

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

NAIBU Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amewataka wafanyabiashara wa pembezoni mwa Shule ya Sekondari Vikokotoni kuondoka mara moja katika eneo hilo, ili wanafunzi wasome kwa utulivu.

Akizungumza wakati alipofanya ziara ya kushtukiza na kuwaondoa wafanyabiashara hao pembezoni mwa ukuta wa shule hiyo, alisema Wizara ya Elimu Zanzibar, haitosita kumchukulia hatua za kisheria mfanyabiashara yeyote atakayekiuka agizo hilo.

Alisema kutafuta elimu ni jambo la muhimu na linahitahiji utulivu wa hali ya juu, hivyo wataendelea kuhakikisha wanafunzi wa shule hiyo wanasoma kwa amani na utulivu.

Aliwataka wanafunzi wa shule hiyo kujitahidi katika masomo yao kwa kuwa tatizo la kelele za wafanyabiashara limeshatatuliwa.

Naye Msaidizi wa Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Mwana Ali Omar, alisema amefurahishwa na hatua ya Naibu Waziri huyo kwa kuwa watoto walikuwa hawasomi kwa utulivu madarasani.

Kwa upande wao wanafunzi wamemshukuru Naibu Waziri na kuahidi kuwa watasoma kwa bidii ili wafaulu vizuri katika mitihani yao ya taifa.

# Vijana wahamasishwa kusoma masomo ya Sayansi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KAIMU Makamu Mkuu wa Chuo cha St. Joseph University Tanzania, Professa Inosent Ngalinda, amesema ili Tanzania iweze kuwa na uchumi wa viwanda lazima vijana wasome Sayansi.

Alitoa rai hiyo wakati akifunga maonyesho ya teknolojia ya sayansi kwa wanafunzi wa shule za sekondari yaliyoandaliwa na Chuo Kikuu cha St. Joseph.

Alisema bila ya sayansi nchi haiwezi kuendelea na ndio maana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, anaiendesha nchi kisayansi kwa sababu yeye ni mwanasayansi.

Aliwataka Watanzania kuangalia mambo ya msingi na kuacha kujikita katika siasa.

Alisema mwanasayansi anaweza kujiajiri bila kutegemea kuajiriwa.

Aliwataka wazazi kuwakazania watoto wao kusoma sayansi kwa sababu masomo hayo yana manufaa zaidi.

Naye Deved Philip Gunda, ambaye ametengeneza mashine ya kuchakata samaki, alisema ameamua kubuni mashine hiyo baada ya kuona kuwa wachuuzi wanavyopata tabu katika kusafisha bidhaa hiyo.

"Mashine hii inasafisha samaki kwa kutoa magamba na utumbo hivyo itasaidia sana kuondoa adha ya kuandaa kitoweo hasa kinamama wamekuwa wakijikata mikono kutokana na kutengeneza samaki," alisema.

Alisema amebuni mashine hiyo tokea Februari mwaka jana na kukamilisha mwezi huu wa Agosti ambayo itasaidia kutengeneza samaki katika mazingira mazuri.

Aliiomba serikali kuwabaini vijana wabunifu na kuwawezesha ili kuboresha mifumo ya viwanda.

Akifunga mafunzo hayo Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslih Hija, aliwaasa wanafunzi kupenda masomo ya sayansi kwa kuwa yatasaidia kufikia azma ya serikali ya nchi ya viwanda.

Akisoma hotuba yake wakati wa kufunga maonyesho hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali (ufundi) Zanzibar, Bakari Ali Silima, alisema, masomo hayo ni muhimu kwa kuwa ndio yatayoipeleka nchi katika viwanda ambayo ni sera ya serikali zote mbili.

Alisema, chuo hicho na wanafunzi wengine wana nafasi kubwa ya kuendelea kuihamasisha jamii kujiunga na masomo hayo ambayo ndio changamoto kubwa kwa vijana wa Zanzibar kuyakwepa masomo hayo.

"Ni imani yangu kwamba maonyesho haya yameleta hamasa kubwa kwa vijana wetu waliokuwapo sekondari kujifunza masomo ya sayansi hasa kwa vijana wetu wa kizanzibari," alisema.

Hata hivyo, alisema kazi za ubunifu zilizobuniwa na wanafunzi wa Chuo cha St. Joseph Tanzania zinaonyesha dhahiri kuwa zinaweza kutatua matatizo yanayoikabili jamii katika sekta mbalimbali ikiwamo viwanda, kilimo, ujenzi, afya na mawasiliano.

Katika maonyesho hayo wanafunzi walipewa zawadi kwa kubuni teknolojia na mshindi wa kwanza ni Shule ya Wasichana Benbella.

# Waomba msaada wa JPM mgogoro wa ardhi

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WANANCHI wa Vilima Vitatu wilayani Babati mkoani Manyara, wanamwomba Rais John Magufuli kutembelea kijiji chao, ili kutatua mgogoro unaoendelea baada ya kuchomewa maboma 32 Julai 8 hadi 10, mwaka huu na kusababisha kaya 248 kukosa mahali pa kulala hadi sasa.

Akisoma jana tamko la wananchi hao jijini Arusha, Mwenyekiti wa Wafugaji Kata ya Ngaiti, wilayani humo, Juma Kwanjai, alisema baada ya kuchomewa maboma hayo Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, alitembelea kijijini hapo Julai 29, mwaka huu na kuagiza kupitia mkutano wa hadhara kuwa wafugaji na wavuvi wasiondolewe.

Kwanjai alisema katika mkutano huo Waziri Mpina alisema Rais Magufuli Januari 15, mwaka huu, aliagiza wananchi wote ambao ni wafugaji, wavuvi na wakulima wanaoishi maeneo ya migogoro wasihamishwe hadi uchunguzi ukamilike.

"Lakini pamoja na agizo hilo bado tumepewa barua mwezi huu tunatakiwa kuhama eneo hili tukiambiwa ni hifadhi, sisi tunateseka kama sio Watanzania, tunamwomba Rais asitume mtu aje mwenyewe kutusikiliza," alisema.

Alisema licha ya Waziri Mpina, pia Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, akiwa ziarani mkoani Simiyu aliagiza kusitishwa operesheni ya kuwaondoa wananchi wa eneo hilo akisema ni raia wasio na hatia.

Kwanjai alisema licha ya maagizo hayo, iko Mahakama ya Rufani Tanzania katika rufani ya madai namba 16 ya mwaka 2013 iliyowapa ushindi dhidi ya kijiji cha Vilima Vitatu na Jumuiya ya Wanyama Pori Burunge (JUHIBU) na iliamuru wananchi hao wasiondolewe kwani eneo hilo ni la malisho.

Hata hivyo, alisema pamoja na maagizo ya viongozi hao na mahakama, lakini bado Agosti 22, mwaka huu, walipokea barua ya Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Vilima Vitatu, Husna Shabani, ikiwaamuru wahame kutoka ardhi hiyo ya malisho kwa sababu ni hifadhi.

Kwa mujibu wa barua hiyo ambayo Nipashe imeiona, inasema: "Mada hapo juu yahusika kutokana na maazimio ya kikao cha Mh. Mkuu wa Mkoa cha tarehe 22/8/2019 maazimio ni kuondoka eneo la hifadhi baada ya siku tatu yaani tarehe 26/8/2019."

Sehemu ya barua hiyo iliyosainiwa na Husna iliendelea kusema: "Hivyo unatakiwa kuondoka eneo hilo mara tu upatapo barua hii na kuhamia maeneo yaliyotengwa yaani mfugo ya ng'ombe."

Mmoja wa wakazi wa eneo hilo, Dorcas Bayai, alisema, wanamwomba Rais awanusuru na mateso wanayopata tangu mwaka 2013 hadi mwaka huu, kwa kuwa wamekuwa watu wa kuchomewa nyumba zao na kuishi kwa mateso makubwa bila amani.

Gidajuri Gwaidanyi, alisema, wanamwomba Rais Magufuli atembelee kijiji hicho yeye mwenyewe akatatue mgogoro huo, kwani wananyanyasika, na sasa wanaishi bila makazi na mifugo yao inaliwa na wanyama kwa kukosa pa kuwahifadhi.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akisalimiana na Mkuu wa Idara ya Biashara za Serikali kutoka Benki ya NMB, Vicky Bishubo, alipotembelea maonyesho ya bidhaa mbalimbali katika kilele cha sherehe ya Siku ya Wakizimkazi inayofanyika kila mwaka katika kijiji cha Kizimkazi Mkoa wa Kusini Unguja juzi. NMB ni mdhamini wa maadhimisho ya siku hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wajawazito watembea kilometa 17 kwa matibabu

**Na Neema Sawaka,** TABORA

WAJAWAZITO na wagonjwa katika Kijiji cha King'wangoko Kata ya Konanne, Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora, wanatembea kilometa 17 kufuata huduma za matibabu.

Hayo yalibainika kwenye harambee ya kuchangia ukamilishaji wa jengo la zahanati na ujenzi wa nyumba ya Mganga iliyofanyika katika kijiji hicho.

Monica Nsima, alisema wajawazito hulazimika kutembea umbali wa kilometa 17 kufuata huduma ya kujifungua hali inayosababisha mama ama mtoto kupoteza maisha.

Alifafanua kuwa huduma za wagonjwa na wajawazito wanaokwenda kujifungua hulazimika kutembea umbali huo hadi katika zahanati za Yasasu au Seleli zilizopo katika vijiji hivyo vya jirani vya Yasasu na Seleli.

Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha King'wangoko, Mashindeke Lumwambe, alisema tangu kupatikana kwa Uhuru wamekabiliwa na changamoto za matibabu na hali huwa mbaya zaidi kipindi cha masika ambapo miundombinu ya barabara huathiriwa na mvua.

Ofisa Mtendaji Kata ya Konanne, Raphael Mwamlima, akisoma taarifa ya ujenzi, alisema ulianza mwaka 2013 kwa wananchi kuchangia Sh. milioni 17, ambazo zimewezesha kujenga jengo la zahanati hadi kulipaua, hivyo kuhitajika kiasi cha Sh. milioni 21 ili kukamilisha ujenzi wa zahanati.

Aidha, alisema kwa upande wa nyumba ya mganga, kunahitajika Sh. milioni 34, hivyo kuongeza wigo la ukamilishaji wake ambao jumla yake utatumia wa gharama ya Sh. milioni 54.9.

Dunia Francis, Mwenyekiti wa Kamati ya harambee, alisema kukamilika kwa zahanati hiyo kutasaidia wakazi 9,805 wa Kata ya Konanne, ambayo tangu kuanzishwa kwake inakabiliwa na changamoto za ukosefu wa huduma za afya.

Mgeni rasmi katika harambee hiyo, Hamisi Mhoja Bundala, Mkurugenzi wa Kampuni ya Hai JM ya jijini Dar es Salaam, alisema suala la kuchangia maendeleo ni la jamii nzima na kuacha kuingiza tofauti za siasa kwa kuacha kutegemea serikali pekee pasipo jamii kuweka nguvu zake.

Jumla ya mifuko 198 ya saruji, mawe tripu 20, misumari kilo 50 na Sh. 4,077,000 ambapo miongoni mwa fedha hizo mgeni rasmi alichangia Sh. 750,000 na saruji mifuko 50.

# Wananchi watakiwa kufuatilia fedha za serikali

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WANANCHI wilayani Nkasi mkoani Rukwa wameshauriwa kuwa na tabia ya kufuatilia fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya afya ili kuhakikisha fedha hizo zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Wito huo ulitolewa jana Divason Abel, Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Life Change Rukwa Development Organization (LCRDO) wakati wa uzinduzi wa mradi wa miezi nane uliofanyika katika kata tatu, vijiji tisa vya wilaya hiyo.

Alisema taasisi hiyo imebaini kuwa jamii inahitaji kujengewa uwezo katika kufuatilia matumizi ya fedha za umma (PETS) katika sekta ya afya kwani hivi sasa serikali inatoa fedha nyingi katika idara hiyo, hivyo ni vema sasa jamii ikahakikisha inafuatilia matumizi ya fedha hizo ili iweze kunufaika nazo.

Naye mlezi wa taasisi hiyo, Ozem Chapita, alisema kuwa katika bajeti ya serikali ya mwaka 2018/2019, serikali kuu ilitoa fedha nyingi kwa lengo la kuboresha huduma za afya ili kuondoa kilio kikubwa cha wananchi katika huduma za afya, hivyo ni muhimu pia kufuatilia kama kweli fedha hizo zinawanufaisha.

Alisema kuna changamoto kubwa kwa kamati za afya za kata na vijiji katika kushiriki mchakato wa mambo yanavyoendelea katika maeneo yao kiasi kwamba hata baadhi ya miradi inayotekelezwa pamoja na kufahamu dawa zilivyofika katika vituo vya kutolea huduma na namna yanayotumika kutokana na kutoshirikishwa na wao wamekuwa wakiona ni sawa.

Mmoja wa washiriki kutoka katika kijiji cha Majengo wilayani Nkasi, Richard Maganga, alisema walikuwa hawajui kama wanawajibika kufahamu kuhusu fedha hizo zinazotolewa na serikali kwani walijua hilo ni jukumu la watendaji wa serikali pekee.

Alisema wamekuwa wakiona zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya zikijengwa wilayani humo pamoja na maeneo mengine, lakini hawakufahamu kama wana wajibu wa kufahamu kinachoendelea zaidi ya kufurahia kuona serikali inatekeleza miradi hiyo ambayo inatekelezwa kwa kodi zao.

Mkurugenzi Mtendaji wa wilaya hiyo, Misana Kwangula, alisema imekuwa ni jambo la kushukuru kuona taasisi hiyo imeamua kuwajengea uwezo wananchi katika halmashauri hiyo kwani daima miradi mingi imekuwa ikitekelezwa mijini na kuwaacha wananchi wa vijijini wakiwa hawana uwelewa na pengine kubaki na malalamiko.

## HABARI KIMATAIFA

# Kenya yaanza kusafirisha mafuta ghafi

**NAIROBI,** Kenya

KWA mara ya kwanza Kenya imeanza kusafirisha mafuta ghafi kwenda nchini Malaysia.

Kiasi cha mapipa 200,000 ya mafuta ghafi yameanza kusafirishwa kwa meli jana kutoka bandari ya Mombasa.

Akiongoza hafla ya kuanza kwa safari za meli kupeleka mafuta hayo katika soko la Kimataifa, Rais Uhuru Kenyatta alisema mafanikio hayo ni ya kihistoria kwa watu wa Kenya tangu taifa hilo lilipoanza harakati za kutafuta mafuta na gesi mwaka 1937.

Rais Kenyatta alieleza kwamba biashara ya mafuta ni mwanzo mpya kwa Kenya na Afrika ya Mashariki.

Vile vile, alieleza kuwa kwa sasa mabadiliko yaliyofanyika katika sekta ya usafiri wa majini kupitia kampuni ya Mediterenia, Kenya itaweza kufanya biashara na bandari zaidi ya 500 duniani.

Rais Kenyatta alisema kuanza kusafirishwa kwa mafuta hayo ghafi kama majaribio katika soko la kimataifa ni jambo linalotia moyo na kuhakikisha kwamba taifa la Kenya litaweza kutimiza azma yake ya kuwa taifa lililo na rasilimali ya mafuta na gesi.

Mafuta hayo ghafi yanayochimbwa katika eneo la Lokichar Jimbo la Turkana, yamekuwa yakivunwa tangu mwaka jana na kusafirishwa kwa malori hadi bandarini Mombasa.

Rais Uhuru (pichani chini) alisema kuwa serikali yake imeweka mikakati ya kuhakikisha Wakenya wote wanafaidika kutokana na pato la mafuta hayo.

Katika hafla hiyo gavana wa Mombasa, Hassan Ali Joho alimtaka Rais Kenyatta kufufua kiwanda cha kusafisha mafuta ghafi kilichoko katika eneo la Changamwe karibu na bandari ya Mombasa kilichofungwa miaka mingi.

Vile vile aliitaka serikali kuwekeza zaidi kwenye viwanda mjini Mombasa ili mafuta hayo yaweze kutumiwa kutengeneza bidhaa mbali mbali zitakazouzwa nchi za nje pamoja na mafuta yaliosafishwa.

Kampuni ya Tullow iligundua uwapo wa mafuta katika ardhi ya Lokichar kaunti ya Turkana mwaka 2012. **DW**



# Uganda yapata kibali kusafirisha bangi Ulaya

**KAMPALA,** Uganda

WAKAGUZI kutoka Umoja wa Ulaya (EU) wameidhinisha Uganda kusafirisha bidhaa za bangi barani Ulaya.

Bangi hiyo itakayotumwa kwenye soko la Ulaya hata hivyo si kwa matumizi ya starehe kama uvutaji bali ni kwa ajili ya matibabu.

Kwa mujibu wa gazeti la Daily Monitor, wakaguzi wa bidhaa za matibabu zitokanazo na bangi kutoka Uholanzi walikagua mashamba ya bangi kwenye wilaya za Hima na Kasese nchini Uganda kati ya Julai 29 na Agosti 4.

Maofisa hao kabla ya kuondoka Uganda waliikabidhi cheti cha kukidhi vigezo kampuni ya Industrial Globus Uganda Ltd waweze kusafirisha bangi kwa kipindi cha Agosti 6, mwaka huu hadi Agosti 5, 2020.

**Baada ya EU kuthibitisha bidhaa zetu usafirishwaji na mnyororo wote wa uzalishaji kuanzia kupanda mpaka kuvuna na kwa bangi utafanyika kikamilifu nchini Uganda na kupelekwa kwenye masoko ya Ulaya.**

Mkurugenzi wa kampuni hiyo, Benjamin Cadet amelithibitishia gazeti hilo kuwa EU wamewapa idhini ya kusafirisha bangi Ulaya.

"Baada ya EU kuthibitisha bidhaa zetu usafirishwaji na mnyororo wote wa uzalishaji kuanzia kupanda mpaka kuvuna kwa bangi utafanyika kikamilifu nchini Uganda na kupelekwa kwenye masoko ya Ulaya," alisema Cadet.

Takribani kampuni 50 zimeomba kibali Wizara ya Afya kuungana na kampuni ya Industrial Globus Uganda Ltd ili kuzalisha bangi kwa ajili ya matibabu.

Bangi inayozalishwa Uganda katika shamba la wilayani Kasese ina virutubisho vya Cannabinol (CBD) na Tetrahydrocannabinol (THC) ujazo wa 2.7mg THC na 2.5mg CBD. Virutubisho hivyo vimethibitishwa Ulaya, Marekani na Canada.

Uganda ilishindwa kusafirisha bangi ya thamani ya dola milioni kwenda Canada na Ujerumani Julai mwaka huu baada ya kampuni ya Industrial Globus Uganda Ltd kutokuwa na cheti kutoka EU.

Uganda ndio nchi pekee Afrika Mashariki ambayo imehalalisha uzalishaji wa bangi, japo kwa matumizi ya kiafya. **BBC**



Viongozi wa kundi la mataifa saba yaliyoendelea zaidi kiviwanda (G7) wakiwa katika mkutano wa kilele wakijadili changamoto mbalimbali. **PICHA: AFP**

# Brazil 'yapiga teke' mabilioni ya G7

**BRASILIA,** Brazil

BRAZIL imekataa msaada wa kifedha wa dola milioni 20 wa kusaidia kuzima moto katika msitu wa Amazon kutoka kundi la (G7).

Nchi za kundi la mataifa saba yenye uchumi mkubwa wa viwanda lijulikanalo kama G7 zimeahidi msaada wa dola milioni 20 kupambana na moto huo wakati wakiwa katika mkutano wa kilele mjini Biarritz, Ufaransa.

Lakini Rais wa Brazil, Jair Bolsonaro alimwambia Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron ashughulikie nchi yake na makoloni yake. Rais Macron ambaye alikuwa mwenyeji wa mkutano huo, aliwasisitizia wenzake kuwa wanapaswa kuupa kipaumbele moto unaowaka katika msitu wa Amazon.

Mbali na fedha hizo, Uingereza kwa upande wake ilihaidi kutoa dola milioni 12, na Canada itatoa dola milioni 11 pamoja na ndege za kuzima moto.

Mkuu wa shughuli za ofisi ya rais wa Brazil, Onyx Lorenzoni (pichani) aliambia tovuti ya habari ya G1 kwamba wanashukuru lakini labda fedha hizo zitafaa



zaidi kupanda miti na kuimarisha misitu barani Ulaya, huku Rais Bolsonaro akisema hamna msaada unaotolewa bure.

"Macron ameahidi msaada kutoka nchi za kitajiri utumike Amazon. Kwa nini macho yao yote wameyaelekeza Amazon? Wanataka nini huko kwa muda mrefu?," alisema Bolsonaro.

Macron alimjibu Bolsonaro kwa kusema kwamba: "Japo kuwa sehemu kubwa ya Amazon imo ndani ya Brazil, lakini hili ni suala la ulimwengu na ujumbe wake kwa kiongozi huyo ni kwamba ulimwengu hautomruhusu kuangamiza kila kitu".

Waziri wa Mazingira wa Brazil, Ricardo Salles awali aliwaambia waandishi habari kwamba wanaukaribisha msaada wa nchi za G7 ili kuukabili moto huo unaoteketeza ekari milioni 2.3 katika msitu wa Amazon.

Lakini baada ya mkutano na Bolsonaro pamoja na mawaziri wake, serikali ya Brazil ilibadilisha msimamo wake. Ingawa asilimia 60 ya msitu wa Amazon imo ndani ya Brazil, msitu huo mkubwa unasambaa pia katika nchi nyingine nane ikiwa ni pamoja na Guiana iliyowahi kuwa koloni la Ufaransa na sasa ni sehemu ya Ufaransa kisiasa na kisheria.

Bolsonaro ambaye ni mkosoaji mkubwa wa suala la mabadiliko ya tabianchi amekabiliwa na ukosoaji kutoka nje na ndani ya nchi yake, kwa kuchelewa kwake kupambana na moto huo wa Amazon.

Wengi hawakufurahishwa na uongozi wake katika suala hilo. Nchini mwake hivi karibuni, maelfu ya watu walimiminika barabarani kukemea uharibifu huo unaoendelea katika msitu wa Amazon. **DW**

# NMB sasa yapeleka fursa ya ubadilishaji fedha Kaskazini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB Kanda ya Kaskazini, imefungua vituo vitano vya kutoa huduma za kubadilisha fedha za kigeni vitakavyokuwa wazi hadi siku za Jumapili na sikukuu ili kuwawezesha watalii na wananchi wengine kunufaika na huduma hizo.

Meneja wa benki hiyo Kanda ya Kaskazini, Aikansia Muro, alisema hayo juzi wakati akizungumza kwenye Jukwaa la Wafanyabiashara wanaonufaika kwa kupata mafunzo ya biashara na mikopo kutoka NMB kuwa mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara ina shughuli nyingi za utalii ambazo zinapaswa kupewa kipaumbele.

Muro alitaja vituo hivyo ambavyo vipo kwenye matawi ya benki hiyo ni Mbuyuni na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa (KIA) mkoa wa Kilimanjaro, Arusha Market na Clock Tower jijini Arusha na tawi lililopo wilayani Karatu ambako ni kituo muhimu kabla ya watalii hawajaingia kwenye Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Hifadhi ya Serengeti.

"Niwajulishe watoa huduma za utalii,wafanyabiashara ,watalii na wananchi kwa ujumla wavitumie vituo hivi kwa sasa wakati uongozi wa benki ukiangalia namna ya kuongeza maeneo mengine ili kuwezesha huduma ya kubadilisha fedha inafanyika kwa ufanisi zaidi kupitia benki yetu," alisema Muro.

Mkuu wa Wilaya ya Karatu, Theresia Mahongo, alisema uamuzi wa kutoa huduma za kubadilisha fedha siku za kawaida hasa Jumapili na sikukuu umepokewa kwa furaha baada ya maduka binafsi yaliyokuwa yakitoa huduma kufungwa na serikali kutokana na kukiuka taratibu za Benki Kuu ya Tanzania (BoT).

Katika hatua nyingine, alipongeza huduma za kijamii zinazotolewa na benki hiyo kuwa zimekua na msaada mkubwa katika huduma za afya na elimu wilayani kwake akitolea mfano Shule ya Sekondari Welwel na Kituo cha Afya Dabard.

"Sekta kubwa katika eneo hili ni utalii niwaombe NMB mshirikiane na wananchi wangu kukuza sekta hii ili iendelee kutoa mchango zaidi wa kiuchumi , niwaombe wafanyabiashara wajitokeze kuwekeza katika ujenzi wa hoteli na huduma nyingine ili watalii waongeze siku za kuwa hapa Karatu," alisema Mahongo.

Mkuu wa Kitengo cha Biashara wa NMB, Donatus Richard, alisema wamekuwa wakifanya mikutano na wafanyabiashara nchini kuwapa mbinu za kufanya biashara katika mazingira yenye ushindani na namna ya kutunza mahesabu ya biashara zao.

Alisema benki hiyo imeshatoa Sh. bilioni 600 kwa wafanyabiashara wadogo na Kati ambayo imekuwa na mchango muhimu katika uchumi nchini kwa kufungua fursa za ajira , uanzishwaji wa viwanda vidogo na ulipaji wa kodi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, akizungumza na Balozi wa Jamhuri ya Rwanda nchini Tanzania, Eugine Kayihura, alipofika Ikulu Zanzibar jana, kumuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi hapa nchini. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# Kongamano la wasomi kujadili tabianchi, usalama wa chakula

**Na Gwamaka Alipipi**

WANASAYANSI watafiti zaidi ya 300 kutoka ndani na nje ya Afrika wanatarajia kukutana nchini kujadiliana matokeo ya utafiti mbalimbali waliofanya kuhusu mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula.

Wasomi hao watakutanishwa katika kongamano litakaloandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Kigoda cha Mwalimu Nyerere cha Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi kwa kushirikiana na Taasisi ya Tathmini Rasilimali pamoja na Kituo cha Mabadiliko ya Tabianchi kuanzia Oktoba 8 hadi 10, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuhusu kongamano hilo, Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu Nyerere cha Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Prof. Pius Yanda, alisema mjadala utajikita katika kuainisha namna matokeo ya utafiti yanaweza kusaidia katika kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

Prof. Yanda alisema wanasayansi hao pia watajadiliana kuhusu usimamizi wa maliasili na mifumo yake ya ki-ekolojia katika kipindi chenye changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi.

"Kongamano litajikita katika maeneo makuu matatu, ubunifu wa teknolojia, katika usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi na usalama wa chakula, pamoja na usimamizi wa maliasili na mifumo ya ki-ekolojia katika kipindi chenye changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi," alisema Prof. Yanda.

Alisema mada kuu ya mkutano ni "Kuelekea kwenye jamii inayohimili changamoto za mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo endelevu".

Alisema wanasayansi hao wataweza kujadiliana kuhusu uchakataji, uzalishaji na uvunaji wa chakula, kwa kuangalia mustakabari wa nchi kwa miaka 10 hadi 20 ijayo.

Alisema watakuwapo pia watunga sera, viongozi wa juu kutoka serikalini pamoja na wanafunzi kutoka vyuo vikuu nchini.

# Marufuku ujenzi nyumba za tope, nyasi mjini

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKUU wa Mkoa wa Lindi, Godfrey Zambi (pichani chini), amewataka wananchi kubadili mtazamo wa maisha, ikiwamo kuachana na tabia ya kuishi kwenye nyumba za tope na nyasi maeneo ya mjini.

Badala yake amewashauri waelekeze mawazo na nguvu zao kwa kujenga kwa kutumia matofali na kuezeka kwa bati.

Alitoa ushauri huo alipokuwa akitatua mgogoro wa viwanja kwa wakazi waishio Mlandege, Kata ya Nachingwea na maeneo mengine katika Manispaa ya Lindi, uliodumu kwa takribani miaka mitano.

Mgogoro wa viwanja kwenye eneo hilo ulianza mwaka 2015, ambapo wananchi zaidi ya 65 wamejitokeza kuomba kupimiwa viwanja na kulipia gharama za upimaji kupitia aliyekuwa Mtendaji wa Kata hiyo, aliyetajwa kwa jina la Nguzo na mwenyekiti wa Mtaa huo, Chimbuli, bila kupewa wala kuonyeshwa.

Akizungumza na wananchi waliokuwa wamejitokeza, baada ya kusikiliza malalamiko yao, Zambi alisema mgogoro uliopo umechangiwa na mambo ya kisiasa kwa kila mmoja kutaka kuonyesha umwamba mbele ya mwenzake.

"Leo mgogoro huu umeisha kwa kila aliyelipia gharama za upimaji atapewa eneo lake," alisema Zambi.

Baada ya kueleza hayo, Zambi aliwataka walioomba kupatiwa viwanja wasimame upande mmoja wakiwa na stakabadhi zao, ambapo wananchi 65 walijitokeza na kuagiza kupewa viwanja vyao mara moja, huku akimuagiza Mkurugenzi wa Manispaa hiyo kufuatilia malipo kama yaliwasilishwa ofisini kwake.

Zambi akizungumza na wananchi hao, aliwasisitiza kutojenga nyumba zao kwa kutumia tope na nyasi, badala yake wajenge kwa kutumia matofali na kuezekwa kwa bati, na atakaeshindwa kufanya hivyo, atanyang'anywa na kupewa watu waliona uwezo wa kutekeleza hayo.

"Ndugu zangu hapa ni mjini, tena ni Manispaa, inatakiwa majengo yake yawe na hadhi sawa na Jina lenyewe," alisema Zambi.

Alisisitiza kuwa atakayeshindwa kutekeleza hilo ni vema akaondoka na kwenda kuishi maeneo ya vijijini na kuwapisha walio na uwezo wa kujenga nyumba bora na za kisasa kwa matumizi ya binadamu.



# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA NYUMBA INAUZWA**
Shamba ekari 13 lililopo Vikuruti barabara iendayo Bagamoyo lina matunda, maji ya dawasco na Kisima Kirefu. Piga simu: 0767 237404, 0715 237 404 na 0767 856900.

## NAFASI ZA KAZI

Anahitajika - Mhasibu na sales Lady
Sifa – Awe Mwanamke
Elimu – Diploma
Ofisi yetu ipo Posta – Dar es Salaam
Kwa Mawasiliano :- 0715 – 885 533


## NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311


**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….. OF 2019**
**In the matter of the Estate of the late AMARJEET SINGH SEMBI of Dodoma Municipality/City.**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY PARAMJEET SINGH SEMBI**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filled on or before the 10 Day of September 2019.
Date at Dodoma this 14TH day of August 2019

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA REGION

215392302

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA

AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.62 OF 2019
In the matter of the Estate of the late SIMON MESHAK of Mvumi Ilolo Area within Dodoma Region.
AND
In the matter of the application for letters of Administration by DANIELI MESHACK

**GENERAL CITATION**

(RULE 75 OF PROBATE RULES GN. 369 OF 163)
ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.


Objections to the grant should be filled on or before the 19 Day of September 2019.

Date at Dodoma this 6TH day of August 2019

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE

2153922202

## KUPOTEA KWA VYETI



**Fransisco Martin Mwamlima** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.1249/0082 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2010 katika shule ya Sekondari Simbega, Cheti cha Diploma kilichotolewa na Chuo cha Tanzania Institute of Accountancy (TIA) mwaka /20142015, Chuo cha degree chenye namba DSM/BPLM/15/33764 kilichotolewa na Chuo cha Tanzania Institute of Accountancy (TIA) mwaka 2017/2018.
**Polisi Taarifa: DAR/MBA/RB/241958**

115391902

## KUPOTEA KWA CHETI



**Hairika Mustafa Meli** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P-2861-0012** kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2015 katika Shule ya Sekondari Kauzeni.Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: MOR/MVO/234603/2019**

15388402

## KUPOTEA KWA PASSPORT/ HATI YA KUSAFIRIA



**Karen Emanuel Matee** anatangaza kupotea kwa hati ya kusafiria /Passport yenye namba **AB594692** iliyotolewa na Ofisi za Uhamiaji Dar es Salaam mwaka 2013. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: DAR/OST/RB/243198/2019**

15391402

## KUPOTEA KWA KADI

Khadija Zakaria Madawili anatangaza kupotelewa na kadi ta gari yenye namba ya usajili T134 DJP, gari aina ya TOYOTA ALTEZA, yenye chasis namba SX10-0050141, engeine namba 359441228. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
Polisi Taarifa:
**DAR/KV/RB/241379/2019**

15390802

IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 68 OF 2019
In the matter of the Estate of the late JOSEPHAT MWITA NYARUGEMBE
And
In the matter of the Application for letters of Administration by LUCIA HAMIDU

**GENERAL CITATION**

All persons claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or letters of Administration) is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before6th day of Septembe,2019.

The will of the said deceased is deposited and open for inspection of the court.

Date 26th day of August,2019

**Resident Magistrate**
**DODOMA** RESIDENT MAGISTRATE BODOMA REGION

215392402

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA MOSHI**
**WILAYA YA MOSHI**
**MAOMBI NA. 168/ 2018**

**MAMA YOHANA KIMARO**
**PAULO FABIAN MGOWI**
**FERDINAND A. ASSENGA…………… MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**
**URUSHIMBWE RURAL PRIMARY COOPERATIVE SOCIETY LIMITED**
**PASCAL ALOIS MALISA**
**MSUYA AUCTION MART……………MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**KWA: PASCAL ALOIS MALISA**

**POPOTE ULIPO**
Kwa kuwa mleta maombi ameleta madai ya kesi na yameelezwa katika nakala ya madai ambayo inapatikana katika Baraza la Ardhi na Nyumba Moshi.Shauri limepangwa kutajwa tarehe 02/0892019 saa mbili na nusu(2:30)asubuhi mbele ya Mheshimiwa Mwenyekiti P.J. Makwandi, hivyo unatakiwa kufika mahakaman wewe au mawakili wako.
ANGALIA: Kama hutohudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu Mahakama itasikiliza shauri hili na kutoa uamuzi upande mmoja.
Imetolewa na kutiwa saini na muhuri wa Baraza hili leo 20 mwezi August, 2019.

**MWENYEKITI**
MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA

115391802

## KUPOTEA KWA CHETI



**Salimu J. Saidi** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0110/0079 kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari ILBORU. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: LUS/RB/1313/2017**

114088502

## KUPOTEA KWA CHETI



**Samwel P. Yegella** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S/1888/0032 kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari St. Patrick Mission .Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: 236161**

15391002


**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie 0767 223 311

Nipashe
MWANGA WA JAMII



**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ADEBAYOR AMWAGA WINO KAYSERISPOR




**ANKARA,** Uturuki

NYOTA wa zamani wa Klabu ya Arsenal, Emmanuel Adebayor amesajiliwa na klabu ya Kayserispor ya nchini Uturuki kwa mkataba wa mwaka mmoja.

Mshambuliaji huyo wa kimataifa wa Togo alikuwa mchezaji huru baada ya kuondoka katika klabu ya Istanbul Basaksehir mapema kipindi cha majira ya joto baada ya kuitumikia kwa kipindi cha miaka mitatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 sasa amehamia kwa Kayserispor, ambayo ilimaliza nafasi ya 10 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ya Uturuki, Super Ligi, msimu uliopita.

Hiyo itakuwa ni klabu ya tisa kujiunga nayo katika maisha yake ya soka kwa Adebayor baada ya kucheza nchini Ufaransa, England na Hispania.

Kwa mara ya kwanza alihamia Ligi Kuu ya England mwaka 2006 akitua Arsenal kabla ya kujiunga na Manchester City mwaka 2009.

Alicheza pia katika klabu ya Real Madrid na Tottenham kwa mkopo kabla ya kusajiliwa moja kwa moja pale White Hart Lane mwaka 2012.

Aliichezea mechi 12 Crystal Palace mwaka 2016 na alifunga bao moja tu kabla ya kutimkia nchini Uturuki.

Awali ilidhaniwa kwamba, Adebayor angetangaza kustaafu kucheza soka la ushindani mwishoni mwa msimu uliopita alipomaliza mkataba wake.

# Pogba azungumzia kubaguliwa kwake

**MANCHESTER,** England

PAUL Pogba amesema kwamba, suala la kubaguliwa kwake kwa sababu ya rangi yake limempa nguvu ya kuwa imara.

Pogba alishambuliwa kwenye mitandao ya kijamii baada ya kushindwa kufunga penalti katika mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Wolves. Mchezo huo uliokuwa wa pili kwao ulikamilika kwa sare ya kufungana bao 1-1 siku ya Jumatatu.

Pia, Jumamosi nyota mwingine wa United, Marcus Rashford alikosa Penalti Uwanja wa Old Trafford wakati wakikubali kupoteza kwa mabao 2-1 dhidi ya Crystal Palace.

Pogba amesema: "Ndugu zangu na kizazi changu kilichopita kilipambana kwa ajili ya kuleta uhuru kwenye kazi, mabasi pamoja na mambo mengine, hivyo sioni taabu kupambana kwa ajili ya haki yangu.

"Ubaguzi wa rangi kwangu naona ni ujinga na unapoteza muda kufanya mambo makubwa," alisema.






# Kane alalamika kunyimwa penalti

**LONDON,** England

HARRY Kane amesema "ni ngumu kuelewa" namna alivyonyimwa penalti wakati Tottenham ikifungwa na Newcastle na anaamini VAR ilitakiwa kubadilisha maamuzi.

Kane alionekana kuangushwa chini na beki wa Newcastle, Jamaal Lascelles katika dakika 10 za mwisho wakati wakifungwa 1-0 Jumapili na mwamuzi Mike Dean aliionyesha kuendelea kwa mchezo.

"Ni ngumu kuelewa namna ilivyotokea," alisema Kane. "Kama ilivyo kwa golikipa akija mbele yako na kukuzuia kwa mikono inakuwa ni penalti.

"Na ndivyo Lascelles alivyofanya. Nilipaswa kupewa penalti, kwa sababu aliniangusha kwa kutumia nguvu.

"Kulikuwa na VAR kwa ajili ya kumsaidia mwamuzi, lakini hakuna kilichotokea."

Kane anaamini kwamba alipaswa kupewa penalti na kwamba mchezo huo ungekuwa na matokeo tofauti.

"Nilikuwa na uhakika kabisa kwamba ile ilikuwa penalti, lakini mambo kama haya yanatokea kwenye soka, na matokeo huwa tofauti kabisa na matarajio."

## HABARI MICHEZO



# LUKAKU AANZA KWA KUTUPIA INTER MILAN

**MILAN,** Italia

MSHAMBULIAJI Romelu Lukaku alifunga wakati akianza kuichezea kwa mara ya kwanza Inter Milan kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, wakati wakiibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Lecce, chini ya kocha mpya, Antonio Conte.

Marcelo Brozovic na Stefano Sensi waliiweka mbele Inter kwa mabao 2-0 katika kipindi cha kwanza, kabla ya Lukaku, aliyesajiliwa kutoka Manchester United mwezi huu, kufungua akaunti yake ya mabao.

Antonio Candreva alikamilisha idadi hiyo ya mabao kwa kufunga kwa shuti kali umbali wa yadi 35.

Inter ilimteua Conte kuwa kocha wake, ambaye aliwahi kushinda mara tatu taji la Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akiwa na Juventus na pia alishinda taji la Ligi Kuu ya England akiwa na Chelsea.

Alitua hapo Inter kuchukua nafasi ya Luciano Spalletti ambaye alitimuliwa baada ya kukaa misimu nane bila kupata taji lolote.

# Dembele chambo ya Barca kwa Neymar

**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona imetoa ofa mpya kwa PSG kwa ajili ya kumnyakua staa wao wa zamani, Neymar na imeongeza dau la fedha pamoja na Ousmane Dembele kwa ajili ya kumnasa nyota huyo wa kimataifa wa Brazil.

Hiyo ni baada ya PSG kupiga chini ofa zaidi ya nne za Barcelona walizowasilisha kwa ajili ya kumsajili mchezaji wake huyo wa zamani ambaye alitua hapo Paris miaka miwili iliyopita kwa ada iliyoweka rekodi ya dunia.

Dili hilo huenda likaishawishi PSG kuachana na Neymar na kumuunganisha Dembele na nyota mwenzake wa kimataifa wa Ufaransa, Kylian Mbappe katika safu ya ushambuliaji ya mabingwa hao wa Ufaransa.

Barcelona na Real Madrid zinapambana kuiwahi saini ya Neymar ambaye inadaiwa kwamba hataki kuendelea kukipiga Ufaransa huku mabosi wake wakiwa tayari kuachana naye katika dirisha hili kutokana na kuchoshwa na tabia zake.

Awali klabu hizo zilituma ofa zao ili kumnasa staa huyo wa kimataifa wa Brazili lakini PSG ilizipiga chini. Mara ya mwisho PSG ilizitaka Barcelona na Real Madrid kuwasilisha ofa zao za mwisho mchana wa Septemba Mosi kabla dirisha kufungwa Septemba 2, mwaka huu.



# Klopp: Aanza kuaga Liverpool



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema kwamba anatarajia kupumzika kufundisha soka mara tu baada ya kumaliza mkataba wake na mabingwa hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Klopp, ambaye alijiunga na Liverpool mwaka 2015 na ana mkataba hadi mwaka 2022, aliiongoza klabu hiyo kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita na ikimaliza nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu, ikipitwa pointi moja tu na mabingwa Manchester City.

Alipoulizwa na Gazeti la Ujerumani la Kicker kama atachukua mapumziko baada ya kumaliza mkataba wake na Liverpool, Klopp alisema: "Inaonekana hivyo. Nani anaweza kusema naweza kuendelea na miaka yote mitatu?

"Kama nikiamua mwenyewe, sitaweza kuendelea, nitachukua likizo na ninataka kuchukua maamuzi mazuri.


"Nina nguvu, lakini nina tatizo moja: Siwezi kuendelea kufanya wakati nikitaka kupumzika.

"Naamini baada ya mapumziko nitakuwa na nguvu zaidi na hapo nitaweza kufanya kazi nipendavyo."

Kabla ya kujiunga na Liverpool, Klopp alifurahia wakati wake pale Borussia Dortmund, ambako alishinda mataji mawili ya ligi pamoja na lile la DFB Pokal, pia akifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2013.

Liverpool, ambayo haijawahi kushinda taji la Ligi Kuu England tangu mwaka 1990, inaongoza msimamo wa ligi hiyo baada ya kushuka dimbani mara tatu.

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MARTIAL AMSUBIRISHA SANCHEZ MAN UNITED

●●● Hilo sasa ni pigo kwa nyota huyo mwenye matumaini ya kujiunga na Inter...

**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United itasubiri kuangalia majeraha ya Anthony Martial yatachukua muda gani kabla ya kuamua kumruhusu Alexis Sanchez kujiunga na Inter Milan, kwa mujibu wa ESPN FC.

**Martial aliumia nyama za paja wakati Man United ikifungwa mabao 2-1 na Crystal Palace katika dimba la Old Trafford Jumamosi.**

Mfaransa huyo mwenye umri wa miaka 23, ambaye msimu huu amefunga mara mbili, atafanyiwa uchunguzi zaidi wiki hii ili kujua ni kwa kiasi gani ameumia.

Hilo ni pigo kwa Sanchez mwenye matumaini ya kujiunga na Inter kabla ya kufungwa kwa dirisha la usajili Septemba 2, mwaka huu.

Miamba hao wa Italia wanajaribu kukubaliana kumchukua raia huyo wa Chile kwa mkopo huku kukiwa na kipengele cha kumnunua moja kwa moja hapo Januari.

Kwa mujibu wa ESPN FC, klabu hizo mbili bado hazijafikia makubaliano na sasa kinachosubiriwa ni majaliwa ya Martial kujua ukubwa wa majeraha yake yatachukua muda gani.

Romelu Lukaku tayari ameondoka na kujiunga na Inter na kuiacha Man United ikiwa na washambuliaji watatu pekee mbele ambao ni Martial, Marcus Rashford na kinda Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 17.

Hata hivyo, Sanchez bado hajacheza mchezo wowote msimu huu wakati akiendelea kupona majeraha ya misuli. Sanchez amefunga mabao matano tu katika mechi 45 alizoichezea klabu hiyo tangu alipojiunga akitokea Arsenal Januari mwaka 2018.

## ZISIKUPITE

### DE BRUYNE AMTULIZA KOMPANY

KEVIN De Bruyne amemtaka mchezaji mwenza wa zamani wa Manchester City, Vincent Kompany kuzima kukosolewa na kupata mafanikio katika majukumu yake mapya kama kocha wa Anderlecht, wakati huu akiwa amevuna pointi mbili tu katika mechi nne za mwanzo wa msimu. ***(Manchester Evening News)***

### PSG YAKOMAA KWA VINICIUS JR

PARIS St-Germain imeiambia Real Madrid watazingatia tu kumuuza nyota wa kimataifa wa Brazil, Neymar, 27, kama klabu hiyo ya Hispania itamjumuisha straika Mbrazil Vinicius Jr, 19, kama sehemu ya mpango huo wa kudumu. ***(AS)***

### NEYMAR AKALIWA KIKAO BARCA

WAKURUGENZI wa Barcelona walikutana Jumatatu kujadili kutoa ofa kwa mshambuliaji wao wa zamani, Neymar. ***(Marca)***

### BONY KUGEUKIWA INTER

INTER Milan inaweza kumgeukia mshambuliaji wa Manchester City Wilfried Bony, 30, nyota huyo wa kimataifa wa Ivory Coast kwa sasa hana klabu baada ya kuachwa na Swansea majira ya joto. ***(Goal.com)***

### MATIC AMVAA SOLSKJAER

NYOTA wa kimataifa wa Serbia, Nemanja Matic, 31, amehitaji mazungumzo na kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer baada ya kupoteza nafasi katika kikosi cha kwanza pale Old Trafford. ***(Mirror)***

### ARSENAL, NACHO KUACHANA

ARSENAL inajiandaa kumruhusu Mhispania Nacho Monreal kujiunga na Real Sociedad wiki hii kama beki huyo mwenye umri wa miaka 33 ataomba kuondoka. ***(Sun)***

### CHELSEA KUMFUNGA ABRAHAM

MSHAMBULIAJI wa Chelsea, Tammy Abraham yupo mbioni kulamba mkataba mpya ambao utakuwa zaidi ya mara mbili ya mshahara wake wa pauni 50,000 anazozipata kwa wiki. ***(Telegraph)***

### ERIKSEN KUIGOMEA SPURS

WAWAKILISHI wa Christian Eriksen hawatazingatia mshahara wa pauni 200,000 kwa wiki ambao Tottenham inataka kumpa nyota huyo wa kimataifa wa Denmark ambaye mkataba wake unamalizika majira ya joto yajayo, kwa sasa anataka kutimkia Hispania. ***(Mirror)***

### DYBALA KUBISHANA ICARDI

INTER Milan na Juventus rasmi zimefanya mawasiliano kuhusu uwezekano wa dili la kubadilishana mshambuliaji Muargentina Mauro Icardi, 26, na Paulo Dybala, 25. ***(Gazzetta dello Sport - in Italian)***

### SHAW MWEZI NJE UNITED

BEKI wa Manchester United, Muingereza Luke Shaw, 24, anakabiliwa na kukaa nje ya uwanja kwa kipindi cha mwezi mmoja kutokana na majeraha ya misuli. ***(Talksport)***

### GRACIA AHAHA WATFORD

JAVI Gracia anahaha kuokoa kibarua chake cha kuendelea kuinoa Watford baada ya kuanza msimu wa Ligi Kuu England kwa vipigo vitatu mfululizo. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## Stars kambini leo

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania (Taifa Stars), inatarajia kuingia kambini leo kujiandaa na mchezo wake wa kuwania kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya timu ya Taifa ya Burundi ugenini Septemba 4 kabla ya kurudiana Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam Septemba 8, mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wilfred Kidau, alisema maandalizi kwa ajili ya mchezo huo yanaendelea vizuri wakishirikiana na serikali kuhakikisha Taifa Stars inaifunga Burundi.

Aidha, alisema kwa upande wa wachezaji wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi tayari wamewatumia tiketi zao ili kuja kujiunga na wenzao lengo likiwa ni kuhakikisha wanashinda mechi hiyo na kusonga mbele.

"Tunaupa umuhimu mkubwa mchezo huo kuhakikisha tunarudi nyumbani na ushindi ndio maana tunaendelea kufanyia kazi programu ya mwalimu," alisema Kidau na kufafanua kuwa mechi ya marudiano kiingilio kitakuwa chini ili kuvutia mashabiki kwenda kuishangilia Stars, na kwa mechi ya ugenini msafara wa wachezaji na wahamasishaji utaelekea Burundi Agosti 31 ukiwa na waandishi wa habari 35.

## Brazuka Marathon kutibu watoto 512

**Na Mary Geofrey**

TAASISI za kifedha 19 nchini zimeandaa mbio za kilometa 10 hadi 15 zijulikanazo kwa jina la 'Brazuka Marathon' zenye lengo la kuchangisha fedha zitakazotumika kwenye matibabu ya watoto 512 wenye umri chini ya miaka mitano ambao wanakabiliwa na tatizo la moyo.

Mbio hizo zinatarajiwa kufanyika Septemba 15, mwaka huu na mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Mratibu wa Brazuka Marathon, Nasikiwa Berya, wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya Uzinduzi wa Brazuka Kibenki Marathon 2019, alisema mbio hizo zitaanzia katika viwanja vya michezo vya Jakaya Kikwete Youth Park.

Alisema watapita mtaa wa Kiungani kupitia Central, Kivukoni, Barabara ya Barack Obama, eneo la Palm Beach na Upanga kisha kurudi katika viwanja vya michezo vya Jakaya.

"Lengo lingine la kuandaa mbio hizi ni kuwasaidia watoto ambao familia zao hazijiwezi kiuchumi na wapo katika Taasisi ya Moyo ya (JKCI) wakisubiri matibabu ili kurudisha faraja na tabasamu kwa wazazi na ndugu zao wanaowauguza," alisema Berya na kufafanua kuwa wanatarajia zaidi ya washiriki 5,000 watajitokeza na takribani Sh. milioni 10 zitapatikana.

# WASHINDI MILIONI 825/- ZA SPORTPESA WAFUNGUKA

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE washindi wawili wa Sh. 825, 913, 640 za Jackpot Bonus ya SportPesa wamewasili jijini Dar es Salaam na kukabidhiwa mamilioni yao huku wakifunguka kuhusu ushindi wao.

**Washindi hao, Kingsley Pascal kutoka Biharamuro mkoani Kagera na Magabe Marwa wa Mugumu, Serengeti wamegawana kiasi hicho ambapo kila mmoja ameibuka na Sh. milioni 412 kitita hicho wakikipata kutokana na wote wawili kubashiri kwa usahihi mechi 13 wikiendi iliyopita.**

Akizungumza na waandishi wa habari, Pascal ambaye ni mtumishi wa umma, alisema alianza kubashiri na SportPesa tangu mwaka 2017 kabla ya wikiendi iliyopita kushinda.

Pascal alisema huo ni ushindi wake wa kwanza kuupata tangu aanze kubashiri na kushinda, hivyo anajisikia furaha.

"Leo Jumatatu ndiyo nimeanza kuamini kuwa nimeshinda rasmi licha ya kupewa taarifa na SportPesa nikiwa nyumbani Kagera.

"Niwaambie Watanzania kuwa hili jambo la ukweli kabisa na mimi ndiye mshindi halali wa Jackpoti hii kubwa ya SportPesa.

"Hivyo niwatake Watanzania wote kuanza kubashiri na SportPesa ili washinde Jackpot Bonus mpya ya Sh. milioni 200, " alisema Pascal.

Kwa upande wa mama yake mshindi huyo, Marry Soud, alisema: "Nilikuwa siamini michezo hii ya kubashiri, lakini baada ya ushindi huu wa mwanangu ndiyo nimeanza kuamini.

"Mwanangu muda mrefu nilikuwa namzuia kucheza michezo hii, lakini baada ya ushindi huu nawashauri vijana wengine wacheze na SportPesa," alisema Marry.

Kwa upande wa Marwa yeye alisema amepokea kwa furaha kubwa ushindi wake baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 13.

"Nianze kwa kuwashukuru SportPesa kwa kuniwezesha kubadilisha maisha baada ya ushindi nilioupata. Niliweka mkeka wa shilingi 2,000 ambao umeniwezesha kupata mamilioni, hivyo ninafuraha kubwa ambayo ninashindwa kuielezea.

"Hizi fedha nilizozipata nimepanga kuzifanyia mengi makubwa ni mapema kuanza kuweka wazi muda huu, acha kwanza nikakae na familia yangu baada ya hapo nitajua maana hizi fedha ni nyingi," alisema Marwa.



Mshindi wa Sh. milioni 412 za JackPot ya SportPesa, Magabe Marwa kutoka Mugumu, Mara akizungumza na vyombo vya habari baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Julius Nyerere jijini Dar es Salaam jana na kupokewa na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas (wa tatu kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Makocha Uganda, Burundi watambiana*

**Somoe Ng'itu,** ASMARA

TIMU ya soka ya vijana ya umri chini ya miaka 15 (U-15) ya Uganda inatarajiwa kuwavaa yosso wenzao wa Burundi katika mechi ya hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Asmara nchini Eritrea.

Uganda itashuka uwanjani kuikabili Burundi ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zake zote nne za hatua ya makundi za Kundi B wakati Burundi iliyokuwa Kundi A yenyewe ilishinda mechi tatu na kutoka sare mchezo mmoja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa kikosi cha Uganda U-15, Magwera Jackson, alisema kikosi chake kimejipanga kuendelea kufanya vizuri katika mchezo wa leo na hatimaye kutinga fainali za michuano hii inayochezwa kwa mara ya kwanza kwenye ukanda huu.

Magwera alisema kila mechi kwao ni sawa na fainali, hivyo amewaandaa wachezaji wake kupambana kama walivyofanya katika michezo iliyotangulia.

"Tunataka kuendelea kufanya vizuri, tumejipanga kupambana katika mechi ya kesho (leo), kwa sababu malengo yetu ni kuchukua kikombe cha mashindano haya, hatutawadharau wapinzani wetu," alisema Magwera.

Naye Kocha wa timu ya Rwanda U-15, Vyes Rwamisaza, ambaye ataikabili Kenya, alisema wanatarajia kuwa na mechi ngumu na yenye ushindani, kwa sababu wamewaona wapinzani wao walivyopambana kwenye mechi zao za hatua ya makundi.

"Tumejipanga kufanya vizuri, tunajua mechi itakuwa ngumu na yenye ushindani, kila timu iliyoingia hatua ya nusu fainali si ndogo, wachezaji wake wameonyesha utulivu, na sisi tunataka kufanya vema kwa sababu tunataka kuwafurahisha watu wetu wa nyumbani," alisema Yves.

Lakhani Sal, Kocha wa Kenya (U-15), alisema vijana wake wako tayari kupambana na hatimaye kupata ushindi katika mechi hiyo ya hatua ya nusu fainali.


"Malengo yetu ni kuendelea kufanya vizuri, ni mashindano ambayo yamesaidia kuendeleza vipaji vya wachezaji wetu, lakini pia kupata ushindi na kuchukua kikombe, itatufanya kuwa na kumbukumbu nzuri kwa wachezaji na nchi pia, tunatarajia kuwa na mechi nzuri na yenye ushindani," alisema kocha huyo.

Mechi ya fainali ya mashindano hayo inatarajiwa kuchezwa keshokutwa Ijumaa na timu zitakazofungwa leo, zitakutana kuwania nafasi ya tatu.

# Michezo

Jumatano Agosti 28, 2019

Nipashe

Martial amsubirisha Sanchez Man Utd UKURASA 30



Kocha wa Simba, Patrick Aussems akiwa na kikosi chake mazoezini kwenye Uwanja wa Gymkhana jijini Dar es Salaam jana, ikiwa ni sehemu ya maandalizi kuelekea mchezo wao wa Ligi Kuu ya Vodacom dhidi ya JKT Tanzania utakaopigwa Uwanja wa Taifa kesho. **PICHA: SIMBA NEWS**

# Aussems: Hatuachi kitu Ligi Kuu na FA

●●● Hayakuwa matarajio yetu, mwaka uliopita tulikuwa na furaha, msimu huu tumekuwa na...

**Na Mwandishi Wetu**

NI kama moto ndiyo umewaka, kwani baada ya kung'olewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems, ameeleza hasira zote sasa wanazielekeza kwenye Ligi Kuu Bara na Kombe la Shirikisho la Soka nchini (maarufu FA Cup).

**Jumapili Simba iliaga rasmi michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu barani Afrika baada ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya UD Songo ya Msumbiji katika Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.**

Kwa sare hiyo, iliipa tiketi UD Songo kutinga raundi ya kwanza ya kufuatia suluhu waliyoipata katika mechi ya awali kwao Msumbiji, hivyo kusonga mbele kwa faida ya bao la ugenini.

Lakini Aussems, juzi na jana alikiongoza kikosi chake kufanya mazoezi kuelekea mechi yao ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu wa 2019/20 dhidi ya JKT Tanzania itakayopigwa Uwanja wa Taifa kesho, huku akieleza hawatarajii kubakiza kitu kwa kuwa sasa lengo lao ni kubeba mataji hayo mawili yenye heshima kubwa kwa ngazi ya klabu hapa nchini.

"Baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa malengo yetu sasa ni kufanya vizuri kwenye mashindano yote kuanzia Ligi Kuu, Kombe la FA na mingine ambayo tutashiriki, " alisema Aussems.

Alisema hakika hayakuwa matarajio yao, lakini hawana budi kwa sasa kugeukia Ligi Kuu na Kombe la FA, michuano ambayo itawapa tena nafasi ya kushiriki kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa ama Kombe la Shirikisho Afrika msimu ujao.

"Hayakuwa matarajio yetu, mwaka uliopita tulikuwa na furaha, msimu huu tumekuwa na huzuni," Aussems alisema.

Bingwa wa Ligi Kuu ndiye anayeiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa wakati mshindi wa FA Cup akipeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Kung'olewa kwa Simba ambayo msimu uliopita ilifika hatua ya robo fainali na kuongeza pointi kwa Tanzania hivyo Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kutoa nafasi nne kwa Tanzania Bara kwenye michuano hiyo ya Caf, sasa kunaifanya Yanga na Azam FC kupigania kulinda nafasi hizo nne kwa kufika mbali katika kinyang'anyiro hicho.

Yanga imetinga raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa kwa kuitoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1 na sasa itakutana na Zesco ya Zambia, wakati Azam FC iliyosonga mbele Kombe la Shirikisho Afrika kwa kuitoa Fasil Kenema ya Ethiopia kwa jumla ya mabao 3-2 sasa itakutana na Triangle FC ya Zimbabwe. Timu nyingine ya Tanzania Bara iliyoaga Kombe la Shirikisho ni KMC FC iliyong'olewa na AS Kigali ya Rwanda kwa jumla ya mabao 2-1.

# Yanga: Lwandamina hatujui, atapata tabu

**Na Mwandishi Wetu**

LICHA ya mashabiki wa soka nchini kuhofia kocha wa zamani wa Yanga, Mzambia George Lwandamina kwamba anaweza kuwa kikwazo kwa klabu hiyo kusonga mbele kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, wametakiwa kuondoa shaka kabisa kwa sababu hii ni "Yanga mpya".

Yanga ambayo imetinga raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa kwa kuitoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1, sasa itakutana na Zesco ya Zambia inayonolewa na Lwandamina, ambayo imeitoa Green Mamba Eswatini kwa jumla ya mabao 3-0. Hata hivyo, Mwenyekiti wa Klabu ya Yanga, Dk. Mshindo Msolla amesema Yanga hii ni mpya na hawana hofu na Lwandamina kuhusu suala la kuijua vema wakati watakapokutana katika michuano hiyo.

Msolla alisema, wachezaji waliopo kikosi cha kwanza cha Yanga ambao Lwandamina anawafahamu si zaidi ya wawili ama watatu, jambo ambalo ana uhakika haliwezi kuwa sababu ya kumhofia kocha huyo.

"Hii ni Yanga mpya, wachezaji wengi ni wapya na ambao Lwandamina anawafahamu sana wanaweza wasizidi wawili na zaidi Kelvin Yondani, hivyo hiyo haiwezi kuwa sababu ya kumhofia," alisema.

Yanga itaanzia nyumbani Septemba 13 kabla ya kuifuata Zesco nchini Zambia katika mechi ya marudiano Septemba 27, mwaka huu na mshindi wa jumla atatinga hatua ya makundi wakati timu itakayotolewa itaangukia mechi za mchujo ili kusaka tiketi ya kucheza hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002